

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**  
**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII**  
**IDARA YA KISWAHILI**

**UCHAMBUZI LINGANISHI WA MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HODIYA ZA  
WADIGO WA MSAMBWENI NA WASWAHILI WA JOMVU KUU**

**NA**  
**MWANARUSI LUNG'ANZI**  
**C50/85231/2016**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Idara ya  
Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**NOVEMBER 2022**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kingine kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi:

Tarehe: 16/11/2022

**MWANARUSI LUNG'ANZI**

C50/85231/2016

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini ya wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi: .....

Tarehe: ..... 16<sup>th</sup> NOV 2022

**PROF. RAYYA TIMAMMY**

(Msimamizi)

Sahihi: .....

Tarehe: ..... 16<sup>th</sup> NOV 2022

**PROF. KINEENE WA MUTISO**

(Msimamizi)

## **TABARUKU**

Kazi hii namtabarukia mamangu mzazi, marehemu Amina Juma ambaye alinishika mkono katika masomo yangu kutoka shule ya msingi hadi chuo kikuu bila kumsahau baba yangu marehemu Lung'anzi aliyehakikisha kuwa sikosi karo yangu tangu mwanzo hadi kilele cha masomo yangu. Mola awarehemu wazazi wangu wote wawili na roho zao azilaze mahali pema peponi.

## **SHUKRANI**

Tasnifu hii imekamilika kwa ukarimu, bidii na hisani za watu tofautitofauti walionishika mkono kuhakikisha ninatembea nao tangu mwanzo wa safari hii hadi kukamilika kwa utafiti huu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Profesa Rayya Timammy na Profesa Kineene wa Mutiso kwa maelekezo yao kuanzia mwanzo hadi tamati ya utafiti wangu. Mola awakirimie mahitaji yao hapa duniani na kesho ahera amin.

Ningependa pia kumshukuru Prof. Iribi Mwangi ambaye ndiye mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili na wahadhiiri wengine idarani kama vile Profesa John Hamu Habwe, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Basilio Mungania, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Mukhwana Ayub na Dkt. Mary Ndung'u.

Shukrani zangu ziwaendee wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja amba ni Fatma Ali Mohamed, Wafula, Gladys, Hyline, Tunu, Ndegwa, Opiyo, Iman Hudaa, Brenda, Bridget na marehemu Grace; Mola ampumzishe mahali pema peponi mwanafunzi huyu ambaye baada ya kufuzu tu katika shahada yake ya uzamili aliaga dunia.

Shukrani zangu za dhati zimwendee pia mume wangu, kipenzi changu, bwana Chimoche Hussein aliyesimama na kujitolea kuwa mlezi wa watoto nilipokuwa masomoni. Mola amjaalie kila la heri hapa duniani na kesho akhera. Nawashukuru watoto wangu Rama, Biasha, Hassan na kitinda mimba changu Shamim waliokuwa wakinipa moyo wa kuendelea na masomo yangu katika hali zote. Shemeji wangu wa rohoni Maximilla Omengo aliyenipa makazi kila niwapo masomoni chuoni; alihakikisha ninapata chakula na mahitaji yote ya muhimu. Mungu ambariki mwanamke huyu kwa moyo wake mkunjufu.

## **IKISIRI**

Nyimbo ni mojawapo wa vipera vyatia fasihi simulizi. Nyimbo huweza kutofautiana au kulingana katika jamii moja hadi nyingine kutegemea mazingira ya jamii maalum. Utafiti huu ulishughulikia uchambuzi linganishi wa maudhui ya nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Utafiti huu uliongozwa na msingi wa nadharia ya uhalisia ambayo inahusu ulinganishi wa mambo kama yanavyotokea katika mazingira anayoishi binadamu. Tuliongozwa na madhumuni manne ambayo ni: kwanza, kuonyesha iwapo kuna usawa katika maudhui ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, pili, kuonyesha tofauti za kimaudhui zilizopo kati ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, tatu, kubainisha namna dini ya kiislamu inavyojitokeza katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni na nne, kuchunguza ushirikiano na ujirani kati ya jamii hizi mbili, yaani jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni unavyoathiri nyimbo zao za kazi. Kulingana na data ya utafiti wetu tuligundua ya kwamba yapo maudhui yanayofanana katika nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na ambayo ni: ushirikiano, umasikini, busara, biashara na bidii na kukashifu uvivu. Vile vile, tulibaini kuwa yapo maudhui machache tu yanayotofautiana katika nyimbo zao za kazi kukiwemo maudhui ya heshima na stara kwa Wadigo wa Msambweni na kwa upande wa Waswahili wa Jomvu Kuu tuliona maudhui ya uvumilivu, ulafi na uroho. Utafiti huu ni wa nyanjani na hivyo tulikusanya data kwa kwenda kwa watafitiwa wetu ambapo tulishirikiana nao katika kufanya kazi na pia tulitumia kamera kurekodi video ya nyimbo walizokuwa wakizimba wakati wa kazi. Hatimaye, tulichanganua data iliyokuwa imepatikana kwa lugha ya nathari kwa kuzinakili nyimbo hizo kisha kuzitolea maelezo ya kiuchambuzi kulingana na madhumuni ya utafiti huu.

## YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU .....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI .....	v
YALIYOMO.....	vi
SURA YA KWANZA .....	1
1.0    Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	7
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	8
1.4    Maswali ya Utafiti.....	8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada .....	8
1.6 Upeo na Mipaka.....	10
1.7 Msingi wa Kinadharia.....	11
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada .....	14
1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nyimbo kwa Ujumla.....	14
1.8.2 Nyimbo za Aina Maalum .....	16
1.9 Mbinu za Utafiti .....	18
1.9.1 Njia za Kuteua Sampuli .....	18
1.9.2 Njia za Kukusanya Data.....	19
1.9.3 Uchanganuzi wa Data .....	19
1.10 Hitimisho.....	19
SURA YA PILI.....	21
NYIMBO ZA HODIYA ZA WASWAHILI NA WADIGO .....	21
2.0 Utangulizi.....	21
2.1 Nyimbo za Hodiya za Wadigo wa Msambweni .....	22
2.1.1 Nyimbo za Hodiya za Ukulima.....	22
2.1.2 Nyimbo za Hodiya za Kutwanga Nafaka.....	28
2.1.3 Nyimbo za Hodiya za Kusaga Mahindi .....	31

2.1.4 Nyimbo za Hodiya za Kusuka Makuti.....	35
2.1.5 Nyimbo za Hodiya za Uvuvi.....	37
2.1.6 Nyimbo za Hodiya za Kugema .....	40
2.2 Nyimbo za Hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu .....	42
2.2.1 Nyimbo za Hodiya za Uvuvi.....	43
2.2.2 Nyimbo za Hodiya za Ukulima.....	45
2.2.3 Nyimbo za Hodiya za Kugema .....	47
2.2.4 Nyimbo za Hodiya za Kusaga Mahindi .....	48
2.2.5 Nyimbo za Hodiya za Ufinyanzi.....	49
2.2.6 Nyimbo za Hodiya za Kutwanga Mahindi.....	52
2.2.7 Hitimisho.....	53
SURA YA TATU .....	54
MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HODIYA ZA WADIGO WA MSAMBWENI NA WASWAHILI WA JOMVU KUU.....	54
3.0 Utangulizi.....	54
3.1 Maudhui ya Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Wadigo wa Msambweni.....	54
3.1.1 Ushirikiano.....	55
3.1.2 Umasikini.....	57
3.1.3 Bidii na Kukashifu Uvivu .....	59
3.1.4 Biashara.....	62
3.1.5 Umuhimu wa Kupata Chakula.....	64
3.1.6 Heshima /Stara .....	65
3.1.7 Busara .....	68
3.2 Maudhui ya Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu.....	70
3.2.1 Umasikini .....	70
3.2.2 Ulafi au Uroho .....	72
3.2.3 Ushirikiano.....	74
3.2.4 Uvumilivu .....	76
3.2.5 Busara .....	77
3.2.6 Biashara.....	78
3.2.7 Bidii na Kukashifu Uvivu .....	79

3.3 Hitimisho.....	81
SURA YA NNE .....	82
KULINGANISHA NA KULINGANUA MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HODIYA ZA WADIGO NA WASWAHILI.....	82
4.0 Utangulizi.....	82
4.1 Kulinganisha Maudhui Yanayojitokeza katika Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni .....	82
4.1.1 Umasikini.....	82
4.1.2 Ushirikiano.....	84
4.1.3 Bidii na Kukashifu Uvivu .....	86
4.2 Kulinganua Maudhui Yanayojitokeza katika Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni .....	89
4.2.1 Maudhui ya Ulafi .....	89
4.2.2 Maudhui ya Uvumilivu .....	90
4.2.3 Maudhui ya Heshima .....	91
4.3 Hitimisho.....	91
SURA YA TANO .....	93
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI .....	93
5.0 Utangulizi.....	93
5.1 Muhtasari wa Utafiti .....	93
5.2 Mahitimisho ya Utafiti .....	95
5.3 Changamoto za Utafiti .....	97
5.4 Mapendelekezo .....	97
MAREJELEO .....	99
DATA YA UCHANGANUZI .....	101
VIAMBATISHO VYA NYIMBO ZA HODIYA ZA WADIGO NA WASWAHILI .....	104

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Nyimbo zina umuhimu mkubwa katika jamii ya kiafrika. Waafrika huhusisha nyimbo mbalimbali na shughuli ambazo wanazifanya. Nyimbo za kitamaduni hupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine hasa zile zinazohusishwa na miviga mbalimbali. Nyimbo za aina hii huelezea historia ya jamii husika na kuonyesha miiko na mbeko za jamii husika. Ni kwa sababu hii basi tunasema kuwa nyimbo huelezea historia ya jamii fulani na ndiposa ni muhimu kuzifanyia utafiti ili kuonyesha matumizi yake katika jamii ya Waswahili na Wadigo. Zipo nyimbo mbalimbali ambazo huimbwa na jamii za kiafrika zikiwemo: nyiso, mapenzi, arusi, siasa, nyimbo za watoto, bembelezi na mbolezi. Nyimbo hizi huimbwa wakati mwafaka kwa kufungamana na shughuli za wakati maalum. Katika utafiti wetu tunazingatia nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.

### 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu unahu uchambuzi linganishi wa maudhui ya nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Utafiti wetu unakitwa katika fasihi simulizi. Kulingana na Matei (2011) fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia lugha kuwasilisha ujumbe unaomhusu mwanadamu kwa njia ya masimulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi simulizi ni sanaa iliyo na tanzu mbalimbali kama vile, hadithi, ushairi simulizi, mazungumzo na semi. Tanzu hizi za fasihi simulizi zina vipera mbalimbali ambavyo hupangwa kulingana na sifa zao. Nyimbo zinapatikana katika utanzu wa ushairi simulizi pamoja na ushairi wenyewe. Nyimbo hulingana kwa kiasi fulani na hata hutofautiana kutegemea na jamii husika. Mwingiliano huu unaweza kuwa wa kimaudhui, kimtindo au hata aina za wahusika. Kwa mujibu wa Matei (2011) nyimbo hubainishwa kwa kuangazia matumizi yake ya lugha, tamathali za usemi kama vile sitiari na tashbihi. Lugha ambayo hutumiwa katika nyimbo huingiliana na aina ya wimbo kama vile, nyimbo za hodiya ambazo ni za kazi huwa na maneno ambayo yanahu kazi husika na pia hutazamiwa kutekeleza majukumu mahsus kama vile kukejeli, kuhamasisha na kuburudisha. Nyimbo zina majukumu muhimu katika jamii na ndio maana tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu nyimbo kama vile nyimbo za sherehe za harusi, sherehe za jando, za mazishi na hata za mapenzi. Tafiti hizi za nyimbo zimefanywa katika jamii mbalimbali hasa za kiafrika na kuonyesha tofauti na mwingiliano uliopo baina ya nyimbo hizo.

Katika utafiti wetu tunashughulikia nyimbo za hodiya za Waswahili na Wadigo. Ili kuelewa jamii zinazohusika katika utafiti huu ni muhimu kuangalia mambo kadhaa yanayohusu jamii hizo kama vile asili yao, maeneo yao ya kijiografia na shughuli wazifanyazo. Binadamu hutumia lugha kuelezea hisia zake. Hisia hizo zinaweza kuwasilishwa kuitia kwa masimulizi, misemo na hatu nyimbo. Hisia za binadamu zinahusiana na mazingira anamoishi, shughuli za kijamii, imani za jamii husika na mambo yanayoendelea kwa wakati husika. Kwa kuangazia historia, nyimbo huimbwa kama njia mojawapo ya mawasiliano; sio lazima mtu azungumze bali anaweza kuitisha ujumbe wake kwa njia ya nyimbo. Kwa hivyo basi, mtu anaweza kuwasilisha hisia zake kuitia kwa nyimbo na ndiposa utafiti huu ni muhimu kwa kuwa unazingatia nyimbo za kazi za Waswahili na Wadigo. Kulingana na Spear (1978), Wadigo ni jamii mojawapo ya makabila tisa yanayokamilisha kundi la Wamijikenda. Spear anaendelea kusema kuwa asili ya Wamijikenda, ni Shungwaya katika bonde la mto Juba ambapo walishambuliwa na Wagalla. Mashambulizi haya ndiyo yaliwafanya Wamijikenda kuhamia pwani na kusambaa hadi Shimba hills na kusini magharibi mwa Mombasa ambapo walibuni kaya Kwale. Utengano ultokea baina yao na kuwafanya baadhi yao kuondoka na kuanzisha kaya Kinondo. Wadigo wengine waliondoka na kuelekea Msambweni ambako walianzisha kaya zingine ndogo ndogo kama kaya Dzombo huko maeneo ya Lungalunga na kaya Ngodo huko Mwanguda.

Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu wanajulikana kwa shughuli za ukulima na uvuvi. Jamii hizi mbili hufanya biashara za kuchuuza samaki baada ya kuvua kutoka bahari Hindi. Hii inaonyesha kuwa Wadigo na Waswahili hufanya shughuli zile zile na hivyo basi, nyimbo za hodiya zinaweza kuwa na mwingiliano mkubwa ingawaje zipo tofauti pia. Tofauti hizi zinatokana na kuwepo kwa imani tofauti baina ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Licha ya kuwepo kwa tofauti baina ya Wadigo na Waswahili, yapo mambo ambayo huwafungamanisha pia na ndio maana tunawatafiti ili kulinganisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo zao za hodiya. Mjumuiko huu wa Waswahili na Wadigo hasa katika biashara ulisababisha mwingiliano wa hali ya juu kati ya jamii hizi mbili. Ushirikiano wa kibiashara wa jamii hizi mbili uliletu pia ujirani wa karibu na kuwafanya kuwa na mambo ambayo yanawasawazisha. Msawazisho huu ulizua tashwishi katika kubainisha baina ya Udigo na Us wahili.

Mbali na ushirikiano wa kibiashara baina ya Wadigo na Waswahili, wote ni wafuasi wa dini ya Kiislamu. Inasemekana kuwa Wadigo na Waswahili walipojiunga na dini ya Kiislamu walikubali

utamaduni wake kiasi cha kuwafanya kusahau mila na tamaduni zao za jadi. Hali hii inathibitishwa kupitia mavazi yao yaliyobadilika na hasa ya wanawake. Wanawake wa Kiislamu huvaan mabuubui na kujifunga kanga mbili na pia wanavaa madera. Watoto wao vile vile huvalia majalbabu, wengine mitandio na suruali ndefu kwa wasichana. Majilbabu haya na suruali zake hufanana na kuwa kama ndizo sare zao za shule. Mara nyingi huwa suruali nyeupe na jalbabu jeupe kutegemea na sare za shule wanazosomea. Wavulana nao hata ikiwa bado wako shule za msingi huvaan suruali ndefu ili kusitiri miili yao. Hata iwe shule ni ya wanafunzi wa dini tofauti tofauti lakini wanafunzi wa Kiislamu mtu anaweza kuwatambua tu kwa kuangalia mavazi yao. Hii inatuthibitishia jinsi ambavyo wameiga mambo yanayohusishwa na dini ya Kiislamu. Tuligundua kuwa Wadigo na Waswahili husalimiana kwa kutumia salamu za Kiislamu na ambazo zinawafanya kuwa na mwonoulimwengu sawa. Hata watoto wadogo wakikutana na watu wakubwa husalimiana kwa salamu hizo hizo za dini ya Kiislamu kwa sababu hawapendelei salamu zao za jadi za ‘shikamoo’ kwa mdogo kumsalimia mkubwa na mkubwa kujibu ‘marahaba.’ Wanaume Waswahili na Wadigo huvaan saruni, kanzu na makubadhi hasa wakielekea msikitini. Wanaume hawa husalimiana kwa salamu za kiislamu, ‘Asalam aleikum warahamatulahi wabarakat’ kwa anayesalimia na anayejibu hujibu, ‘waalekum salam warahamatulahi wabarakat’. Tulibaini kuwa Wadigo na Waswahili hawasalimiani kwa urahisi kwa salamu zao za kiasilia na hili linaonyesha kuwa wamepokea dini na ndiposa wanafanya shughuli kama wafanyavyo wafuasi wa dini ya Kiislamu. Ndiposa tunasema kuwa Waswahili na Wadigo wameiga mambo mengi ya dini ya Kiislamu.

Tuligundua pia kuwa Waswahili na Wadigo hawaozwi kwa kufuata mila zao. Kwa mfano, kabla ya maingiliano baina ya Wadigo na Waswahili, mambo mbalimbali yalifanywa kwa bwana na bibi harusi ili ndoa ibarikiwe na kuashiria kuwa amekabidhiwa mke kirasm. Miviga iliyofanywa wakati wa harusi ya Wadigo ilikuwa kwamba bwana na bibi harusi waliketishwa mlangoni na kupewa mawaiidha. Bwana harusi alitemewa maji yaliyonywewa na mzee kisha kujitemea ye ye mwenyewe na baadaye kumtemea bibi harusi. Hata hivyo, baada ya muingiliano baina ya Wadigo na Waswahili, viviga hivyo vilibadilika na wakaanza kufuatia taratibu za dini ya Kiislamu. Utaratibu wa harusi za Kiislamu ni kuwa bwana anapeleka posa kwa msichana aliyemchagua baada ya kumpenda na kudhihirisha kwamba wako tayari kufunga ndoa na kuishi pamoja kama mume na mke. Baada ya wazazi wa bwana harusi kupeleka posa, utaratibu wa kupeleka vyakula ambavyo wanaitishwa na familia ya bibi harusi mtarajiwa, kukiwemo mchele, unga wa ngano, unga wa sima, viazi, dawa za pilau, maziwa, mafuta ya uto na vitunguu kama neti mbili.

Kulingana na Wadigo wa Msambweni ni desturi yao kwamba bwana harusi vile vile hutakiwa kutoa kima fulani cha pesa kama laki moja na nusu. Pesa hizi huwa zimeitishwa na wazazi wa msichana na kisha huibariki ndoa ya watoto wao. Pesa ambazo hulipwa kama mahari ya msichana hugawanywa kwa wazazi wote wawili ambapo kilemba ni cha baba na maziwa huwa ni ya mama. Wazazi hao huelewana wao wenyewe watagawanya pesa hizo viyi kwa kuwa hakuna kima maalum ambacho kimewekewa mama au baba. Isipokuwa kulingana na mazoea, baba hupata pesa zaidi ikilinganishwa na za mama. Bwana harusi pia hutoa mbuzi kama watatu na kamba zake; hizo kamba huwa ni bora zikiwa za leso ambazo zitavaliwa na mama yake msichana. Akina mama wenyewe hupendekeza leso za mali ya Abdalla. Kwao, hizo huwa na sifa na utamu wake wa kipekee wakijifunga. Kwa upande wa msichana, hiyo siku ya kupelekwa mizigo huwa kuna kikapu cha uchumba ambacho huwa ni nguo tofauti tofauti kama buibui, nikabu, dera, vitambaa vyta kushona marinda, leso, vitenge vyta kujifunga, sabuni na virembesho mbalimbali. Hivyo vitu akivipokea pia huwa kuna mtu wa kumpeleka chooni na kumtia maji ya uchumba siku hiyo, kumaanisha ya kwamba sasa ameposwa na hafai kuwa wazi na kuzunguka ovyo; anapaswa akitoka awe amevaa buibui na nikabu kujisitiri ili asije akatamaniwa na wanaume wengine. Hatimaye ndoa itakayofungwa hufuata taratibu za dini ya Kiislamu. Vile vile Waswahili na Wadigo hufuata taratibu za dini ya Kiislamu katika mambo kama vile mazishi na hili linaonyesha kuwa jamii hizi mbili zinazuata utaratibu wa dini moja na kuashiria mwengiliano baina yao.

Wadigo wa Msambweni mbali na kushirikiana na Waswahili wa Jomvu Kuu katika kufanya biashara wao ni wakulima wa jadi. Shughuli zao za kukidhi maisha yao ni kazi ya ukulima. Wao hulima nafaka mbalimbali kama mahindi, mchele, pojo na maharagwe. Vile vile, wao hujihusisha na kazi ya uvuvi hasa ikizingatiwa ya kwamba wanaishi kwenye ufuo wa bahari. Mbali na kazi hizo, wao pia wanajulikana kwa kazi ya ugemaji ikichukuliwa ya kwamba wao wanakuza minazi kwa wingi. Hizi ndizo kazi ambazo hufanywa kwa kiasi kikubwa na Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Wakati wa kufanya kazi hizi, Wadigo na Waswahili huimba nyumba zinazoingiliana na kazi husika ili kuwapa moyo wa kuendelea na kazi na kuondoa uchovu na kuwafanya kuendelea na kazi hadi watakapoimaliza.

Kulingana na Njogu na Chimera (1990) Waswahili kwa ujumla vyano vyao vilikuwa katika lugha za jamii ya Wabantu waliokuwa wakulima na ambao walifika pwani za bahari ya Hindi Kenya na kuishi huko. Wasemaji wao wa awali walikaribia wazungumzaji wa Kipokomo. Wazee hao wa Waswahili hatimaye waliunda vijiji kwenye pwani ambako waliendeleza shughuli ya uvuvi kisha

katika shughuli zao za biashara na uvuvi waligawanyika ambapo baadhi yao walibaki Lamu, wengine walienda Malindi na Mombasa. Waswahili waliupokea Uislamu kutoka kwa Waarabu wakati walikuwa katika shughuli za kibiashara. Kando na kuwa Waswahili na Wadigo ni wakulima, wavuvi na wagemaji, pia wanajulikana kwa ufinyanzi wa vyungu ambavyo huviuza mionganini mwao na pia kuvitumia kwa matumizi yao ya nyumbani. Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu wametunga nyimbo ambazo huziimba wakati wanapofanya kazi hizi mbalimbali na ambazo tutazishughulikia katika utafiti wetu. Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu kuu wanaishi katika eneo moja na hivyo basi ni majirani. Wote wanafuata desturi za dini ya Kiislamu, wanafanya kazi sawa na hivyo basi inakuwa vigumu kuwatofautisha. Hali hii inatupa ari na msukumo wa kutaka kufafanua na kujua ikiwa huo ushirikiano wao wa kila namna umeathiri hadi shughuli zao za kazi na pia iwapo nyimbo za hodiya zinatofautiana kutoka kwa jamii moja hadi nyingine. Katika utafiti huu tunanuia kuonyesha nyimbo za kazi za Wadigo na Waswahili zinaangazia maswala yepi na huwa na mwelekeo upi?

Nyimbo zina umuhimu wa kipekee katika jamii. Umuhimu huu wa nyimbo hutegemea aina ya wimbo na maudhui yanayojitokeza. Nyimbo ni kipera mojawapo cha utanzu wa ushairi simulizi na huwasilisha hisia za waimbaji. Wasomi mbalimbali wameweza kuelezea dhana ya nyimbo na inavyoolekea ni kuwa wote wanakubaliana kuwa nyimbo ni tungo zenye mapigo ya kimziki na ambazo huwasilisha ujumbe kwa lugha ya mkato. Wamitila (2008) ameshughulikia nyimbo na anasema kuwa,

“Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka.

Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na  
mapigo ya silabi, hupangwa kwa utaratibu au muwala  
wenye mapigo ya kimuziki au wizani.”

Wamitila anaonyesha kuwa nyimbo huibua taswira fulani na ndio maana waimbaji huteua wimbo wa kuimba kwa mujibu wa shughuli inayofanywa. Vile vile, Wamitila anaonyesha kuwa nyimbo huwasilishwa kwa utaratibu maalum kinyume na uwasilishaji wa hadithi. Ni kwa sababu hii ndio nyimbo huchukuliwa kuwa na nafasi kubwa katika shughuli za jamii mbalimbali. Tuseme kuwa shughuli nyingi na hasa za Waafrika hufungamana na nyimbo. Katika utamaduni wetu wa Kiafrika, nyimbo hupamba tamasha mbalimbali na kuzifanya zifane sana. Nyimbo hizi zina asili ya shughuli za binadamu na huzingatia miktadha mbalimbali ya shughuli hizo na huwa na

majukumu anuai. Kulingana na Wamitila (2003) nyimbo huwa na majukumu mbalimbali katika jamii yakiwemo:

- i. Huwa kama hifadhi ya mambo muhimu ya kihistoria kwenye jamii mbalimbali. Kwa mfano, kuna nyimbo na tenzi ndefu ndefu tu ambazo zinatupa kumbukumbu kuwahu su watu mashuhuri kama vile, Mwanakupona na Fumo Liongo.
- ii. Hutumiwa kama kiungo mahususi cha kupitisha thamani ya kiasili katika jamii mbalimbali na pia huashiria vipengele tofauti tofauti katika jamii hiyo husika.
- iii. Hutumiwa kama kiburudisho. Kwa hivyo ni njia ya kiburudisha na kutumbuiza wasikilizaji na waimbaji wenyewe. Hata katika sherehe za jando, harusi na hata mazishi, watu huimba, kujiburudisha au kuliwazana.
- iv. Hudhihirisha umbuji wa mila na desturi za jamii na huwa na muundo maalum wenye mnato wa lugha mahususi, ishara na picha. Mnato huu ndio hukifanya kipera cha nyimbo kuwa cha kipekee.
- v. Hutumiwa kama kihamasishaji cha kutenda mambo tofautitofauti katika jamii hasa nyimbo za siasa na za hodiya.
- vi. Aidha, nyimbo hutumiwa kama kichochezi cha hisia za kuchangamkia shughuli fulani, kwa mfano katika sherehe za harusi ambapo nyimbo hutumiwa kuongezea hadhira msisimko wa shughuli nzima.
- vii. Ni kipera muhimu cha kuelimisha na kupitisha maarifa mbalimbali mionganoni mwa wanajamii, na hivyo nyimbo huwa ni kiungo muhimu katika jamii.
- viii. Nyimbo ni akisiko zuri la kufurahia kwa walio na utamaduni huo.

Majukumu haya yaliyoelezwa na Wamitila yanaashiria kuwa nyimbo huwa na nafasi muhimu katika jamii kwa kuwa huwasilishwa kutegemea tukio linaloendelezwa. Katika utafiti wetu tunazingatia nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Hodiya ni nyimbo ambazo huimbwa wakati wa kufanya kazi. Matei (2011) anasema kuwa hodiya ni nyimbo za kazi kwa ujumla wake. Amezigawa nyimbo hizi za kazi zaidi kwa kutegemea shughuli mahususi. Anasema kuwa zipo hodiya za wavuvi ambazo anaziita kimai na vile vile wawe za wakulima. Hii ina maana kuwa nyimbo za kazi huwa za aina mbalimbali na maudhui yake hutegemea shughuli husika kama inavyobainika katika utafiti huu.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Waafrika kwa ujumla huwa na nyimbo zinazothibitisha mila na desturi zao mbalimbali. Wana nyimbo za nyiso, nyimbo za mbolezi, nyimbo za mapenzi, nyimbo za harus, nyimbo za bembelezi na nyimbo za kazi ambazo zinajulikana kama nyimbo za hodiya. Nyimbo hizo hubeba majukumu mbalimbali kulingana na jamii zinazohusika na kazi inayofanywa. Kwa mfano nyimbo za hodiya ambazo tunazishughulikia kwa mujibu wa mada ya utafiti wetu huwa na majukumu mbalimbali yakiwemo kuwatia moyo watu wafanye kazi kwa bidii, kuwahamasisha na kujenga maadili mema kwa wanajamii.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu nyimbo kama kipera cha fasihi simulizi. Kuna wale walio tafiti nyimbo za harus, nyimbo za siasa, nyimbo za watoto wa shule za chekechea, fani katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai, nyimbo za harus za wanawake wa Mombasa, nyimbo za harus za Wadawida na nyenginezo. Mbali na tafiti hizo zote, kwa ufahamu wetu nyimbo za hodiya za makabila ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni hazijafanyiwa utafiti. Kwa hivyo kuna umuhimu wa kufanya utafiti wa nyimbo za hodiya za jamii za Waswahili na Wadigo ili kuziba pengo lililowazi. Pili tunataka kuonyesha tofauti zilizopo za kimaudhui kati ya nyimbo hizi za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Tatu tunataka kuangalia jinsi dini ya Kiislamu inavyojitokeza katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu.

Kulingana na historia ya makabila haya mawili, yaani Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni ni kuwa hawa ni watu majirani walio na uhusiano wa kila aina; tuseme wanasadiana katika kutatua matatizo yao, hufanya sherehe zao pamoja, huwa wanaoana yaani msichana wa kidigo anaweza kuolewa na mvulana Mswahili kutoka Jomvu Kuu. Vile vile, Wadigo na Waswahili ni wafiasi wa dini moja ya Kiislamu na hivyo hifuata taratibu sawa katika shughuli zao mbalimbali. Swali ni je, ushirikiano wao utaishia hapa au hata umeathiri nyimbo zao za kazi? Kwa kuangazia maswali haya katika utafiti wetu tumepata mwelekeo wa maswali ya utafiti wetu. Swali hasa ni kuangalia ikiwa maudhui yaliyomo katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu yanafanana na yale maudhui yaliyomo kwenye nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni au la. Swali hili litatuwezesha kubaini maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni manne ambayo yanalenga kulinganisha na kulinganua maudhui yaliyomo katika nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Madhumuni hayo ni:

- i. Kuchunguza usawa uliopo baina ya maudhui ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.
- ii. Kubainisha tofauti za kimaudhui zinajitokeza kati ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.
- iii. Kueleza jinsi dini ya Kiislamu inaathiri katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.
- iv. Kufafanua namna ushirikiano na ujirani kati ya jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni unavyoathiri nyimbo zao za kazi.

### **1.4 Maswali ya Utafiti**

- i. Je, kuna uwezekano wa kuwepo kwa usawa wa kimaudhui kati ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni?
- ii. Je, tofauti zipi za kimaudhui zinajitokeza baina ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni?
- iii. Je, ni vipi dini ya Kiislamu inaathiri nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni?
- iv. Je, ushirikiano na ujirani wa Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu unaathiri vipi nyimbo zao za kazi?

### **1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Nyimbo za hodiya katika jamii nyingi za Waafrika zinafilia kwa sababu ya uvumbuzi wa teknolojia, hivi kwamba kazi ambazo zilikuwa zikifanywa na binadamu zinafanywa na mitambo. Watu wanatumia mashine na matingatinga kufanya kazi kama vile kutwanga mahindi, mchele, kusaga mahindi na kulima. Hii ina maana kuwa wakati wa kufanya kazi hizi, watu wanaoshughulikia mitambo ndio huwepo na huwa hawana wakati wa kuzungumza na wenzao kutokana na sauti inayotolewa na mitambo yenyewe. Nyimbo za hodiya huimbwa na watu

wanapofanya kazi kwa kutumia mikono yao, hasa wanaposhirikiana. Nyimbo za hodiya huimbwa zaidi watu wanapofanya kazi kwa kikoa. Nyimbo hizi huambatana na kazi husika na huwa na uamilifu mahususi kama vile kuondoa uchovu na kuwapa watu ari ya kuendelea na kazi. Ni kwa misingi hii basi ambapo tunasema kuwa nyimbo za hodiya ni muhimu na ndio maana tunafanya utafiti huu ili kuweka kumbukumbu ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Utafiti wetu utasaidia katika kuweka hifadhi maktabani kwa matumizi ya vizazi vijavyo ikizingatiwa kuwa utangamano baina ya watoto na wazee wao umepunguzwa kwa sababu ya elimu. Hii inaonyesha kuwa hodiya zitaendelea kusahaulika kadri miaka inavyosonga na basi vizazi vijavyo havitakuwa na ufahamu wa nyimbo za kitamaduni hasa zile za kazi. Kama tujuavyo fasihi simulizi kwa kawaida huwa haiandikwi bali huhifadhiwa akilini mwa fanani ambaye husimulia hadhira yake. Ingawa hivyo, kutokana na mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia, imekuwa vigumu kwa jamii kujumuika kama ilivyokuwa enzi za mababu kwa ajili ya kuendeleza fasihi simulizi. Kwa hivyo basi, utafiti wetu utasaidia katika kuhifadhi nyimbo za hodiya kwa ajili ya vizazi vya baadaye ambavyo huenda wasiwe na fursa ya kusikiza nyimbo hizi wakati kazi zinapofanywa, hasa ikizingatiwa kuwa wenyewe kuzijua wanaendelea kuisha. Tukizingatia ya kwamba vijana wa siku hizi hata hawapendi kuishi mashambani wote wanakimbilia mijini. Hizo nyimbo za kazi zinahitaji kuwekewa kumbukumbu ili vizazi vijavyo visikose kumbukumbu za mila na desturi za mababu zao.

Utafiti huu umekitwa katika nyanja ya fasihi simulizi ambayo inakusudiwa kuhifadhiwa akilini na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo. Kutokana na mabadiliko ya kijamii ambapo watu wanaishia kuhamia mijini kutafuta ajira, basi fasihi simulizi inaendelea kufifia. Utafiti huu utachangia kimawazo katika fasihi simulizi. Basi mawazo yetu yatatumika kuwaelimisha watu kutoka jamii mbalimbali na hasa Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu ambao wamehamia mijini watapata kuelewa sifa za nyimbo zao za hodiya. Tuseme tu kuwa tunataka kutoa mawazo ya kiusomi kuhusiana na nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Tukizingatia ya kwamba utanzu wa fasihi simulizi umo katika hatari ya kuangamia kwa kuwa haujaandikwa ila hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Watu wanakufa na hakuna anayejali ya kwamba hao wanaokufa wanaenda na ujumbe muhimu ambao kuupata tena ni vigumu ili urithishwe kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo basi, utafiti huu utawafaa sana wasomi wanaokaa mbali na pwani ambao wanataka kuzielewa nyimbo za hodiya za Waswahili na Wadigo wataweza

kuzipata maktabani kwa urahisi. Kwa njia hii, fasihi simulizi itakuwa inaendelezwa kwa vizazi vingi vijavyo.

Baada ya kusoma na kupitia tafiti tofautitofauti zilizoandikwa tuliona jamii mbalimbali zimefanyiwa utafiti kuhusu kipera cha nyimbo katika fasihi simulizi. Kuna tafiti kadhaa za nyimbo zilizofanywa za jamii ya Wataita, Wameru, Wamaasai na Wakikuyu. Katika jamii ya Wadigo kilichotafitiwa ni ulinganisho wa maudhui ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Vile vile nyimbo za harusi za wanawake Waswahili wa Mombasa pia zilifanyiwa utafiti. Nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni hazijafanyiwa utafiti. Ni pengo hili ndilo limetupa ari ya kutaka kufanya utafiti kuhusu ulinganisho wa kimaudhui wa nyimbo za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu.

## **1.6 Upeo na Mipaka**

Katika utafiti huu wa nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni tumejikita katika jamii ya Wadigo wanaoishi kusini mwa Mombasa, yaani kaunti ya Kwale. Hasa wale wa Msambweni. Hata ingawa Wadigo kwa ujumla wanapatikana katika sehemu mbalimbali kama vile Ng'ombeni, Ukunda, Tiribe, Tiwi na Shimoni. Lakini kwa sababu ya mtawanyiko huo wa kimazingira, imekuwa vigumu kutafitia kwote huko. Hivyo basi tumeshughulikia Wadigo wa Msambweni pekee ambao shughuli zao za kazi ni uvuvi, ukulima, na kugema. Vile vile tumeshughulikia nyimbo za kazi za nyumbani za wanawake kama vile kutwanga, kusaga mahindi na usukaji wa makuti. Waswahili kama walivyo majirani wao Wadigo, wanapatikana sehemu tofauti tofauti za Pwani kwa mfano kunao wanaoishi Lamu, Malindi, Jomvu, Pate, Vanga na Faza. Kwa sababu ya upana wa kimaeneo, itakuwa vigumu kutafiti tukitumia Waswahili wote wanaoishi katika hizo sehemu mbalimbali. Hivyo tumejikita kwa Waswahili wa Jomvu Kuu ambao wanajulikana kwa shughuli zao za ufinyanzi, uvuvi, ukulima na ugemaji.

Katika utafiti wetu, tulikusanya nyimbo tatu tatu kwa kila kazi. Aidha kazi ya ukulima, tutakuwa na nyimbo tatu za Wadigo wa Msambweni, nyimbo tatu za kazi ya kugema na nyimbo tatu za kazi ya uvuvi. Kwa ujumla, tutakuwa na nyimbo tisa za kazi za wanaume. Kazi za wanawake wa Kidigo nazo pia tunakusanya nyimbo tatu za kutwanga, nyimbo tatu za kusaga mahindi na nyimbo tatu za kusuka makuti. Kwa ujumla, zote zitakuwa ni nyimbo kumi na nane. Vile vile katika kuangalia hizo nyimbo tunazozifanyia utafiti, tumezingatia wanaume na wanawake wenye takriban miaka hamsini na zaidi. Hao ndio watafitiwa wa utafiti na ambao tunajua kuwa wana tajriba ya fasihi

simulizi hasa kuhusiana na nyimbo zetu za kazi. Ni wazi kwamba hatungefaulu tukijikita kwenye vijana wa siku hizi wa makamu ambao hawana hata uelewa wa nyimbo za hodiya.

Katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu, pia nao tulikusanya nyimbo tatu za ukulima, nyimbo tatu za ugemaji na nyimbo tatu za uvuvi kwa upande wa wanaume. Kwa upande wa wanawake, tumekusanya nyimbo tatu za kutwanga mahindi, nyimbo tatu za kusaga mahindi na nyimbo tatu za kufinyanga vyungu. Kwa ujumla, tuna nyimbo kumi na nane. Utafiti huu umetegemea wazee wanaume kwa wanawake wenye umri wa miaka hamsini na zaidi vile vile. Kwa hivyo utafiti wetu umekuwa na mkusanyiko wa nyimbo thelathini na sita. Nyimbo zenyewe tumeziteua kimaksudi na ambazo zinatuwezesha kuafikia madhumuni ya utafiti wetu.

### **1.7 Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu ni wa kiusomi na hivyo basi umekitwa kwa msingi wa nadharia ambayo itatuwezesha kuafikia madhumuni yetu ya utafiti. Kwa mujibu wa Massamba (2007) nadharia ni utaratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo. Hivyo basi nadharia ni sayansi inayohusiana na kanuni za kijumla zitumiwazo katika utafiti wa kazi fulani. Msomi huyu anaonyesha kuwa nadharia ni muhimu katika utafiti kwa kuwa humuongoza mtafiti katika kujibu swali lake la utafiti.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia huangazia mambo kama vile maudhui ndani ya kazi ya kifasihi, urahisi wa kazi yenyewe na uhalisia ambao hubadilikabadilika kwa sababu ya mabadiliko ya kijamii na kimazingira. Nadharia ya uhalisia basi inaendana na matukio yanayoendelezwu katika jamii. Nadharia ya uhalisia ni nadharia itumiwayo kuelezea hali ilivyo katika jamii mahususi. Katika utafiti huu, tunaangazia maudhui katika nyimbo na ndiposa tuliteua nadharia ya uhalisia kama msingi wa kazi yetu. Nyimbo ni kipera cha ushairi simulizi katika fasihi simulizi ambacho kinahusishwa na binadamu na mazingira anayoishi. Binadamu huakisi mazingira anayoishi na hivyo basi kila shughuli huambatana na mazingira anamoishi. Hivyo basi kigezo tulichokitumia kutathmini kazi hii ni utumizi wa nadharia ya uhalisia ambayo ni ulinganishi wa mambo kama yalivyotokea katika mazingira ya binadamu kwa kuangazia nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) dhana ya uhalisia ilianza kutumika takribani mnamo mwaka wa 1790. Katika mwaka huo, Emmanuel Kant katika kitabu chake kilichoitwa *Critique of*

*Judgement* alitumia mbinu ya udhahania kamilifu kama kinyume cha uhalisia. Kadri miaka ilivyosonga, kulizuka wahakiki kama vile Sehiller waliokuwa wakitumia istilahi hizi mbili yaani udhanifu na uhalisia kuashiria vinyume. Nadharia ya uhalisia imeweza kupitia mabadiliko kwa kuangaziwa na wananaadharia mbalimbali. Kwa kuwa nadharia ya uhalisia huendana na mazingira, hivyo basi mabadiliko ya kimazingira hupelekea kuwepo kwa mambo mapya ambayo yanaweza kutafitiwa kwa kujikita katika nadharia ya uhalisia.

Nadharia ya uhalisia imeelezwa na wasomi mbalimbali kutegemea mazingira ya kazi husika. Wafula na Njogu (2007), wanatolea fafanuzi zaidi juu ya uhalisia kwa kusema kuwa hili ni tapo mojawapo maarufu sana kwenye ulimwengu wa fasihi lenye msukumo mkubwa sana. Wanaendelea kusema kuwa dhana ya uhalisia hutumika kwa maana kuu mbili. Mwanzo ni katika kuelezea tapo la kihistoria la kipindi fulani maalum cha fasihi za Ulaya. Pili, ni dhana ambayo huhusishwa na sanaa ya kifasihi inayooynesha hifadhi au kuakisi sifa bainifu zinazohusu uhalisia. Kwa kiasi fulani, kazi ambazo zinaangaliwa kwa kufuata mkabala wa uhalisia zinapaswa kuwa kama akisiko ama kioo cha hali halisi ya mazingira ya maisha ya wanajamii wanaohusika. Kutokana na maoni yao, tunaweza kusema kuwa uhalisia unahuksika zaidi na mazingira fulani hivi kwamba maudhui yanayojitokeza katika kazi fulani ya kifasihi huendana na mazingira ya jamii husika. Walengwa wa kazi ya kifasihi huweza kuelewa kazi ilioandikwa ua inayowasilishwa iwapo inashughulikia hali halisi ya mazingira yao. Mathalan, mtegaji wa kitendawili anapaswa kuulizia mambo ambayo yanapatikana katika mazingira yao ndiposa wateguaji waweze kutafakari na kupata jibu baada ya kufananisha sifa za kitendawili na mambo yanayowazunguka. Hii ina maana kuwa mazingira ni muhimu katika kuelezea kazi ya fasihi. Vivyo hivyo, nyimbo pia huendana na mazingira na ndiposa tukajikita katika jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu.

Katika kazi ya fasihi, uhalisia unapaswa kuonyesha uwezo wa kusawiri au kutoa picha ya hali halisi hasa kwa kuzingatia ukweli wake au kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Mambo kama haya ndiyo yaliyotumika huko Ufaransa na waandishi kama vile Flaubert katika mwaka wa 1850. Flaubert anasemekana kuwa alifafanua kazi ya fasihi kwa kuonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo katika uhalisia wake. Maoni yake ni kuwa uhalisia unajihuksisha na uigizaji wa mazingira anamoishi mwanadamu. Kwa hivyo basi, waandishi wa fasihi wanapaswa kuzingatia mazingira ya walengwa wa kazi zao ili iweze kuelewka. Nyimbo pia ni kipera cha ushairi simulizi ambao ni utanzu mojawapo wa fasihi simulizi. Nyimbo huimbwa kutegemea

mazingira kama vile nyimbo za mbolezi humbwa wakati wa mazishi kwa lengo la kuwaliwaza waliofiwa. Hii ina maana kuwa waimbaji wanapaswa kuteua nyimbo za kuimba katika shughuli fulani na ambazo zitawiana na hali halisi. Nyimbo za hodiya ambazo huimbwa wakati wa kufanya kazi hutofautina kutoka kazi moja hadi nyingine. Zipo nyimbo za wavuvi, wakulima na wagemaji kama ambavyo tutakavyoonyesha katika sura zifuatazo za tasnifu hii.

Wasomi wengine wanasema kuwa uhalisia unahusishwa na saikolojia ya wahusika. Huu ni uhalisia wa hali ya walengwa wa kazi ya kifasihi. Mathalan, Hegel katika kitabu chake kiitwacho *Aesthetics* alitumia neno uhalisia kudhihirisha kazi ya kifasihi iliyo na wahusika ambao matendo yao yanajengwa na hali ya kisaikolojia inayowazunguka. Uhalisia wa hali ya watu ambao ni wahusika wa kazi fulani ya kifasihi ni muhimu katika kujenga taswira kwa walengwa wa kazi husika. Nyimbo za hodiya zinapoimbwa huendana na kazi mahususi na kuonyesha changamoto za kazi na umuhimu wa kufanya kazi. Wavuvi huimba nyimbo zinazoashiria sifa na changamoto za uvuvi huku wakulima wakiimba wawe ambazo zinaashiria hali halisi ya ukulima. Kwa hivyo, kazi ya kifasihi huendana na mazingira na huonyesha saikolojia ya wahusika kama anavyosema Hegel. Kulingana na mawazo ya Hegel msanii anapaswa kuyachora maisha ya kijamii katika mipaka ya kijamii, kiuchumi, kidesturi na kisiasa. Msingi huu unafanana na mawazo ya mwanafalsafa Schelling ambaye anachukulia kwamba huwa kuna kufanana kwa jinsi mtu anavyoweza kuyazuia na kuyafafanua mambo, yaani kuyapima na kuyachuja mambo akilini mwake kibinagsi.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) uhalisia hutilia maanani na kusositiza uangaziaji wa maisha na matendo kwa uaminifu wake. Mtazamo huu unazingatia uwasilishaji wa mambo kama yaonekanavyo katika jamii. Waandishi wanaoandika kwa mtazamo huu wanapaswa kuongozwa na picha na mandhari yaonekanayo katika jamii ya mlengwa wa kazi husika. Uhalisia umehusishwa na mikondo mbalimbali mionganoni mwao ni:

- i. Ni mwelekeo uliojikita katika sayansi kwa kufafanua jambo na kwamba uhalisia unahusu ugunduzi wa mambo kwa kutumia teknolojia.
- ii. Ni mwelekeo unaozingatia upinzani dhidi ya bunilizi ya kinjozi ambao ni utunzi fulani wa kifasihi ambao mwandishi anaandika kutumia wahusika ambao sio wa kawaida. Ambapo uhalisia unasisitiza utumizi wa wahusika wa kawaida na wala sio wahusika ambao sio wa kawaida.

- iii. Ni mbinu ya kusanii ilio na maakisiko katika hali ya maisha ya binadamu ya kawaida. Hivi kwamba chochote kitendwacho na wahusika kinategemea sana mazingira waliyomo watendaji.
- iv. Ni mbinu ya kuhakiki inayojikita katika matumizi ya mazingira ya wahusika na lugha wanayotumia.

Tukizingatia mada ya utafiti wetu inayohusu maudhui katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, nyimbo za hodiya hutendeka katika hali halisi ya maisha ya binadamu wanapofanya kazi fulani. Nyimbo za hodiya huangazia mambo yanayodhihirika katika jamii husika na shughuli zao za kiuchumi. Nyimbo za hodiya huwasilisha majukumu kama vile kukashifu uvivu na kukejeli na kusifu matendo yanayotendwa na wanajamii. Hii ndio sababu iliyotufanya tuchague nadharia ya uhalisia ambayo inajikita katika maudhui ya kazi ya kifasihi kwa mujibu wa mazingira ya wahusika. Nadharia ya uhalisia ni mwafaka katika utafiti huu kwa kuwa inaangazia maudhui kama yanavyojoitokeza katika kazi za kifasihi kwa mujibu wa mazingira maalum. Kwa hivyo basi, nadharia hii imetufaa katika kulinganisha na kulinganua maudhui katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni hasa tukizidi kuzingatia mawazo ya Hegal, utafiti wetu umezingatia mawazo ya Hegal.

## **1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada**

Kuna waandishi mbalimbali walioshughulikia utanze wa fasihi kwa ujumla. Kuna wale walioandika kwa undani kuhusu utanze wa fasihi andishi kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi. Kuna wale walioandika kuhusu fasihi simulizi kwa mapana na wengine kuandika tu kuhusu kipera fulani katika fasihi simulizi. Utafiti wetu unahu kuhusu utanze wa nyimbo kama kipera cha fasihi simulizi. Sisi tunazingatia nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Aidha tunaangalia yaliyoandikwa kuhusu mada hii kama yalivyoandikwa na watafiti wengine. Kazi za watafiti wengine zitatufaa katika kutuwekea msingi wa utafiti wetu.

### **1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nyimbo kwa Ujumla**

Ni watafiti wengi tu walioshughulikia utanze wa nyimbo kwa ujumla. Hata hivyo tunazingatia baadhi yao tu na ambao kazi zao ni muhimu kwa utafiti huu wa sasa. Wamitila (2003) aliandika kuhusu utanze wa nyimbo kwa ujumla. Aliandika kuhusu nyimbo na nafasi ya nyimbo katika

jamii. Muktadha wake ulikuwa kuhusu majukumu yanayotekelawa na nyimbo katika jamii. Vile vile, aliangalia aina za nyimbo na uainishaji wake ambapo aliangalia nyimbo za bembelezi kutoka jamii mbali mbali kama vile Wameru, Wakikuyu, Waswahili na jamii nyinginezo; zote zikiwa na maudhui ya kuwabembeleza watoto walale na hasa wanapolia. Wamitila aliangalia nyimbo kwa kuainisha ngoma za Waswahili ambazo huchewa na watu mbali mbali kama vile namna ambavyo vugo huchewa na wanawake watu wazima, kishuri huchewa na wasichana, mkwaju huchewa na wanawake na wanaume. Nao msondo huchewa na vijana. Wanaume wanapokuwa peke yao hucheza kirumbizi. Pia aliangalia nyimbo za jamii ya Waswahili za watoto wa chekechea, kisha akaangalia nyimbo za wawe ambazo ni nyimbo za wakulima. Aliangalia pia nyimbo za kimai zinazohusishwa na mabaharia na nyimbo nyinginezo. Utafiti wake basi ultutia mori ya kutaka kuchambua zaidi maudhui ya nyimbo za kazi yanayojitokeza katika jamii mahususi ya Waswalili wa Jomvu Kuu, hasa tukiyalinganisha na ya jamii ya Wadigo wa Msambweni. Vile vile, kazi yake imetusaidia kuieleta jamii ya Waswahili zaidi. Ingawa hivyo, utafiti wake unatofautiana na wetu kwa kuwa tunalinganisha maudhui ya nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu.

Kinoti (2007), alishughulikia mambo mengi kuhusu nyimbo. Kwanza aliangalia aina za nyimbo mbalimbali zikiwemo za sherehe za kuzaliwa kwa mtoto katika jamii ya Wameru. Katika jamii hii ya Wameru, mtoto anapozaliwa watu walishereheke kwa nyimbo nne kwa mtoto wa kiume na nyimbo tatu kwa mtoto wa kike. Wale watoto wengine pia walishereheke kuzaliwa kwa mtoto mwenzao. Hilo lilichukuliwa kama tukio muhimu kwa vile watoto wengi walikuwa wakifariki sana kwa sababu ya maradhi ya ukosefu wa lishe bora. Aidha Kinoti pia aliangalia nyimbo za kumpa mtoto jina katika jamii mbalimbali nyimbo hizo zilisifu watu waliotajwa. Kinoti pia alitafiti kuhusu nyimbo za matambiko ziimbwazo wakati kumetokea janga au tatizo lolote ama iwe ni ukame wa muda mrefu au mafuriko, na kunapotokea haja ya kufanya tambiko kwa sababu ya tukio fulani. Hii ni kwa sababu Waafrika asilia huamini kuwa kuna Mungu na miungu hivyo anapopatwa na shida fulani hana budi kufanya matambiko kama njia ya kujitakasa. Kinoti aliangalia nyimbo za matambiko ya Wameru ambao huimba wakati wa kiangazi. Vile vile aligusia nyimbo za miviga za shughuli za Kaya kwa Wamijikenda na hasa Wadigo. Kinoti alipata kuwa watu wateule hasa wazee huvalia kaniki nyeusi na kuenda huko mizimuni kuomba mvua. Wazee hawa wateule huandamana siku fulani na kwenda huko kwa imani kuwa baada ya kuomba hiyo

miungu yao mambo hasi ambayo wamekuwa wakiyapitia yatabadilika. Baada ya maombi hayo mvua hunyesha kuashiria imani yao kuwa kuna miviga fulani ambayo ilikuwa imefanywa visivyo.

Kinoti aliangalia pia nyimbo za bembelezi za jamii ya Waswahili, Wakikuyu, Wanyokore na Wameru. Pia aliangalia sifa za nyimbo za watoto wa Kimeru wanapocheza. Kwa mujibu wa Kinoti, nyimbo hizi zina sifa kama vile kuwepo na ngoma na ala nyinginezo za muziki pamoja na unenguaji wa viuno na kuchezesha viungo mbalimbali. Isitoshe aliangalia nyimbo za tohara za Waafrika, nyimbo za mapenzi na za harusi za jamii ya Wameru. Kisha akaangalia nyimbo za hodiya na kupata kuwa nyimbo hizi huambatana na kazi husika. Kinoti anatoa mifano ya kazi kama vile za kulima, kutwanga, kusaga mahindi, kuvuna na nyinginezo. Alitutajia jamii ya Wameru wakiwa na nyimbo za kazi, jamii ya Maasai ambayo bado wana nyimbo za kazi, Waswahili bado wana nyimbo za wawe za wakulima, kimai za mabaharia na kongozi zinazosherehekewa mwishoni mwa mwaka. Kazi ya Kinoti ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa ilituwekea msingi katika uchanganuzi wa madhumuni ya utafiti huu. Ingawa hivyo, utafiti wetu unatofautiana na wake kwa kuwa tunajikita katika ulinganisho wa maudhui katika nyimbo za kazi za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.

Njogu na Chimera (1990) waliandika kuhusu wawe. Watafiti hawa wanasema kwamba wawe ni aina ya nyimbo ambazo huimbwa wakati watu wanafanya kazi ya kulima na kusaidia katika kazi za shambani kwa ujumla. Vile vile walitafiti kuhusu kimai ambazo ni nyimbo za mabaharia ambazo huimbwa kama njia ya mawasiliano ili kutiana mori wakati wa uvuvi. Watafiti hawa wamejikita kwa sifa za nyimbo za kazi ilhali sisi tunashughulikia nyimbo hizi kimaudhui. Hata hivyo kazi ya Njogu na Chimera imetufaa sio haba kwa kuwa sote tunashughulikia kipera cha nyimbo na hasa nyimbo za hodiya. Kazi yao imetusaidia kuielewa jamii ya Waswahili kwa ujumla.

### **1.8.2 Nyimbo za Aina Maalum**

Katika kisehemu hiki tunashughulikia nyimbo maalum kama ambavyo zimeelezwa na watafiti mbalimbali. Timammy (2002) alitafiti nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili. Katika utafiti wake alijikita katika nyimbo za harusi za wanawake Waswahili wa Mombasa. Kwenye utafiti wake, ye ye alijihusisha na mtindo wa nyimbo hizi za harusi za wanawake Waswahili wa Mombasa. Utafiti wake ni muhimu kwetu kwa kuwa tunachunguza kipera cha nyimbo ambazo alizitafiti ila kazi yake inatofautiana na hii ya sasa kwa misingi ya mada ya uchunguzi. Utafiti wetu sisi umo

katika kuangalia nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu hasa tukizingatia ya kwamba Jomvu Kuu imo Mombasa. Ingawa hivyo, kazi yake imetusaidia kuielewa jamii ya Waswahili kwa kina.

Dau (2014) alitafiti kuhusu nyimbo za kiasili za harusi za jamii ya Wadigo na jamii ya Waswahili. Kazi yake hasa iliangazia majukumu ya nyimbo za kiasili za Wadigo na Waswahili hasa akilinganisha na kutofautisha maudhui yanayojitokeza kwenye hizo nyimbo za harusi za jamii hizo mbili. Katika utafiti wake, Dau alipata kwamba upo mwingiliano wa kimaudhui baina ya nyimbo za kiasili za Wadigo na Waswahili ambazo huimbwa kwa malengo ya kuwatumbuiza waliofika kwenye sherehe. Vile vile, nyimbo hizo huwa na ujumbe kwa waliolengwa hasa bibi na bwana harusi. Dau aligundua kuwa katika jamii zote mbili, nyimbo za harusi za kiasili zinadhahirisha maudhui ya maombi kwa wanaooana. Kwa upande wetu nasi, kazi yetu inahu su ulinganishi wa maudhui ya nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Hata hivyo, kazi ya Dau imetusaidia katika kuangazia hasa maudhui ya nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni iwapo yanafanana. Kazi yake imetupa hamu ya kuamini kuwa iwapo Waswahili wana nyimbo za harusi basi pia hawakosi nyimbo za hodiya. Kazi yake imetusaidia kuelewa jamii ya Wadigo kwa ujumla pia.

Mugambi (2007) alitafiti majukumu ya nyimbo mbalimbali. Mugambi alishughulikia nyimbo kwa ujumla wake na wala hakujikita katika jamii mahsus. Baadhi ya majukumu anayoyaangazia Mugambi ni kama vile, kuburudisha, kuliwaza, kuelimisha na kuonya dhidi ya tabia fulani hasi. Utafiti wake ni muhimu kwa huu wa sasa kwa sababu tunachunguza kipera cha nyimbo kama alivyofanya na vile vile, majukumu kama alivyoyaeleza Mugambi yanatuwezesha kuzielewa nyimbo za kiasili na hivyo kupata maudhui katika nyimbo husika. Fauka ya kwamba utafiti wetu unahu su nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, utafiti wa Mugambi umetufaa katika kujibu maswali ya kazi yetu. Kazi yake imetusaidia katika kutambua pengo lilipo kwani nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo hazijatafitiwa kamwe.

Beja (2001) alifanya utafiti wa nyimbo za matanga za kundi la Wagirlama. Alijikita katika maudhui yaliyomo katika nyimbo hizo. Beja alipata kuwa nyimbo za Wagirlama huwa na maudhui mbalimbali. Beja anasema kuwa nyimbo za matanga huimbwa wakati ambapo mtu ameaga dunia na hukusudiwa kuwaliwaza waliofiwa. Beja pia anasema kuwa nyimbo za matanga husawiri mazingira na hali. Hali yenyewe huwa ya kuomboleza. Kazi ya Beja imetufaa kwa kuwa

alishughulikia maudhui katika nyimbo. Ingawa hivyo, utafiti wake umetofautiana na huu wa sasa kwa kuwa tunatafiti kuhusu nyimbo za hodiya ambazo huimbwa katika mazingira tofauti na nyimbo za matanga. Kwa hali hii basi, maudhui yetu yanatofautiana na aliyoyapata Beja kwa kuwa sisi tunachunguza nyimbo ambazo huimbwa watu wakiwa wanafanya kazi. Utafiti wake umetusaidia katika kufafanua maudhui ya nyimbo kwa ujumla.

Kutokana na kazi zote zilizoangaliwa kuhusu nyimbo, tunaweza kubaini kwamba hakuna kazi yoyote inayofanana na utafiti wetu. Ni wazi kwa maoni yetu kwamba nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo na Waswahili hazijatafitiwa. Ni imani yetu kwamba utafiti wetu utakidhi mahitaji yetu ya kuweka kumbukumbu maktabani.

## **1.9 Mbinu za Utafiti**

Utafiti wetu unashirikisha aina mbali mbali za mbinu za utafiti ambapo tunazingatia sana maktaba ambako tumesoma vitabu vyenye maelezo kuhusu fasihi simulizi kwa ujumla. Vile vile, tumetumia mtandao kupata maelezo kuhusu nadharia ambayo tunatumia katika utafiti wetu. Njia nyingine tulioitumia katika utafiti wetu ni kwenda nyanjani. Huko nyanjani tumejikita katika uchunguzi shiriki na Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni katika kukusanya data tuliyohitaji.

### **1.9.1 Njia za Kuteua Sampuli**

Njia ambayo tumetumia katika kupata sampuli ni kutumia wanaume kumi wenye umri wa miaka hamsini na zaidi kwa kuwa ndio ambao wametusaidia katika kupata data yetu ikizingatiwa kuwa umri wao mpevu unaashiria kuwa walikuwa wakiziimba nyimbo za hodiya. Vile vile, tumetumia wanawake kumi wenye umri sawa na hao wanaume. Hii ni kwa sababu vijana wa siku hizi wengi wao hawana uelewa wa hizi kazi na nyimbo zao kwa sababu kazi zao nyingi zinafanywa na mitambo. Pia vijana wengi wamehamia mijini na hivyo kuajiriwa katika makampuni ambapo hawana wasaa wa kuimba huku wakiendelea na kazi. Hawa wanaume na wanawake tulisaidiwa kuwapata kupitia kwa wazee wao wa vijiji. Wazee hawa wa vijiji ndio walituelekeza kwa hawa wazee na wanawake wakongwe kwa sababu wao ndio wanajua wanapatikana wapi.

### **1.9.2 Njia za Kukusanya Data**

Njia za kukusanya data huko nyanjani ilikuwa kushirikiana kwa kutumia mbinu ya uchunguzi shiriki ambapo tulifanya kazi na wakongwe hawa huku wakiimba nyimbo zilizoendana na kazi husika. Uchunguzi shiriki ulituwezesha kujifunza kuziimba nyimbo zao za hodiya. Vile vile, kwa kutumia kamera ambayo imo katika simu, tuliwarekodi wakongwe hawa wakiwa wanaimba nyimbo zao za kazi mbalimbali kama vile kulima, kutwanga, kusaga, kuvua, kugema na kusuka makuti. Data iliyokuwa imepatikana tuliiandika katika daftari baada ya kutoka nyanjani na kisha kuteua iliyokuwa mwafaka katika kuafikia madhumuni ya utafiti wetu. Hatimaye tulichanganua data yetu kwa njia ya kinathari.

### **1.9.3 Uchanganuzi wa Data**

Data tuliohitaji ilitokana na nyimbo teule za hodiya ambapo tulijikita katika nyimbo thelathini na sita. Nyimbo za kazi ya ukulima ambayo hufanywa na wanaume na wanawake tulizingatia nyimbo tatu ambazo zilikuwa zinasawiri maudhui katika nyimbo za hodiya. Hivyo basi kwa usaidizi wa simu na uelewa uliotokana na kujifunza nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni tuliteua nyimbo tatu tatu za kazi za uvuvi na ugemaji kwa upande wa wanaume Wadigo. Kwa upande wa wanawake, vile vile, tulichanganua nyimbo tatu za kazi ya kutwanga mahindi, tatu za kazi ya kusaga na tatu za kazi ya kusuka makuti.

Kwa upande wa Waswahili wa Jomvu Kuu pia tulijiunga nao katika kufanya kazi za kutwanga, kusaga na kufinyanga vyungu kwa wanawake na kwa upande wa wanaume tuliungana nao katika shughuli za uvuvi, ugemaji na ukulima. Tulipokuwa na wao tulijifunza nyimbo wanazoimba wakiwa kazini mwao. Hivyo kwa ujuzi huo na usaidizi wa simu tulifanikiwa kurekodi nyimbo kumi na nane ambazo tisa ni za wanaume na tisa ni za wanawake wanazoimba wanapokuwa wakifanya kazi zao za ukulima, uvuvi, ugema, kutwanga, kusaga na kufinyanga vyungu. Data tuliyokuwa tumeipata tulichanganua kwa misingi ya nadharia ya uhalisia.

## **1.10 Hitimisho**

Katika sura hii, tulitanguliza kwa kueleza kuhusu jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Hususan tuliangazia maeneo yao wanamoishi na muingilio wao katika shughuli zao za kila siku. Vile vile, katika sura hii tuliangalia tatizo la utafiti na madhumuni ya kuchagua

mada hiyo, sababu za kuchagua mada ni athari ya kupotea kwa nyimbo za hodiya kwa sababu ya mitambo ya kufanya kazi hizo. Tumeonyesha kuwa kusudi la kufanya utafiti huu ni kuhifadhi maktabani nyimbo mbali mbali za kiasili kwa matumizi ya vizazi vijavyo ambavyo havitapata nafasi ya kusikiza nyimbo hizi zinapoimbwa kwa sababu ya mabadiliko mbalimbali ya kijamii kukiwemo uhamiaji mijini kwa lengo la kutafuta ajira. Tumeshughulikia pia msingi wa nadharia ambayo ilituongoza katika utafiti wetu na ambayo ni nadharia ya uhalisia. Nadharia hii inahusu uwezo wa kusawiri kazi ya kifasihi kwa kutoa picha ya jinsi binadamu anavyoingiliana na mazingira yake. Nadharia hii ilitusaidia kuafikia malengo yetu kwa kuwa inaangazia maudhui ya kazi ya kifasihi. Hatimaye tumeangalia yaliyoandikwa kuhusu mada kwa ujumla na yaliyoandikwa kuhusu nyimbo maalum, upeo na mipaka ya utafiti na mbinu tulizozitumia katika utafiti huu.

## **SURA YA PILI**

### **NYIMBO ZA HODIYA ZA WASWAHILI NA WADIGO**

#### **2.0 Utangulizi**

Katika sura hii tunajikita katika kutambua aina mbalimbali za nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na vilevile tuangazie nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni. Nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni tunazozishughulikia ni pamoja na nyimbo za kazi ya uvuvi, ukulima, kutwanga mahindi, kusaga mahindi, kugema na kusuka makuti. Kati ya kazi tulizozitaja hapo juu kuna kazi zinazofanywa na wanaume peke yake na zile zinazofanywa na watu wote, yaani wanawake kwa wanaume kama kazi ya ukulima. Kazi za kutwanga na kusaga mahindi, kusuka makuti ni kazi za wanawake isipokuwa kwenye dharura ndipo wanaume wanapozifanya. Kazi ya kugema ni kazi inayohusu kukwea minazi na kugema tembo na hivyo basi ni kazi ya wanaume pekee kwa kuwa wanawake hawaiwezi. Tuligundua kuwa Wadigo walikuwa wakiimba nyimbo za aina mbalimbali kutegemea aina ya kazi na ambazo tunazishughulikia katika sura hii.

Waswahili wa Jomvu Kuu wanazo nyimbo ambazo wao huziimba wakati wanapofanya kazi. Wanaume hufanya kazi kama vile ugemaji na uvuvi huku wanawake wakifanya kazi za ufinyazi, na kusaga na kutwanga mahindi. Tuligundua kuwa kazi ya ukulima hufanywa na wanawake na wanaume vile vile. Zipo nyimbo ambazo huimbwa na Waswahili wa Jomvu Kuu wanapokuwa wakifanya kazi. Tulibaini kuwa nyimbo za kazi ambazo huimbwa na Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni hazifanani. Ingawa jamii hizi mbili hujihisisha na kazi sawa, tuligundua kuwa nyimbo zao zinatofautiana na ndio sababu tunataka kuona iwapo zinabeba maudhui sawa au la. Katika sura hii, tunaangazia kazi za ukulima, ugemaji, uvuvi, kusaga na kutwanga mahindi na ufinyanzi wa vyungu. Tunajikita katika maudhui ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni kwa sababu ya ujirani wao na hasa tukizingatia ya kwamba wote ni wafuasi wa dini ya Kiisilamu jambo linalotufanya kuamini kuwa jamii hizi mbili zina imani sawa.

## **2.1 Nyimbo za Hodiya za Wadigo wa Msambweni**

Wadigo wa Msambweni hufanya kazi mbalimbali ambazo zinawawezesha kujikimu kimaisha. Tumeonyesha kuwa wanaume hufanya kazi ya uvuvi unaoendelezwa katika bahari Hindi na ugemaji ambao unahusisha kukwea minazi na kuangua nazi zenyewe. Kwa upande mwingine, wanawake Wadigo wanahuksika na kazi kama vile za kusaga na kutwanga mahindi na kusuka makuti. Hii ina maana kuwa kazi za Wadigo wa Msambweni zimebainishwa kwa misingi ya jinsia kutegemea shughuli zinazoendelezwa. Tunaanza kwa kazi ya ukulima ambayo hufanywa na wanawake na wanaume.

### **2.1.1 Nyimbo za Hodiya za Ukulima**

Ukulima unahusisha kutifua udongo, kuatika mbegu, kuzipalilia wakati ukifika na kisha kuvuna mazao baada ya kukomaa. Wadigo wa Msambweni walipanga siku tatu mfululizo za kufanya kazi hiyo ya kulima kisha wakajipa siku moja ya kupumzika. Hizo siku hazina mpangilio wa kufuatana kama vile tulivyo na siku za wiki, yaani Jumatatu hadi Jumapili. Siku zao hazifuatani na siku za wiki. Isipokuwa tu siku ya Ijumaa ambayo ni siku yao ya kwenda kuswali msikitini swala ya Ijumaa na ambayo ndio wao hupata fursa ya kupumzika. Hivyo basi siku yao ya kwanza baada ya ile siku yao ya kupumzika huitwa ‘kualuka’. Hiyo ni siku yao ya kwanza kwenda shambani kufanya kazi ya ukulima. Siku yao ya pili ni siku ya ‘kurima phiri’. Siku yao ya tatu ni ‘pkwisha’, kisha ikafuatiwa na siku ya ‘Juma’. Siku hizo tatu Wadigo wa Msambweni hurauka kwenda mashambani mwao na kufanya kazi ya kulima; iwe ni kupanda, kupalilia mahindi ama nafaka mbalimbali. Hii inaonyesha kuwa Wadigo huwa hawafanyi kazi siku zote za juma bali huwa na siku tatu maalum ambazo zimetengwa kwa ajili ya kazi ya ukulima.

Wadigo wa Msambweni wanapokuwa katika shughuli za ukulima wao hufanya kila juhudhi ya kutiana mori ya kufanya kazi ili kuondoa uchovu; wale walegevu nao hujikuta wanachangamka katika kazi. Wadigo hutumia ala za muziki kama vile gunda na zumari wanapokuwa wanaimba nyimbo zao. Ala hizi za muziki huwfurahisha sana hasa wakiwa kwenye kazi ya jumuiya ambayo wanairejelea kama ‘mwerya’, yaani kundi la watu wanaoenda kulima katika shamba la mmoja na kesho yake kundi hilohilo linaenda kwa mtu mwingine. Mzunguko huo hufuatwa kwa utaratibu mpaka watu wote wanaohusika katika ulimaji huu wa kikoa wameisha. Hili linafanywa kwa lengo la kusaidiana kazi mbalimbali ili kukamilisha kazi kwa haraka na urahisi. Hali ya kulima kikoa

huonyesha ushirikiano na umoja katika kufanya kazi. Wadigo wa Msambweni wanapokuwa kazini mwao ya ukulima huimba nyimbo za kazi mbalimbali kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

Mwongozaji: *Endekala nyuma ndiye, gonzi gonzi baa x 2*

Wapokezi: *Gonzi wee baa,*

*Gonzi wee baa,*

*Gonzi wee baa,*

Mwongozaji: *Endekala nyuma ndiye,*

*Gonzi gonzi baa x 2*

Wapokezi: *Gonzi wee baa*

Mwongozaji: *Endekala nyuma ndiye*

*Gonzi gonzi baa x 2*

Wapokezi: *onzi wee baa x 2*

## **Tafsiri**

Mwongozaji: Atakaye baki nyuma aitwe kondoo wee baa x 2

Wapokezi: Kondoo wee baa

Kondoo wee baa

Mwongozaji: Atakaye baki nyuma aitwe kondoo wee baa x 2

Wapokezi: Kondoo wee baa

Kondoo wee baa

(Wimbo 1- kulima)

Huu ni wimbo ambao huimbwa na Wadigo wa Msambweni wa jinsia ya kiume na kike wakati ambapo kazi ya ukulima imeshika kasi. Kama tulivyosema awali ni kuwa Wadigo hufanya kazi ya ukulima kwa kikoa kutoka shamba la mmoja wao hadi kwa mwingine. Hodiya ambayo tumeirejelea hapo juu huimbwa hasa pale ambapo kuna mtu anayeonekana amechoka na ana ulegevu au uvivu wa kuendelea na kazi. Kutokana na hodiya hii, ni kwamba anayeonekana kuwa anabaki nyuma kwa sababu ya uvivu hurejelewa kama kondoo. Kondoo ni mnyama ambaye

hufugwa nyumbani. Kondoo ni mkubwa kama mbuzi na aliye na manyoya marefu. Sifa kuu ya kondoo ni kwamba hapendi kulia sana. Hali ya kuwa mtulivu ndio huwafanya watu kuamini kuwa kondoo ni mnyama mvivu. Hii ndio sababu ambayo inawafanya Wadigo wa Msambweni kumrejelea mtu mvivu kazini kama kondoo.

Hodiya hii ya Wadigo huimbwa kwa sauti huku watu wanaofanya kazi wakiwa wameinama wanalima. Wimbo huu unakashifu uvivu na kwa kuwa hakuna anayetaka kuchukuliwa kuwa kama kondoo, basi kila mtu hutia bidii ili asije akawa chanzo cha kuwarudisha wenzake nyuma. Hivyo kila mtu anajitahidi, anajituma na kutia bidii ili asiachwe nyuma. Hodiya hii huimbwa kwa lengo la kutiana shime ili mtu asipatwe na aibu na kuitwa kondoo ambaye ni mnyama anayejulikana kwa sifa ya uvivu. Vile vile lengo kuu la kulima kikoa huwa ni kuhakikisha kuwa sehemu kubwa imeshughulikiwa kwa muda mfupi na kukamilisha kazi ya mmoja wao ili waende kwa mwingine. Wadigo wa Msambweni wanapolima hugawa shamba husika kwa kulikata visehemu vidogovidogo halafu kila mmoja anashika sehemu yake. Hivyo kila mmoja anajikaza asibaki nyuma kwa kuwa itakuwa sio vizuri kurejelewa kama kondoo kuashiria sifa ya uvivu.

Waimbaji ambao ni Wadigo wanaofanya kazi ya ukulima wanakashifu uvivu mionganoni mwa wanaofanya ya ulimaji kikoa. Wadigo wa Msambweni wanatumia mbinu ya sitiari kuashiria mtu mvivu. Sitiari ni mbinu ya ulinganisho wa moja kwa moja. Katika wimbo huu, waimbaji wanamlinganisha mtu mvivu na kondoo, mnyama anayechukuliwa kuwa mvivu. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa hodiya za Wadigo wa Msambweni hubeba maudhui ya uvivu kwa lengo la kuwakashifu wale wanaotaka kufanya kazi pole pole. Vile vile, ili kupunguza uvivu, Wadigo wanawagawia kila anayelima sehemu yake ili kumfanya kutia bidii kama wenzake na kumaliza kwa wakati ufaao.

Wadigo wa Msambweni huwa na wimbo ambao huimbwa wanapolima wakati wa kiangazi. Wimbo huu huimbwa na wanawake kwa wanaume wa Kidigo wa Msambweni wanapofanya kazi ya ukulima kuashiria athari za kiangazi. Kiangazi ni majira ya mwaka wakati jua linapokuwa kali baina ya vuli na masika. Wakati wa kiangazi kunakuwa na ukame hivi kwamba hamna mvua na hivyo basi ni vigumu kupata chakula hasa mboga. Hata hivyo wakulima huandaa mashamba yao wakati wa kiangazi wakisubiri majira ya mvua ili wapande mimea. Wadigo wa Msambweni wamebuni wimbo ambao wao huimba wanapofanya kazi ya ukulima majira ya kiangazi kama ifuatavyo:

Mwongozaji:           *Nanzala mayo nanzala*  
                          *Narimira mariga wee*  
                          *Nanzala mayo nanzala*  
                          *Narimira mariga wee x 2*

Wapokezi:            *Nanzala mimi nanzala*  
                         *Narimira mariga wee*  
                         *Nanzala mimi nanzala*  
                         *Narimira mariga wee x 2*

Mwongozaji:         *Nanzala mayo nanzala*  
                         *Narimira mariga wee*  
                         *Nanzala mayo nanzala*  
                         *Narimira mariga wee*

### Tafsiri

Mwongozaji:         Nina njaa mimi nina njaa  
                         Nalimia ‘mariga’ wee x 2

wapokezi:            Nina njaa mimi nina njaa  
                         Nalimia ‘mariga’ wee x 2

Mwongozaji:         Nina njaa mimi nina njaa  
                         Nalimia ‘mariga’ wee x 2  
                         (Wimbo 2- kulima)

Hodiya hii ya Wadigo wa Msambweni inaonyesha athari za kiangazi ambapo watu huwa na njaa kwa kuwa chakula hupungua ikilinganishwa na majira ya mvua. Wimbo huu huimbwa wakati watu wanalima kuwakumbusha wakati wa kiangazi ambapo chakula kilikuwa kimepungua na kuwafanya hata kuenda msituni kuchimba viazi viazi msituni ambavyo huwa viko chungu sana. ‘Mariga’ ni kama viazi; mti huu haupandwi mashambani, humea wenyewe huko msituni. Watu huchimba na kuchambua viazi na kuvianika kwenye juu kisha baada ya kukauka kuwekwa kwenye

pakacha na kulazwa kwenye mto ili ule uchungu ulioko kwenye hayo ‘mariga’ utoke. Kisha asubuhi watu huchukua mapakacha yao na kwenda kupika nyumbani kama muhogo. Ndipo hapo wakati wa kilimo watu huimba huo wimbo ili watu watie bidii wasipatwe na shida ya chakula tena majira ya kiangazi yatakapofika.

Wimbo huu unaelezea athari za njaa ambazo ni kama vile kusababisha mauti kutokana na kula vyakula mwitu ambavyo ni vichungu na vyaweza kuwa hatari kwa wanadamu. Hata hivyo, Wadigo wa Msambweni wamedhihirisha kuwa wao hutafuta njia za kupambana na njaa kwa kuendea viazi mwitu, kuvikausha na kisha kuvitumia kama muhogo. Wimbo huu unaimbwaa kwa kusudi la kuwafanya watu kutia bidii ili kuepuka kuathirika na njaa wakati wa kiangazi kiasi cha kuwafanya kutafuta vyakula mwitu ambavyo vyaweza kuwa hatari kwao. Wadigo wa Msambweni wanapokuwa wakiimba wimbo huu huwafanya kuwa na ari ya kufanya kazi ili kuwa na chakula cha ziada ambacho kitatumiwa wakati wa kiangazi.

Hodiya ya tatu ambayo huimbwa na wakulima kuashiria kuwa chakula kimeisha na hivyo basi wanapaswa kutia bidii zaidi kuhakikisha kuwa wanapata cha kutia tumboni. Wimbo ufuatao huimbwa kwa lengo la kuwatia shime watu shambani ni:

Mwongozaji:                   *Chirumu changamika nyumbani*  
   *We mganga ooh wee! Changamika*  
   *Nyumbani we mganga*  
   *Kukachaa weee kukacha*  
   *Mayo kukacha we chijembe*  
   *Chinaburuga mtsanga*  
   *Ha ha ha ha*

Wapokezi:                       *Chijembe chinaburuga*  
   *Mtsanga*

Mwongozaji:                   *Ha ha ha x 3*

Wapokezi:                       *Chijembe chinaburuga*  
   *Mtsanga x 3*

### Tafsiri:

- Mwongozaji: Kisu kilipotea nyumbani kwa mganga  
Ooh wee! Kilipotea nyumbani  
Nyumbani we mganga  
Kumekuchaa wee! Kumekucha  
Mama kumekucha
- Wapokezi: Kijembe kinalima mchanga
- Mwongozaji: Ha! Ha! Ha!
- Wapokezi: Kijembe kinalima mchanga x 3  
(Wimbo 3- kulima)

Katika wimbo huu, mkulima anarejelewa kama mganga. Mganga ni mtu ambaye anachukuliwa kuwa na uwezo usio wa kawaida kama wanadamu wengine. Kwa hivyo tunatarajia kuwa hakuna ambalo linapaswa kumshinda kama vile kisu kupotea nyumbani mwake na asikipate. Sitiari imetumika hapa pia kwa kuwa mkulima anachukuliwa kuwa hapaswi kukosa chakula. Hii ni kwa sababu yeye kama mkulima anapaswa kutia bidii kulisha jamii kukiwemo wale ambao sio wakulima. Wadigo wanaposema kuwa ‘kisu kimepotea nyumbani’ huwa wanamaanisha chakula kimeisha nyumbani mwa mkulima. Kwa hivyo basi wakulima wanapaswa kutia bidii kulima wapate chakula kiwe kama silaha yao ya kujikinga dhidi ya njaa.

Wimbo huu hususan huimbwa wakati wa kupalilia mahindi. Mara nyingi wakati wa kupalilia mahindi watu hutumia vijembe vidogo ili wasikate mimea. Hodiya ambayo tumeirejelea hapa husaidia kuwatia shime wakulima katika kazi kwa sababu chakula hakipo nyumbani. Upungufu wa chakula nyumbani huwa na madhara mengi kama vile kuwalazimu Wadigo wa Msambweni kula ‘mariga’ ambayo yanaweza kuwadhuru iwapo hayatakaushwa vyema. Kwa hivyo basi wakulima huimba hodiya hii kuwakumbusha kuwa chakula kimeisha nyumbani na hivyo basi wanatakiwa kutia bidii wasije wakakosa chakula tena. Watu huwa wepesi wa kulima kwa vile hata vijembe vinavyotumiwa ni vidogo na huamini kuwa mkulima hatakiwi kukosa chakula nyumbani. Wimbo huu pia unawakumbusha wakulima kuwa wanatumia vijembe ambavyo ni vyepesi na ambavyo havichoshi na hivyo basi wanapaswa kupalilia sehemu kubwa sana.

Tumeangazia nyimbo za hodiya ambazo ni wawe kwa upande wa Wadigo wa Msambweni. Wawe huimbwa na wakulima wanapofanya kazi shambani. Kazi ya ukulima hufanywa na wanaume na wanawake. Wanawake pia huwa na kazi zao na ambazo hazifanywi na wanaume wa Kidigo. Wanawake wa Kidigo wa Msambweni hufanya kazi ya kutwanga nafaka baada ya kuvuna na huambatana na nyimbo kama tutakavyoonyesha katika sehemu ifuatayo.

### **2.1.2 Nyimbo za Hodiya za Kutwanga Nafaka**

Nafaka ni zao la aina za mimea ambazo huwa ni punje na huhusisha mawele, mpunga, mtama na mahindi. Katika jamii ya Wadigo tunapata nafaka kama vile mahindi na mchele. Nyimbo ambazo tunazirejelea hapa ni zile ambazo huimbwa na akina mama wakati wanafanya kazi ya kutwanga mahindi na mchele. Wakati wa kutwanga mara nyingi huwa ni wanawake wawili wawili wanatwanga kwa kupishana ili mahindi yatakate haraka. Nyimbo zenyewe ni:

Mwongozaji: *Ndiye ooya mundawe*

*Naumere tuchi na ndago*

Wapokezi *Tuchi! Tuchi! Na ndago*

Mwongozaji: *Ndiye ooya mundawe*

*Naumere tuchi na ndago*

Wapokezi *Tuchi! Tuchi! Na ndago*

Mwongozaji: *Ndiye ooya mundawe*

*Naumere tuchi na ndago*

Wapokezi *Tuchi! Tuchi! Na ndago*

#### **Tafsiri:**

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake  
kumee magugu na nyasi.

Wapokezi: kumee magugu na nyasi,  
magugu na nyasi

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake  
kumee magugu na nyasi.

Wapokezi: kumee magugu na nyasi,  
magugu na nyasi

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake  
kumee magugu na nyasi.  
(Wimbo 4- kutwanga mahindi)

Wimbo huu huimbwa ili kuwatia mori na motisha wanawake wanaofanya kazi ya kutwanga mahindi. Wanawake hawa wa Kidigo hutakiwa kutwanga mahindi kwa muda mrefu bila kupumzika. Wimbo huu huwatia nguvu za kutwanga mahindi hayo bila kupumzika. Kama ni mchele hutakata vizuri bila kuvunjikavunjika. Wanawake wa boma moja huwa na siku maalum ya kutwanga. Hususan siku ya Ijumaa, siku ambayo ni ya kupumzika ambapo watu hawaendi kwenye makonde yao. Wanawake hawa hukaa katika kivuli ambapo kunakuwa na vinu kama vinane na wanawake wakiwa na mahindi yao wanatwanga na kuyaanika. Hivyo hao hufurahia na kuimba nyimbo zao za hodiya huku wakicheza. Hufanya hivyo ili kutoa uchovu na kutohisi uvivu. Wakiwa na hivyo vinu wanasaidiana na wanatwanga mahindi ya mmoja kama mara tatu na mwengine mara tatu na hili hufanya kazi kuwa rahisi. Wimbo mwengine ambao huimbwa wakati wanawake wa Kidigo hutwanga ni:

Mwongozaji: *Chibundani kakufipkwa kunani*

Wapokezi: *kuchifipkwa kunadepkwa achetu*

Mwongozaji: *Chibundani kakufipkwa kunani*

Wapokezi: *kuchifipkwa kunadepkwa achetu*

Mwongozaji: *Chibundani kakufipkwa kunani*

Wapokezi: *kuchifipkwa kunadepkwa achetu*

### Tafsiri:

Mwongozaji: Shambani ‘chibundani’ hakufikwi kuna nini

- Wapokezi: Watu wakifika kunatahiriwa wanawake.
- Mwongozaji: ‘Chibundani’ hakufikwi kuna nini
- Wapokezi: Kwatahiriwa wanawake
- Mwongozaji: Shambani ‘chibundani’ hakufikwi kuna nini
- Wapokezi: Watu wakifika kunatahiriwa wanawake.  
 (Wimbo 5- Kutwanga)

Kazi inapofika kileleni wanawake huwa na mori kabisa na huendelea kuimba hodiya hii ili kuondoa uchovu. Wanafurahia kazi ya kutwanga bila uchovu maana huwa wanatwanga kwa kupishana. Wimbo huu unawaonya wanawake dhidi ya kwenda shambani wakati wa kutwanga mahindi. Hii ni kwa sababu wakati wa kutwanga mahindi watu wamemaliza kazi ya kulima, kupalilia na kisha wamevuna na hivyo basi wanatakiwa kuyashughulikia mahindi yaliyovunwa. Wimbo huu unaashiria umuhimu wa kufanya kazi na kuikamilisha bila kuingilia kazi nyingine kabla ya kukamilisha ya wakati husika. Wimbo wa tatu ambao huimbwa wakati wanawake wanatwanga mahindi ni:

- Mwongozaji: *Yenderemwa mlumewe ni*  
*bobo lofu x 3*  
*Ise vyala naye ni bobo lofu*
- Wapokezi: *Ananyendeka na chitseko*
- Mwongozaji: *Nine vyala*
- Wapokezi: *Ananyendeka ni chitseko*
- Mwongozaji: *Mlamuwe!*
- Wapokezi: *Ananyenduka na chitseko*
- Mwongozaji: *Shangazire*
- Wapokezi: *Ananyendeka na chitseko*
- Mwongozaji: *Yendremwa mlumewe ni*  
*bobo lofu x 3*  
*Avyazie*

Wapokezi: *Ananyendeka na chitseko*

**Tafsiri:**

Mwongozaji: Atakaye choka mume wake

Hana faida x 3

Bavyaa

Wapokezi: Anatembea na kicheko

Mwongozaji: Mavyaa

Wapokezi: Anatembea na kicheko

Mwongozaji: Shemegi yake!

Wapokezi: Anatembea na kicheko

Mwongozaji: Shangazi yake

Wapokezi: Anatembea na kicheko

Mwongozaji: Atakayechoka mume wake

hana faida x 3

wazazi wake wanatembea na kicheko.

(Wimbo 6- kutwanga)

Wimbo huu unaonyesha kuwa mwanamke mvivu ni aibu kwa mume wake, mavyaa wake na hata kwa jamii yake yote. Hivyo wanapotwanga huwa hakuna kupumzika kwa sababu mtu hapendi aonekane kuwa mumewe na jamaa yake kwa jumla hawana umuhimu wowote. Wimbo huu unawafanya wanawake kutia bidii kwa kuwa anawakilisha jamaa yake yote hapa. Wanawake hawa pia hutwanga mahindi kikoa na hivyo basi sio vyema mmoja wao kuwa mlegevu na kuanza kupumzika kabla ya kukamilisha kazi.

### **2.1.3 Nyimbo za Hodiya za Kusaga Mahindi**

Baada ya kutwanga mahindi huwa ni lazima yasagwe kwa kutumia jiwe la kienyeji ambalo linajulikana kama ‘lala’ kwa Kidigo. Mahindi hayo husagwa ama na mwanamke mmoja au kama jiwe ni zito sana wanawake wawili huketi wakiangaliana na jiwe hilo huwa katikati wakisukuma

hiyo ‘lala’. Wakati wa kusaga mahindi, mwanamke mmoja huwa anashughulika na kuweka mahindi kidogo kidogo kwenye hilo jiwe ambalo husaga hayo mahindi na kuyageuza unga. Wakiwa katika kazi hii basi huimba nyimbo mbali mbali. Kazi hiyo hufanywa mchana kutwa au usiku mzima. Nyimbo zinazoimbwa wakati wa kusaga mahindi ni kama zifuatazo.

Mwongozaji: *Chimbere mbere Fatuma tumbo imbere x 2*

Wapokezi: *Kama ni hanzo kamuuze baba mdide*

*We mwenye wagunduliwa poreee*

*Fatuma poree*

Mwongozaji: *Naona ajabu Fatuma kulala na nduguyeee x 2*

Wapokezi: *chamba ni hanzo kamuuze baba mdide go*

*gakoo gagunduliwa poree Fatuma poree*

### **Tafsri:**

Mwongozaji: Kimbelembale Fatuma tumbo limbele x 2

Wapokezi: Kama ni uongo akaulizwe baba mdogo siri yake iligunduliwa  
polee Fatuma polee x 2

Mwongozaji: Twaona ajabu Fatuma kulala na ndugu yake x 2  
polee Fatuma polee.

Kama ni uongo akaulizwe baba mdogo siri yake iligunduliwa  
polee Fatuma pole.

(Wimbo 7- kusaga)

Huu wimbo ultungwa na vijana waliokuwa wakimkejeli dada mmoja aliyetungwa mimba na kaka yake akiwa bado masomoni. Hilo ni jambo la aibu. Hivyo basi kukomesha tabia kama hizo, watu huimba nyimbo kama hizo wakati wanaposaga mahindi ili kukashifu hiyo tabia ya kufanya mapenzi kiholelaholela. Wanawake hao huimba wimbo kama huo ili kukejeli tabia kama hizo kwa watoto wao. Wanawake hawa huimba wimbo huu ili kuwakumbusha watoto wao wa kike kuwa

wanapaswa kufanya kazi badala ya kuzururazurura ovyo ovyo. Wimbo mwingine ambao wanawake huimba wakati wa kusaga mahindi na hilo jiwe ni kama ufuatao:

*Nasaga vidzunga uyangu mino reroo wee mino.*

*Nkalole mtsedza wangu. Mjeni achedza munjitire sima*

*Nkalole mtsedza wanguuu mjeru*

*Acheza m jitire sina x 3*

### Tafsiri

Nasaga viunga vyangu mimi

Leo mimi nikaangalie mkwe wangu

Mgeni akija mpikie sima

Nikaangalie mkwe wangu

Mgeni akija mpikie sima x 3

(Wimbo 8- kusaga)

Wimbo huu huimbwa na mwanamke anapokuwa akisaga mahindi na ‘lala’ akiwa peke yake. Mara nyingi hilo jiwe huwa ni zito kusukuma. Hivyo huwa mtu anachoka haraka. Kupunguza hayo machovu humlazimu msagaji kuimba wimbo ili kujipa moyo wa kusaga unga mwingi mara moja. Vile vile humburudisha anapokuwa akifanya kazi. Mwimbaji anaonyesha kuwa anasaga mahindi ili aweze kupata unga wa kumpikia mgeni atakayekuja sima na pia anaweza kuwatemebelea wakwe zake na kuwagawia unga huo. Wimbo mwingine ambao huimbwa na akina mama wakati wa kusaga mahindi ni kama ufuatao:

Mwongozaji: *Unaphaya phaya we mayo unaphaya*

Wapokezi: *Gomba usikirwe*

Mwongozaji: *phaya we mayo unaphaya*

Wapokezi: *Gomba usikirwe*

*Mpkwaza mwanaa wa mwanzo*

*Mpkwaza mwana wa mwanzo*

*Naye wahenda uka*  
*Achisengera mbere*  
*Ta yuyu wa phiri naye*  
*Wahenda gapuza puzaa*  
*Richa umbeye mayo vyala*  
*Richa umbeya*  
**Wapokezi:** *Gomba usikirwe*  
**Mwongozaji:** *Una nung'unung'u mayo vyala*  
*Una nun'gu nun'gu*  
*Gomba usikirwe*

**Tafsiri:**

**Mwongozaji:** Waruka ruka mavyaa  
 Waruka ruka  
**Wapokezi:** Sema usikizwe  
**Mwongozaji:** Mkaza mwana wa mwanzo  
 Aliondoka akasonga mbele  
**Wapokezi:** Huyu wa pili naye alifanya kuyapuuza  
**Mwongozaji:** Wacha umbeya mavyaa  
**Wapokezi:** Sema usikizwe  
 (Wimbo 9- Kusaga)

Huu ni wimbo wa harusi ambao huimbwa wakati wa harusi kumuonya mavyaa mwenye tabia ya kusengenya kiasi cha kutowapa amani wakaza wa wana wao. Sasa wanawake pia huimba wimbo huu wakati wa kusaga mahindi ili kushutumu tabia mbaya ya kusengenya wakaza wana. Hili hufanywa kwa nia ya kurekebisha tabia mbaya na tena kujiburudisha wakiwa kazini hasa wakiwa wanasukuma hilo jiwe wakiwa wawili. Hodiya hii inaonyesha kuwa masengenyo huwa na athari hasi kwa jamii hasa iwapo ni mkaza mwana anasengenya. Wanawake wanaimba wanapokuwa

wakifanya kazi ili kukashifu tabia hasi na kuwataka wengine kufanya kazi badala ya kuwasengenya watu wengine.

#### **2.1.4 Nyimbo za Hodiya za Kusuka Makuti**

Kusuka makuti ni kutengeneza makuti ambayo hutumiwa kuezeka paa za nyumba na hutumiwa kama mabati. Makuti hutengenezwa kutokana na majani ya minazi yaliyokauka, huwa yanalogheshwa na kushonelewa kwenye mti hivyo kutumiwa kuezeka nyumba. Kazi hii hufanywa na wanawake wakati wa mapumziko ya mchana. Makuti hayo hutumiwa na wenyewe nyumba iwapo zinavuja na pia wanawake huuza makuti hayo ili wapate pesa za kuwasaidia na matumizi mbalimbali. Watu hununua makuti hayo waezeke paa zao za nyumba au hata za biashara. Wanawake wakiwa kwenye kivuli wakifanya hiyo kazi huko Msambweni huimba nyimbo zao. Hodiya ambazo huimbwa huwa wakati mwingine ni nyimbo ambazo huimbwa hata wakati wa harusi na huwa na lengo la kujiburudisha tu. Kwa mfano:

Mwongozaji: *Sheria! Sheria!*

*Sheria mhondo Lungunzu x2*

Wapokezi: *Sheria mhondo Lungunzu*

*Mayo yuno tsawe wahala*

*Magana achigatiya nyumbani*

*Kayafungula mwana kumanina*

*Chivyere mwenehu usiende hivyo*

*Sharia mhondo lungunzu*

#### **Tafsiri:**

Maongozaji: Sheria! Sheria!

Kesho Asubuhi

Wapokezi: Mama huyu babu alichukua pesa akazitia nyumbani

Hakumtuza mwana kumanina kivyere kesho usifanye hivyo

Sheria kesho asubuhi.

(Wimbo 10- kusuka makuti)

*Chivyere wee! Nzala na ayao*

*Mbona ikakuverera*

*Chivyere wee! Nzala na ayao*

*Mbona ikakuverera*

*Mwenye wataka mahari*

*Chiremba na maziya*

*Uchihewa tsetsetse*

*Ukamanya wee pha Kasimu*

*ziphapho chivyere wee*

*nzala na ayao mbona*

*ikakuverera!*

**Tafsiri:**

Kivyere njaa na wenzako

Mbona imekuzidia wewe

Ulitaka mahari, kilemba na maziwa

Ukapewa vyote umejua kwa Kasimu ziko umerudi tena

Kivere njaa na wenzako mbona imekuzidia!

(Wimbo 11- kusuka makuti)

*Nkaangirwaaa! Nkaangirwa*

*Nkaangirwa mayo ho nkaangirwa*

*Mchetu wakoma mayo wee*

*Anahulwa mizigo*

*Anajita koma wee*

*Anahulwa mizigo*

*Analumwa inchitswa we*

*Anahulwa mizigo*

*Anavunzwa mongomongo we*

*Anahulwa mizigo*

**Tafsiri:** Ametishiwa mama

Ametishiwa na mwanamke mwendawazimu

Anatuliwa mizigo

Anapandishwa wazimu

Anatuliwa mizigo

Yuaumwa na kichwa

Anatuliwa mizigo

Yuavunjwa uti wa mgongo

Anatuliwa mizigo.

(Wimbo 12- kusuka makuti)

Nyimbo hizi tatu huimbwa na wanawake wa Kidigo wakati wanapokuwa wakisuka makuti. Katika kufanya kazi yao ifane basi huwa wanajiburudisha na nyimbo za Kidigo za kiasili na nyingine ni za harusi nyingine ni za kufukuza mashetani basi huziimba kwa lengo la kujiburudisha, kujielimisha na hata kukejeli tabia fulani kwenye kijiji chao. Hodiya hizi huimbwa ili kukashifu tabia hasi na uvuvi katika jamii. Nyimbo hizi pia zinainmbwa wakati wa kufanya kazi kwa lengo la kuwapa watu ari ya kuendelea na kazi.

## **2.1.5 Nyimbo za Hodiya za Uvuvi**

Nyimbo ambazo huimbwa na wavuvi katika shughuli zao za uvuvi hurejelewa kama kimai. Wanaume wa kidigo wa Msambweni wanapokuwa huko baharini wakivua samaki huwa na uchovu na usingizi mwingi sana. Hivyo basi wao hujiburudisha na kuondoa usingizi kwa kuimba nyimbo

mbalimbali wasihisi uchovu wala usingizi wakiwa wametulia na kufanya kazi yao ya uvuvi. Tutaangazia nyimbo ambazo huimbwa na wavuvi ili kupambana na changamoto za baharini.

Mwongozaji: *Richa Richa chiruwa*

*Cha matsere*

Wapokezi: *Maimbi hiya maimbi higo*

*Haya nabwa nago sawa*

Mwongozaji: *Maimbi hiya maimbi higo*

*Haya nabwa nago sawa*

Wapokezi: *Maimbi hiya maimbi higo*

*Haya nabwa nago sawa*

*ukapata haya ukakosa haya*

*Maimbi higo haya nabwa nago sawa*

### **Tafsiri:**

Mwongozaji: Wacha wacha kiluwa cha mahindi

Wapokezi: Mawimbi haya mawimbi

Haya naanguka nayo sawa

Ukipata sawa ukikosa sawa

Haya mawimbi haya naanguka nayo sawa

(Wimbo 13- uvuvi)

Mwongozaji: *Chivyere ajenio hana haa*

Wapokezi: *Mayo rero haa rero akedzu*

*Kanya mlomooo*

Mwongozaji: *Unachibako shaunvuo sino*

*Idikedza tutamusana*

*Unayanya ganya shabinado*

*Sino ukedza tulamusane*

Wapokezi: *Tulamusane*

Mwongozaji: *Una uchoyo shaunyoo*

Wapokezi: *Sino ukedza tulamusane*

### **Tafsiri**

Mwongozaji: Kivyere wageni wako hawa

Wapokezi: Mama leo haa leo wamekuja

Kanya mdomo wako

Mwongozaji: Uko mchokozi shauri yako sisi tumekuja

Wapokezi: Tusalimiane

Mwongozaji: Una choyo shauri yako

Wapokezi: Sisi tumekuja tusalimiane

(Wimbo 14- uvuvi)

*Kata nguooo umphirikire maayo*

*Ye mwenye anazarai nyumbani kwa*

*Chorirooo. Anaona haya aya ni*

*bumu bumu. Kura ni mchina, kura ni chitenge*

*Akachita gonga nyumbani phahi pkwa chirirooo*

### **Tafsiri**

Nunua nguo umpelekee mama.

Mama amezirai nyumbani kwa kilio.

Anaona haya wenzake wamevaa nguo mpya

Mali ya kichina na kitenge.

Ameshika tama nyumbani kwa kilio.

(Wimbo 15- uvuvi)

Wimbo wa kwanza ambao tumeurejelea katika sehemu hii unaashiria kuwa ni ombi ambalo linafanywa na wavuvi ili kuwa tayari kukabiliana na changamoto za baharini kama vile mawimbi na kukosa kupata samaki. Wimbo huu huimbwa muda wa swala ya alfajiri wanapowania kurudi ufuoni kabla ya swala ya alfajiri. Wavuvi wanaonyesha sala yao na kusema kuwa bahari inahusishwa na changamoto nyingi na huenda hata wakakosa kukamata samaki na hivyo wanaimba kwa kusema kuwa watakabiliana na hali yoyote hata kama watakosa kuvua. Wimbo wa pili unakashifu uchoyo. Uchoyo ni hali ya kutotaka kula na wengine. Kwa hivyo basi, wavuvi wanatiana moyo na kuonyesha kuwa wanapaswa kutia bidii ili wavue samaki wengi na wapate kuwagawia watu wengine. Wimbo wa tatu pia huimbwa na wavuvi huko baharini wanapokuwa wakivua samaki kwa ajili ya kufukuza mashetani baharini. Wavuvi huamini mashetani haya ndio husababisha mawimbi makali ambayo huwaangamiza wenzao. Wimbo huu pia unaonyesha changamoto ambazo wavuvi hupitia baharini.

### **2.1.6 Nyimbo za Hodiya za Kugema**

Wanaume wa Msambweni pia hujipata kwenye shughuli ya kugema tembo kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Kazi hii hufanywa asubuhi saa kumi na mbili hadi saa moja na nusu na saa sita hadi jioni. Sio Wadigo wote walio na minazi kwa hivyo mtu huenda kuomba ruhusa kwa mtu mwenye minazi akipewa huanza kazi hiyo. Katika maelewano huwa kuna siku za mwenye minazi na siku za mgema. Yaani akiuza tembo kwenye siku si zake basi hizo pesa hupewa mwenye minazi halafu siku zake zikifika huchukua pesa hizo. Wakiwa katika kazi hizo za kugema hujishughulisha na kuimba na hata kupiga mbinja kwa lengo la kuwaondolea uoga. Huko juu ya minazi ni mbali na kuna hatari za kuwa pengine kuna nyoka, nyuki au hata kuanguka. Katika hali ya kuondoa mawazo na kujiburudisha wakiwa kazini mwao huimba nyimbo kama zifuatazo.

*Mwongozaji: Naphiya mndani nkarinde maruwa kunde zinasira mlamu niendeze*

*Mpokezi: Niendeze mimi dede nkakala bung'o kurinda maruwa x 2*

*Naphiya mndani nkarinde maruwa kunde zinasira mlamu niendeze*

*Niendeze mimi dede nkakala bung'o kurinda maruwa x 2*

*Mwongozaji:*           *Nkakala bung'o kurinda maruwa wee*  
*Rero narinda maruwa*

**Tafsiri:**

Mwongozaji:       Naenda shambani nikalinde maua  
                         Kunde zinaisha shemegi

Wapokezi:           Nifanyeje mimi dada  
                         Nimekuwa bung'o nalinda maua

Mwongozaji:       Nimekuwa bung'o kulinda maua  
                         Leo nalinda maua.

(Wimbo 16- kugema)

Juma lola lola dedee x 2  
Kurusa kuna tabu lola dedee  
Uchifikiri dini ahera kuna mambo  
Roho zindapheya x 2  
Mbere ya Mungu

**Tafsiri**

Juma oa oa kakaa x 2  
Kutongoza kuna shida oa kaka  
Ukifikiri dini ahera kuna mambo  
Roho zitaenda x 2  
Mbele ya Mungu.

(Wimbo 17- kugema)

*Naihwa ni mayooo*  
*Dzombo ni kuree*  
*N'tsape naphi ko*  
*Nyikaa kuna adzomba*  
*Naihwa ni mayoo*  
*Dzombo ni kuree*  
*Nitsape naphi ko nyikaa*  
*Kuna adzombaa*

**Tafsiri:** Naitwa na mama  
Dzombo ni mbali  
Nipite na wapi na huko nyikani kuna ‘ageryenge’. Watu wenye lugha tofauti na wao hata wakiongea hawaelewani.

(Wimbo 18- kugema)

Hodiya hizi ambazo huimbwa wakati wa kugema zinaashiria changamoto za ugemaji na pia matarajio ya wanaogema. Mgema hupanda juu ya mnazi na hivyo wanaweza kuona kila mahali huku chini. Kwa sababu hiyo basi, huimba wimbo wa pili ambao tumeurejelea kwa lengo la kuwaelezea wanawake walioko chini wasiogee mtoni kwa kuwa wataonekana. Wavulana ambao hawajaoa bado wanahimizwa kuoa ili wawe na kizazi kwa sababu anaweza akafariki wakati wa kugema. Pia, wavulana wanashauriwa kuoa ili wasije wakawatongoza wasichana ambao tayari uchi wao umeonekana wakati wanapokuwa wakioga mtoni. Ikumbukwe kuwa dini ya Uislamu huwahitaji wanawake kujisitiri wasije wakaonyesha sehemu zao za mwili. Kwa hivyo basi, waimbaji wa nyimbo hizi wanaendeleza taratibu za dini yao kwamba mvulana anapaswa kuoa mwanamke ambaye amejisitiri na pia aoe mapema ili pate kizazi kabla ya kuangamia. Sehemu ifuatayo tunaangalia nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu.

## **2.2 Nyimbo za Hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu**

Waswahili wa Jomvu Kuu wanatumia lahaja ya Kijomvu katika kuzungumza Kiswahili. Hata hivyo, katika utafiti wetu hatujazingatia lahaja ya Kijomvu kwa sababu utafiti wetu haukuhusisha

mambo ya lahaja. Kwa hivyo katika kuandika nyimbo zetu, hatukuzingatia lahaja bali katika nyimbo zao za kazi, tuliandika kwa Kiswahili sanifu bila kuzingatia lahaja ya Kijomvu. Wajomvu nao kama walivyo Wadigo hufanya kazi mbalimbali ili kujikimu kimaisha. Kazi zinazofanywa na wanaume ni uvuvi na ugemaji. Hizi ni kazi ambazo huwasaidia kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Wanawake nao kwa upande mwingine hufanya kazi ya ufinyanzi, kutwanga na hata kusaga mahindi. Ukulima hufanywa na Waswahili wa jinsia zote mbili. Katika utafiti wetu tulijikita katika nyimbo zao za hodiya za ukulima, uvuvi na kugema kwa wanaume na kazi ya kutwanga, ufinyanzi na kusaga mahindi kwa upande wa wanawake.

### **2.2.1 Nyimbo za Hodiya za Uvuvi**

Waswahili wa Jomvu Kuu wanajulikana sana kwa kazi ya uvuvi. Makao yao hususan ni huko kwenye ufuo wa bahari ya Hindi. Kwa vile wanaishi karibu na bahari bila shaka shughuli kuu ya wanaume ya kujikimu kimaisha ni uvuvi. Tuligundua kuwa shughuli ya uvuvi hufanywa usiku ili kukesha baharini wakivua samaki. Samaki hao huwa ni wa kitoweo chao cha nyumbani na pia wa kuuza ili kujikimu kwa mahitaji mengine ya kimaisha. Tulibaini kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu hupitia hali ngumu ya maisha na hivyo hulazimika kula chakula mara mbili tu kwa siku. Wao hunywa kiamsha kinywa wanapotoka baharini asubuhi. Chakula hicho hutayarishwa mapema ili wapate muda wa kupumzika na kulala. Pia hii huwa ni baada ya shughuli za kuuza samaki kwa wachuuzi huko ufuoni mwa bahari wakati wa asubuhi. Wanaume hawa wanapokuja nyumbani huja na kitoweo ambacho hutayarishwa kwa ama kukaangwa au kupikwa. Huu mchuzi wa samaki hutolewa na chakula chao cha jioni ambacho hutayarishwa mapema na wake zao. Kufikia alasiri chakula cha jioni huwa kiko tayari na hupakuliwa ili wale mapema na kuwapa nafasi waume zao kuenda baharini kuvua samaki tena.

Kazi yao huwa ni ya kukesha baharini usiku kucha. Kukesha ni kazi ngumu na hatari kwa maisha yao. Hivyo wakiwa huko baharini inawalazimu wajipe shughuli za kuwafanya wasihisi usingizi na uchovu bali waendelee kujizatiti na kazi yao. Hii inawezekana kwa kupiga gumzo sana na kuimba nyimbo za kuwafanya kuondoa usingizi na uchovu. Kwa hivyo wavuvi hao huimba nyimbo za kazi kama zifuatazo.

*Pweza kamwambia ngisi tupite tukimaizi.*

*Maji yakiacha mwamba tutafutwao nsisi.*

*Ngisi tuache tupite.*

(Wimbo 1- uvuvi)

Wimbo huu huimbwa huku wakiwapiga vijembe wale watu wengine ambao wana tabia ya kuingilia mambo yasiyowahu. Wao huwakejeli sana watu wenyewe kujihusisha na mambo yasiyokuwa yao. Huimba wimbo huo huku wakiwa wanaendelea na kupiga kafi. Kwa hivyo huwa wako makini na hatari inayowakabili wakiwa humo baharini. Kuna hatari ya dau kupinduka na kuwafanya waangamie hivyo huwa wanahimizana na kupiga kafi na huku wakitia nyavu na kutoa wanapokuwa wameshika samaki. Kwa hivyo inawapasa wawe chonjo sana wasipoteze maisha yao. Hii ni kwa sababu huwa wako huko katikati ya bahari na iwapo lolote la hatari litatokea inakuwa vigumu kwa mtu kuogelea hadi ufuoni mwa bahari. Mara kwa mara wengi wao hupoteza maisha yao katika harakati za kuogelea hadi mwisho. Wimbo mwingine ambao wao huimba wakiwa uvuvini mwao ni:

*Jomvu si mbali*

*Mwendo wa saa moja na mbele*

*Kuna kiwiko*

*Twendeni mkiningoja msikengwe*

*Ni Kanuke mwana kumuiza koja.*

(Wimbo 2- uvuvi)

Hii ni hodiya ya Waswahili wa Jomvu Kuu ambayo huimbwa na wavuvi wanapokuwa wakivua samaki. Wavuvi huimba nyimbo mbalimbali ili kukabiliana na hatari za baharini na hata kutiana imani kwamba Jomvu Kuu sio mbali hivyo wasikimbiane hasa wanapokwenda kwa pamoja. Mambo yao huwa ni ya kushirikiana na kuyafanya kwa pamoja. Iwapo kutakuwa na yule hataki kushirikiana na wenzake huimbiwa na kurejelewa kama ‘Kanuke’ ile akome tabia ya kutotaka kushirikiana na wenzake. Wimbo mwingine ambao Waswahili wa Jomvu Kuu huimba wakiwa kazini mwao katika uvuvi ni kama ufuatao:

*Aendaye Tanga ni nani*

*Akaniitiye Swalehe, kero hakubwaga zani*

*Kuchenza ngoma pekee*

*Kucheza ngoma pekee na jeuri tele*

*Utadhani hana watu kero*

*Hukubwaga zani kucheza ngoma pekee.*

(Wimbo 3- uvuvi)

Tukiangalia hata hizi nyimbo zao za hodiya zinapiga vita sana mambo ya mtu kufanya jambo pekee. Wao hufurahia jambo la kufanya kwa ushirikiano. Wao ni watu wapendanao na kwa hivyo shida ya mmoja ni ya watu wote. Na iwapo utaonekana hushirikiani na wenzio, basi utakuwa adui kwao na utaimbiwa wimbo unaokashifu tabia hiyo hasi.

## **2.2.2 Nyimbo za Hodiya za Ukulima**

Mbali na uvuvi, Wajomvu nao hujihusisha na kilimo cha nafaka kama vile mahindi. Waswahili wa Jomvu Kuu hujishughulisha na ukulima kwa sababu ya uhaba wa kazi. Wengi wao hulima kwenye makonde yao na kupanda vyakula vyta kuwasaidia kwa matumizi yao ya kila siku na baadhi hufanya kazi katika makonde ya watu wengine ili kupata pesa. Wakiwa katika kazi ya kulima, huimba wimbo kama ufuatao:

*Abdalla Mwijaa usifanye jeuri*

*Ukafanya kama yule sote Jomvu*

*Tatu na tule. Ulafi na uroho sote tule*

(Wimbo 4- kulima)

Wanapofanya kazi ya ukulima huhimizana na kukanyana dhidi ya ulafi ambao husababisha kuwepo kwa upungufu wa chakula. Hapo ndipo mhusika Abdalla anaambiwa kwa kumshawishi asifanye ujeuri wakati wa kufanya kazi ya ukulima bali atie bidii. Tabia ya ulafi huisha tu pindi chakula kinapokuwa kingi. Chakula kikiwa kingi watu wote watakula bila ya uroho kwa sababu kunacho cha kutosha na hata zaidi na hivyo kila mmoja anajua kuwa atashiba. Kwa hivyo wimbo huu unawataka watu wafanye kazi ili waweze kuwa na chakula cha kutosha wakati wote. Wajomvu ni watu wanaoishi karibu na bahari. Kuna ngome zao ambazo wakati wa majilio ya Wazungu walitaka kupokonywa na kuwafanya maskwota. Waswahili wa Jomvu Kuu walitunga wimbo wa kuhimizana wakati wakilima wawe makini na hao Wazungu wasije wakapokonywa ngome zao.

Waliimba nyimbo zifuatazo kuhimizana dhidi ya kuzembea kisha hatimaye kufanywa maskwota na pia kupigana kwa sababu ya chakula:

*Kuna Saidi Halifa na Saidi Barahashi*

*Mzungu ataka ngome*

*Ngome ataipatapi*

*Asipate kwa nini na Saidi Halifa ako.*

*Hivyo Wazungu wanaeza pata ngome*

*Kwa ushirikiano wa Saidi Barahashi.*

(Wimbo 5- kulima)

*Karibuni wafalume, hii ndio Jomvu Kuu.*

*Jomvu yetu ya mashimo yatumiza maguu*

*Saidi wa Mbashiri, Mchangamwe mbeko,*

*Alimpiga mamaye kwa kipande cha ukoko.*

(Wimbo 6- kulima)

Wimbo wa tatu huimbwa kwa lengo la kukashifu kitendo cha kumpiga mama kwa sababu ya chakula. Hii inaonyesha kuwa njaa huweza kuwafanya watu kung'ang'ania chakula na hata kupigana. Hapa Wajomvu wanaimba huku wakimkejeli Mchangamwe mwenye alimpiga mamaye kwa kipande cha ukoko. Hii ni ishara ya kuvutana kwa chakula ambacho ni kichache. Mama na mwanawe wanapokonyana kipande cha ukoko. Mwisho mama anashindwa nguvu na baadaye anapigwa na mwanawe kwa sababu ya kipande cha ukoko. Hili ni jambo la aibu ambalo halistahamiliki na ni mwiko kwa Wajomvu. Kwa hivyo basi wimbo huu huimbwa ili kuwahimiza watu wajikaze kwenye mashamba yao kwa lengo la kupata chakula cha kutosha kwa imani kwamba chakula kikipatikana dhiki kama hizi hazitakuwepo. Tumeshughulikia nyimbo ambazo huimbwa na Waswahili wa Jomvu Kuu wakati wanalima. Tumeonyesha kuwa wawe hizi huwaburudisha na kwa wakati huo huo kuelimisha na kuonya dhidi ya tabia fulani hasi. Sehemu ifuatayo tunaangazia nyimbo ambazo huimbwa wakati Waswahili wanapogema.

### **2.2.3 Nyimbo za Hodiya za Kugema**

Kazi ya kugema ni kazi ambayo mtu hufanya kwa minajili ya kupata pesa za matumizi au hata ni biashara. Kugema ni kazi ambayo inahusu kufunga kibuyu kwenye mnazi katika tawi changa kisha kukinga tembo ambalo hudondoka pole pole mchana kutwa na usiku kucha. Mgema huchukua tembo hilo asubuhi na jioni. Mchana hukwea huo mnazi kuenda kuchonga lile tawi vizuri ili tembo liendelee kutona. Wajomvu wakiwa katika shughuli hiyo ya kugema huimba nyimbo ili kuondoa uoga ambao mtu huwa nao. Vile vile, huimba ili kuwajulisha watu kwamba juu ya mnazi kuna mtu na iwapo anataka kujisaidia hapo karibu na njia pia ajue kuna mtu juu ya mnazi. Wimbo ufuatao huimbwa na Waswahili wa Jomvu Kuu wanapogema:

*Unatembo tamuu weee una tembo tamu*

*Unatembo tamu weee u mnazi wa jaka x 3*

(Wimbo 7- kugema)

Mgema huimba wimbo huu kujiburudisha na kujitia moyo kuwa tembo lenyewe litakuwa tamu na hivyo litapata mtu wa kununua. Mgema pia huimba wimbo huu ili kuwajulisha wateja wake kwamba tembo liko tayari. Wimbo huu una sifa ya urudiaji na ni mfupi. Mgema anauimba akiwa anayarudia maneno kwa lengo la kujifurahisha na vile vile kuwajulisha wanaotumia tembo kuwa litakuwa tamu na hivyo wawe tayari kulinunua. Mfano mwingine wa wimbo unaoimbwa na Wagema Waswahili wa Jomvu Kuu wakiwa wanagema ni kama ufuatao:

*Na hii Fotijizazi ndo nyumba namba wani*

*Hata Wazungu wakija mpaka waingie ndani kisha watoke na nje waitizame gadeni*

*Na hii fotijizazi imepandwa na maua.*

*Ili Wazungu wakija, wapate kufurahia.*

*Kisha waipige picha waipeleke Ulaya.*

(Wimbo 8- kugema)

Wimbo huu unaonyesha kuwa wanafurahia mandhari ya Mombasa ambayo Wazungu pia huyafurahia wanapotembea huko. Wazungu hawa wanapofika Pwani hupiga picha hapo Fotijizazi na kuenda nazo kwao na kuweka kumbukumbu ya mandhari ya kupendeza ya Mombasa. Mgema hujifurahisha na kujiburudisha akiwa kazini kwake na wimbo huu hasa kwa kuwa wanayafurahia

pia mandhari hayo. Wimbo mwingine ambao pia huimbwa na Wagema wanapofanya kazi ya kugema ni:

*Njooni Jomvu madafuni,*

*Misheni na hata Jomvu Kuu,*

*Mufurahie madafu, Maji ya mnazi,*

*Babangidaa Mwinyikombooo mnywe maji ya madafu na mnazi.*

(Wimbo 9- kugema)

Hodiya hii huimbwa na wagemaji ambao huangua madafu. Wimbo huu huburudisha wanaokuwa wakiangua madafu kwa lengo la kuwaeleza wanunuzi kuwa madafu yako tayari. Wimbo huu pia husaidia katika kuwatia shime ya kuendelea na kazi. Wimbo huu unamfurahisha akiwa kazini mwake vile vile akitaja wateja wake maarufu na hili humpa moyo kuwa atayaiza madafu yake. Waswahili wa Jomvu Kuu na hasa wanawake husaga mahindi pia wakiimba kama tutakavyoshughulikia katika sehemu ifuatayo.

#### **2.2.4 Nyimbo za Hodiya za Kusaga Mahindi**

Kazi ya kusaga mahindi kwa upande wa Waswahili wa Jomvu Kuu hufanywa na wanawake kama ilivyo kwa Wadigo wa Msambweni. Wanawake hawa huimba hodiya mbalimbali kwa lengo la kujiburudisha na kujifurahisha wanapoendelea na kazi ya kusaga mahindi. Vile vile wanawake hawa huimba nyimbo hizi za hodiya kwa lengo la kuondoa uchovu na kuwapa ari ya kuendelea na kazi ya kusaga mahindi. Nyimbo ambazo huimbwa ni kama vile,

*Kibunzi mwakani tupite kwa juu*

*Hebu tupite kwa Pwani twende forodhani tukaoge*

*Babanda babanda singejila ndimi mwamlambaji*

*Fungu la njiwa kapata kibanda nijitie.*

(Wimbo 10- kusaga mahindi)

Huu ni wimbo ambao huimbwa wakati wa Sikukuu ya mwaka mpya wakati ambapo wanawake wa Jomvu Kuu huenda Pwani kuoga na kuanza mwaka mpya. Hata hivyo, tulibaini kuwa wimbo huu pia huimbwa wakati wanawake wanafanya kazi ya kusaga mahindi. Wanawake huimba

wimbo huu ili kuwapa moyo wa kuendelea na kazi wamalize na kisha waende kujiburudisha huko pwani. Mifano mingine ya nyimbo ambazo huimbwa na wanawake wanapokuwa wakifanya kazi ya kusaga mahindi huko Jomvu Kuu ni kama zifuatazo:

*Hakimu Mwamadi na waziri Kombo,*  
*Kamwambie Kombo awakanye watoto wasifanye kondo,*  
*Tundugu moja eee*  
*Twaingia Shela tuwarembo*  
*Ni myyama gani asiye na umbo? x 2*  
(Wimbo 11- kusaga mahindi)

*Nina maneno wee nina maneno ntaka sema*  
*La kwanza tulikite hema*  
*La pili wanajifunga vibwebwe wawe na hema.*  
*La tatu kunakuja Warabu wadai watumwa*  
*We tumchezee Khalifa bin Helesi.*

(Wimbo 12- kusaga mahindi)

Nyimbo hizi huimbwa pia na wanawake wakiringiana wakati wa harusi hata mmoja aingie kati aseme tulikita boma. Wakati wa kusaga mahindi mwanamke wa Jomvu Kuu huimba wimbo kama huu akijifurahisha na kazi yake. Wanawake ambaao ni Waswahili wa Jomvu Kuu huimba nyimbo hizi kama hodiya wakati wanapokuwa wakisaga mahindi. Nyimbo hizi zinimbwa wakati wa kufanya kazi ya kusaga mahindi kwa kusudi la kufanya kazi kwa bidii kisha wapate nafasi ya kuburudika. Hii inaonyesha imani yao kuwa watu wanapaswa kuburudika baada ya kumaliza kazi. Kwa hivyo basi, wale wanaozembea kazini hawatapata fursa ya kuenda kuburudika kama wenzao ambaao walitia bidii na kumaliza kazi yao haraka.

## **2.2.5 Nyimbo za Hodiya za Ufinyanzi**

Kazi ya ufinyanzi wa vyungu ni kazi iliyopendwa na Waswahili wa Jomvu Kuu tangu jadi. Wanapenda kufanya kazi hiyo kwa malengo ya kwamba ni vyombo vyatuhusu kutumia nyumbani. Hivyo

kuna mitungi ya kuekea maji ndani ya nyumba. Wanaamini ya kwamba maji yakiwekwa mitunguni huwa baridi wakati wote. Vile vile, kuna vyungu nya kukaangia mchuzi, navyo hujulikana kama vikaango. Waswahili wa Jomvu Kuu huamini kuwa mchuzi ukipikwa kwa kutumia kikaango hicho huwa mtamu sana. Vile vile, kunazo pia liga. Liga ni kama kibakuli cha kupakulia mboga wakati wa kupakua chakula. Vibakuli hivyo vinapendelewa kwa kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu wanaamini kuwa wanapovitumia mboga hazipoi haraka kama kwa sahani zingine za kawaida. Wao pia hutengeza vyetezo ambavyo hutumika kuwekea makaa na kufukiza udi chumbani. Tuligundua kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu hapo zamani walikuwa hawategemei vyombo nya madukani. Wao hujitengenezea vyombo vyao nya nyumbani kwa kutumia udongo. Walijitengenezea mitungi ya kuchotea maji, vyungu nya kupikia sima na kuwekea mboga kama tulivyotangulia kusema mwanzoni.

Kunao Waswahili ambao walipendelea kutumia vitu ambavyo vilikuwa vimefinyangwa bali hawakuweza kutengeneza kwa sababu ya ukosefu wa uelewa au muda wa kufinyanga. Kwa hivyo, watu hawa waliweza kununua bidhaa zilizokuwa zimefinyangwa na wafinyazi mashuhuri wa Jomvu Kuu. Hii ni inaonyesha kuwa ufinyanzi pia ni kazi muhimu ya kujikimu kimaisha. Hadi wa leo, wanawake hao wanapatikana mjini Mombasa maeneo ya Mwembe Tayari. Wengine wako huko Jomvu Kuu kwenyewe wakiendeleza biashara zao za uuzaaji wa vitu vilivyofinyangwa. Waswahili wa Jomvu Kuu wanapokuwa katika kazi ya ufinyanzi hujipata wakiimba nyimbo hizi mbalimbali kuonyesha shida zinazowakabili na vile vile furaha yao. Mfano wa nyimbo hizo za hodiya ni kama zifuatazo:

*Sijaona samaki kutiwa maembe*

*Na kumbe vile kutiwa kisha ikaingizwa thembe.*

*Haifai ni churuzu inga maguu ya ng'ombe.*

(Wimbo 13- ufinyanzi)

Ujumbe wa wimbo huu ni wazi kuwa unakashifu mapishi mabaya. Churuzu ni mchuzi ambao uko maji sana tu na hauna ladha. Waimbaji huimba wimbo huu kwa lengo la kutoa tahadhari kwa wanawake ambao ni wavivu hawataki kuwa makini wakati wa kupika. Wimbo huu unawataka wale wasiojua mapishi vizuri wajifunze kutoka kwa wanawake wenzao. Ni kwa sababu hii ambapo

tunasema kuwa wimbo huu huimbwa kwa minajili ya kuwataka wanawake wajue kupika vizuri. Hodiya nyingine inayoimbwa wakati wa ufinyanzi ni ifuatayo:

*Mliolala amkeni mje mumake kimako*

*Paka wa mwingo ni mwivi*

*Kafunike chungu chako.*

*Mkoko una pevuka kalinoe shoka lako.*

(Wimbo 14- ufinyanzi)

Walengwa wa wimbo huu ni wanaume ingawa unaimbwaa na wanawake ambao ni Waswahili wa Jomvu Kuu. Ujumbe wa wimbo huu unamtaka mwanamume kuwa na bidii kazini ili kupunguza umaskini. Wimbo huu unaonyesha kuwa mwanamume anapaswa kuwa na mali ili mke wake asimwache na kuchukuliwa na mwanamume mwingine kwa sababu ya umasikini. Vile vile, wimbo ufuatao huimbwa kama hodiya ya kukashifu umaskini ambao husababishwa na uvivu.

*Tumasikini hatuna kitu ela mbeleee ndo kazi yetu*

*Twatengeza vyungu ndo tupate sima*

*Tumasikini hatuna kitu*

*Ela mbelee ndo kazi yetu.*

(Wimbo 15- ufinyanzi)

Wimbo huu wa hodiya huimbwa watu wanapokuwa wakifanya kazi kwa nia ya kujiliwaza dhidi ya umasikini walio nao. Wanawake huimba wimbo huu kuonyesha kwamba tegemeo lao ni ufinyanzi wa vyungu na ndio unaweza kuwaondolea umaskini. Wanawake hawa wa Jomvu Kuu ni watu wa matumaini makubwa hata ingawa kazi yao iko chini sana. Majilio ya mitambo mingi ya kutengeneza vyombo vingi vya plastiki na vya glasi kwa matumizi ya nyumbani hayajawavunja mioyo. Wafinyanzi huendeleza kazi zao za ufinyanzi kwa bidii kwa kuamini kuwa ndio njia yao kuu ya kupambana na umaskini.

## **2.2.6 Nyimbo za Hodiya za Kutwanga Mahindi**

Wanawake wa Jomvu Kuu vile vile hutwanga mahindi ili wayasage yawe unga. Wakati wa kutwanga mahindi wao huimba nyimbo mbalimbali za kuwatia shime na kuondoa machovu ili wafanye kazi hiyo kwa haraka. Huimba nyimbo mbalimbali kama zifuatazo.

*Mambo na wenyewe wee*

*Mambo na wenyewe*

*Wenyewe ni sisi*

*Natulikokote wee x 3*

*Ubela ubela*

(Wimbo 16- kutwanga)

*Mwenyewe natwanga kinu change*

*Sitaki shari memwatani kifunge kaniki*

*Kinu change ni mutwanga kwa kishindo*

*Kisha natwanga kwa kishindo*

(Wimbo 17- kutwanga)

*Kinuu kinu*

*Kinu twanga*

*Mama akitwanga atwangaje*

*Nami nikatwanga kama yeye*

*Kinuu kinu*

*Kinu twanga*

(Wimbo 18- kutwanga)

Nyimbo hizi za hodiya huimbwa na wanawake wanapotwanga mahindi kwa ajili ya kusaga na kupata unga. Vile vile, nyimbo hizi zinaashiria ushirikiano wa wanawake Waswahili wa Jomvu Kuu wakati wa kutwanga mahindi na kuonyesha umuhimu wa ushirikiano huo. Nyimbo hizi

huwasaidia wanawake wanaotwanga mahindi katika kupunguza machovu na pia huwapa ari ya kuendelea na kazi yao kwa bidii.

### **2.2.7 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangalia nyimbo mbalimbali za kazi za jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Katika jamii ya Wadigo wa Msambweni, tumeangazia nyimbo kumi na nane. Nyimbo tatu za kazi ya ukulima, ambayo hufanywa na watu wote, wake kwa waume, tukaangalia nyimbo tatu za kazi ya uvuvi ambayo ni kazi ifanywayo na wanaume, nyimbo tatu za kazi ya kugema ambayo pia hufanywa na wanaume. Kwa upande wa wanawake, tumetafiti nyimbo tatu za kazi ya kutwanga, tatu za kazi ya kusaga mahindi na tatu za kazi ya kusuka makuti. Kwa upande wa Waswahili wa Jomvu Kuu, vile vile tumeangazia nyimbo kumi na nane. Miongoni mwazo ni nyimbo tatu za kazi ya kulima, ambayo hufanywa na watu wote wanawake kwa wanaume. Nyimbo tatu za kazi ya kugema ambayo ni kazi ya wanaume na nyimbo tatu za kazi ya uvuvi ambayo ni kazi ya wanaume vile vile. Kwa upande wa wanawake, tumeangazia nyimbo tisa za kazi za wanawake ambapo tatu ni za kazi ya kusaga mahindi, tatu za kutwanga mahindi na tatu za kazi ya ufinyanzi. Nyimbo za hodiya ambazo tumezirejelea zinaonyesha kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni huwa na nyimbo tofauti za kufanya kazi zile zile ingawa ni majirani.

## **SURA YA TATU**

### **MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HODIYA ZA WADIGO WA MSAMBWENI NA WASWAHILI WA JOMVU KUU**

#### **3.0 Utangulizi**

Katika sura hii, tunaangazia maudhui mbalimbali yanayodhihirika katika nyimbo za hodiya za Jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1990), maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi yoyote ile ya fasihi. Wamitila (2008) naye anasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Anaendelea kusema kuwa maudhui hujumuisha dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafunzo na falsafa ya watu mbalimbali. Kutokana na maoni yao tunaweza kusema kuwa maudhui ni mawazo ya kijumla ambayo yanajitokeza katika kazi yoyote ile ya kifasihi. Ima ni mashairi, riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Maudhui ni ujumbe ambao msanii anataka kuupitisha kwa hadhira. Basi hadhira iwe tendi au tuli bora wameupata ujumbe kupitia kwa kuusoma, kuusikiliza au kupitia maongezi ya ana kwa ana. Maudhui ndio mambo ambayo humshughulisha mtunzi wa kazi husika. Katika jamii za Wadigo, kazi za ukulima, uvuvi, kutwanga, kugema na hata kusaga mahindi huambatana na nyimbo. Nyimbo kwa ujumla huwa ni burudani kwao na huwasaidia kuondoa uchovu na kuwatia ari ya kuendelea na kazi. Mara nyingine nyimbo za hodiya huangazia hali halisi inayojitokeza katika jamii husika. Nyimbo za Wadigo na Waswahili huwasilisha maudhui mbalimbali kama tutakavyojadili katika sura hii. Katika sura hii tunaangazia nyimbo ambazo tumezirejelea katika sura ya pili. Kwa sababu ya kwamba katika sura ya pili tulizitaja nyimbo kwa lugha ya kiasili. Katika sura hii, tumetumia tu tafsiri ya nyimbo kwa sababu ya kueleweka na wasomi na hatutarudia wimbo mzima.

#### **3.1 Maudhui ya Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Wadigo wa Msambweni**

Nyimbo za hodiya huimbwa wakati wa kufanya kazi mbalimbali. Nyimbo hizi hutofautiana kisifa kutegemea na aina ya kazi inayofanywa. Nyimbo hizi vile vile huwasilisha maudhui mbalimbali kutoka kwa jamii moja hadi nyingine. Kwa ujumla nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo hubeba maudhui tofauti tofauti kama tutakavyoonyesha katika sura hii.

### **3.1.1 Ushirikiano**

Katika jamii ya watu wanaoishi kwa upendo, umoja na amani, lazima waonyeshe pia ushirikiano katika kutimiza mambo yao. Jamii ya Wadigo wa Msambweni huonyesha ushirikiano wao wa dhati kupitia kazi zao mbalimbali ambazo huwajenga kama jamii moja. Itokeapo ya kwamba mtu amezidiwa na kazi kama vile za shamba, watu huungana pamoja na kuifanya kwa pamoja ili kujenga uhusiano wao.

Watu hulima kikoa; leo watu wanakusanyana na kwenda kwa shamba la mmoja wao na kulima mchana kutwa hadi watakapomiliza konde lake. Siku nyingine wanaenda kwa mwingine. Hivyo basi husaidiana kiasi cha kwamba wakati wa mavuno hakuna anayekosa chakula. Huo ushirikiano huendelea hadi wakati wa kuvuna iwe ni mahindi au mchele; wote huungana pamoja na kufanya kazi hizo pamoja. Wakiwa katika hizo shughuli za kufanya kazi pamoja, iwe ni kulima magugu, kupalilia mahindi au kuvuna mahindi shambani watu huonyesha upendo wao kwa kujitolea kufanya kazi hizo katika mashamba yao na ya wenzao bila kinyongo. Ni wakati kama huu ndipo hujikuta wakiimba nyimbo zao za jadi za kuonyesha upendo na ushirikiano. Mfano wa wimbo wa kuonyesha ushirikiano wakati wa kufanya kazi ya kulima ni:

Mwongozaji:                   Kisu kilipotea nyumbani kwa mganga

                                     Ooh wee! Kilipotea nyumbani

                                     Nyumbani we mganga

                                     Kumekuchaa wee! Kumekucha

                                     Mama kumekucha

                                     Kijembe kinalima mchanga

                                     Ha! Ha! Ha!

Wapokezi:                      Kijembe kinalima mchanga x 3

Katika hodiya hii, maneno “kukacha wee kukacha mayo” yana maana ya ‘kumekucha wee mama kumekucha.’ Watu wanahimizana kwamba kumekucha waende shambani wakafanye kazi kwa bidii. Kwa sababu ya kuonyesha ushirikiano, watu wote wake kwa waume hupatikana mashambani wakifanya kazi zao iwe kulima, kupalilia au hata kuvuna. Hayo huwa ni majira ya kufanya kazi na kila mmoja anapaswa kuwajibika isiwe kwamba mkulima anakosa chakula nyumbani kwake.

Hakuna mtu hupatikana nyumbani masaa ya kazi, labda awe mgonjwa. Wimbo wenyewe unaimbwaa na zaidi ya mtu mmoja maana kuna mwongozaji na mpokezi. Hali hii inaonyesha ushirikiano baina ya wanajamii wakati wa kufanya kazi ya ukulima. Kazi ya ukulima hufanywa na wanawake na wanaume kama tulivyotangulia kusema na hivyo basi ushirikiano unadhihirika baina ya jinsia hizi mbili kuhakikisha kuwa chakula hakikosekani nyumbani mwa mkulima. Ukosefu wa chakula nyumbani mwa mkulima itakuwa kama kinaya na ndio maana wanashirikiana ili wasije wakakaa njaa.

Kazi ya kutwanga mahindi hufanywa na wanawake. Mfano ufuatao ni wa wimbo unaodhihirisha maudhui ya ushirikiano wakati wanawake wanapofanya kazi ya kutwanga mahindi.

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake

kumee magugu na nyasi.

Wapokezi: kumee magugu na nyasi,

magugu na nyasi

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake

kumee magugu na nyasi.

Wapokezi: kumee magugu na nyasi,

magugu na nyasi

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake

kumee magugu na nyasi.

Wanawake hutwanga kwa kupishana na hili ni jambo linaloonyesha ushirikiano baina ya wanajamii. Wakati wanapofanya shughuli hii, hutwanga mahindi kwa muda mrefu bila kupumzika. Kazi hii inahitaji kufanywa kwa muda mrefu bila kupumzika. Ushirikiano baina ya wanawake wanaotwanga mahindi ndio huwawezesha kuifanya kwa muda mrefu bila kuchoka huku wakihimizana kwa wimbo huu. Nia yao kubwa huwa ni kuhakikisha mahindi yanatoka wishwa haraka, hivyo huwa hawapumziki ili kazi iishe kwa haraka. Wanawake wanaonyesha ushirikiano wao kwa kutwanga mahindi ambapo watu wawili hutwanga katika kinu kimoja kwa kupishana hadi mahindi yatoke wishwa. Kama hiyo kazi ya kutwanga inaendelea kwa kupishana, wanawake hao hawapaswi kupumzika haraka ndipo hujipata wakiimba wimbo kama huu ili mtu

asihisi uchovu wakati wa kufanya kazi. Ni katika hali ya kuonyesha ushirikiano huo ndipo kazi huonekana nyepesi japo ni ngumu. Wimbo wenyewe unaonyesha wanawake wanafanya kazi ya kutwanga mahindi kwa ushirikiano. Maneno kama “mundawe naumere tuchi na ndago” yana maana kuwa shamba la asiyependa kushirikiana limee aina ya nyasi ngumu kuzilima ambazo zina mizizi ambayo ni migumu kuichimba. Kwa hivyo mwanamke atajizatiti katika kazi yake ya kutwanga ili katika imani yake shamba lake lisimee hayo magugu magumu.

Nyimbo za kimai ambazo huimbwa na wavuvi baharini pia zimedhihirisha maudhui ya ushirikiano. Wavuvi wanaonyesha ushirikiano wao hasa tukiangalia vifaa vya kuvulia samaki kama nyavu na dau sio wote wako na uwezo wa kuvipata vyombo hivyo. Ila kwa kushirikiana hujipata wakivua samaki kwa pamoja wala mtu hawezi jua mwenye nyavu ni yupi na wa kuazima ni yupi. Hali hii huwatia imani kuwa wanawenza kupambana na dhiki za baharini kwa pamoja. Wimbo ufuatao huimbwa na wavuvi wakati wako baharini wanavua.

Mwongozaji:                   Wacha wacha kiluwa cha mahindi

Wapokezi:                   Mawimbi haya mawimbi

                                 Haya naanguka nayo sawa

                                 Ukipata sawa ukikosa sawa

                                 Haya mawimbi haya naanguka nayo sawa

Ushirikiano wa wavuvi unadhihirika katika wimbo huu ambapo mmoja anaongoza wimbo huku wengine wakiupokea. Kazi ya uvuvi vile vile hufanywa kwa ushirikiano kama vile wakati wameshika samaki mtu mmoja anaweza kushindwa kuinua nyavu kutoka baharini na ndio maana wao hushirikiana katika kila shughuli ya uvuvi. Ushirikiano wa wavuvi pia huwawezesha kupambana na mawimbi baharini kwa pamoja. Maneno kama “mawimbi hiya mawimbi haya nabwa nago sawa” yanaonyesha ushirikiano kwa maana kuwa hata ingawa kuna mawimbi makali lakini bado wanapambana nayo kwa pamoja mradi wapate samaki.

### **3.1.2 Umasikini**

Wadigo wa Msambweni ni watu wanaoishi maisha ya hali ya umasikini. Huwa hawana kazi za kuajiriwa bali hutegemea sana kilimo, uvuvi, kusuka makuti na kugema. Hizi ni kazi za kubahatisha kwa sababu zinategemea sana hali ya anga. Kukiwa na kiangazi kwa muda mrefu basi

mazao na mavuno huwa shida sana. Basi wakati wa shughuli za kilimo hujipata wakiimba nyimbo za kazi kama zifuatazo kuwakumbusha na kuhimizana wasipatwe na janga la njaa hadi kula ‘mariga’ ambapo kama tulivyotangulia kusema hapo awali kwamba ‘mariga’ ni kama viazi ambavyo humea msituni na huwa uchungu sana. Wakati wa kiangazi Wadigo wa Msambweni huenda na kuvichimba na kuvishambua na kuvilowesha kwenye maji ya kupita usiku kucha ili uchungu utoke kisha baadaye wavipike kama viazi. Picha hii inayopatikana katika mazingira haya anayoishi Mdigo wa Msambweni inaingiliana vizuri na nadharia yetu ya uhalisia ambayo inahusiana na binadamu na mwngiliano wake katika mazingira anamoishi.

Mwongozaji: Nina njaa mimi nina njaa

Nalimia ‘mariga’ wee x 2

wapokezi: Nina njaa mimi nina njaa

Nalimia ‘mariga’ wee x 2

Mwongozaji: Nina njaa mimi nina njaa

Nalimia ‘mariga’ wee x 2

Wimbo huu unaonyesha umaskini katika jamii kiasi cha kula vyakula ambavyo humea mwituni. Watu wanaoimba wimbo huu wanatiana moyo na hili linawawezesha kupambana na njaa ambayo imewakumba. Kuwepo kwa njaa katika jamii ni ishara ya umaskini. Maneno kama “nanzala” nina njaa, ‘mariga’ viazi vichungu vya msituni vinavyomea vyenyewe vinaonyesha umasikini mkubwa sana. Wimbo huu huimbwa wakati wa kulima ambapo wao hulima kikoa na kuhimizana watie bidii wasije wakapatwa na njaa msimu wa kiangazi. Mfano mwngine wa wimbo unaoonyesha umasikini wa Wadigo wa Msambweni ni huu ambao huimbwa na wanawake wakiwa wanasaga mahindi,

Nasaga viunga vyangu mimi

Leo mimi nikaangalie mkwe wangu

Mgeni akija mpikie sima

Nikaangalie mkwa wangu

Mgeni akija mpikie sima x 3

Maudhui ya umaskini yanajitokeza katika wimbo huu pale ambapo mwanamke anaposema kuwa anasaga “vidzunga”, yaani viunga vichache kwa maana kuwa hana nya kutosha. Mwimbaji wa hodiya hii anasema kuwa anatamani asage unga mwingi lakini kwa sababu ya kwamba hana mahindi ya kutosha inamlazimu asage vichache ili aweze kumpelekea mkwe wake na kisha mgeni akitokea nyumbani apate ya kupikiwa sima. Maneno yaliyotumiwa katika wimbo huu yanaonyesha hali ya umasikini walio nao.

Mfano mwengine wa wimbo unaoonyesha maudhui ya umasikini ni ufuatao:

Mwongozaji:	Sheria! Sheria!
	Kesho Asubuhi
Wapokezi:	Mama huyu babu alichukua pesa akazitia nyumbani
	Hakumtuza mwana kumanina kivyere kesho usifanye hivyo
	Sheria kesho asubuhi

Kawaida ya wanajamii wa Msambweni, msichana anapoposwa na kulipiwa mahari basi ni jukumu la wazazi wote wawili na mashangazi kumtuza kwa kumzawadia vyombo nya jikoni na hata zawadi za nguo ili anapoenda kwa bwanake asionekane wa kuombaomba vitu nya jikoni kama kifumbu, chuma cha chapati, karai na vitu vyinginevyo. Wakati mwengine kwa sababu ya hali ya umasikini, mtu huwa na tamaa ya kula zile pesa bila kumfanya anachostahili mwanawe anapolewa. Hivyo basi wanawake wanapokuwa wanasuka makuti huimba wimbo kama huu kudhihirisha umaskini. Umaskini ndio humfanya mtu kutotimiza anayotakiwa na tamaduni kufanya kama vile kumzawadi msichana aliyeposwa kwa kumpa pesa za kununua vyombo nya jikoni.

### **3.1.3 Bidii na Kukashifu Uvivu**

Uvivu ni hali ya mtu kujilegeza viungo vyake nya mwili kiasi cha kuelekea kufanya kazi kwa ulegevu au hata kutofanya kazi hiyo kabisa. Wadigo wa Msambweni hukashifu sana uvivu kwa kuitia nyimbo zao za kazi. Nyimbo za hodiya za kukashifu uvivu huimbwa na Wadigo kwa lengo la kuwataka wanaofanya kazi watie bidii ili kupigana na umaskini ambao unadhihirika kutokana na ukosefu wa chakula nyumbani na hasa kwa mkulima. Wanawake wanapokuwa wakitwanga mahindi kwa ushirikiano hufanya kazi kwa muda mrefu na kwa sababu wao huwa wawili wawili

basi uvivu hauruhusiwi kamwe ili waweze kukamilisha kazi hiyo kwa wakati ufaao. Wimbo ufuatao unahimiza kuwepo kwa bidii kazini na huimbwa na wanawake wanapokuwa wakitwanga mahindi:

- Mwongozaji: Atakaye choka mume wake  
Hana faida x 3  
Bavyaa
- Wapokezi: Anatembea na kicheko
- Mwongozaji: Mavyaa
- Wapokezi: Anatembea na kicheko
- Mwongozaji: Shemegi yake!
- Wapokezi: Anatembea na kicheko
- Mwongozaji: Shangazi yake
- Wapokezi: Anatembea na kicheko
- Mwongozaji: Atakayechoka mume wake  
hana faida x 3  
wazazi wake wanatembea na kicheko

Wimbo huu unabainisha maudhui ya bidii kwa kila mwanamke anayehusika katika kazi ya kutwanga mahindi. Kila mhusika katika kazi hii anapaswa kujifunga kibwebwe ili asije akachukuliwa kuwa mvivu. Uvivu ndio unaokashifiwa katika wimbo huu. Mathalan, maneno “yenderemwa mlumewe bobolofu” kwa maana ya yule atakayepumzika haraka inaashiria kuwa mumewe ni mtu ambaye hana maana. Kila mwanamke hapendi mumewe aonekane kama mtu ambaye hana maana. Kwa hivyo kila mwanamke hutia bidii wakati wa kutwanga mahindi ili mumewe asionekane mtu asiye na maana. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke mvivu ni fedheha kwa familia yake nzima wakiwemo wazazi wake, mavyaa, bavyaa, shangazi na hata shemeji yake. Maneno yaliyotumiwa katika wimbo huu yanaonyesha kuwa mwanamke anapokuwa mvivu basi anaiaibisha jamaa yake yote. Kwa hali hii basi hakuna mwanamke ambaye atakayetaka jamii yake ichekwe kila mahali wanapopita kwa sababu ya uvivu wake. Wimbo huu ni mwafaka katika kumfanya kila mwanamke anayetwanga mahindi kutia bidii.

Wakulima pia huwa na nyimbo ambazo zinawasilisha maudhui ya bidii na kukashifu uvivu. Zipo wawe ambazo zinaonyesha athari za uvivu kukiwemo kukosa chakula nyumbani mwa mkulima. Mkulima anachukuliwa kuwa mtu asiyetakiwa kukosa chakula nyumbani mwake na iwapo atakosa basi itakuwa inaonyesha kuwa hakutia bidii kama wenzake. Wakulima wanapokuwa wakifanya kazi ya kulima huimba wawe mbalimbali ili kuondoa uchovu na kuwatia shime ya kuendelea na kazi. Wawe hizi pia huwa na maudhui ya kukashifu uvivu na huwataka wakulima kutia bidii wasije wakakosa chakula nyumbani mwao. Kwa mfano,

Mwongozaji:           Kisu kilipotea nyumbani kwa mganga

                         Ooh wee! Kilipotea nyumbani

                         Nyumbani we mganga

                         Kumekuchaa wee! Kumekucha

                         Mama kumekucha

                         Kijembe kinalima mchanga

                         Ha! Ha! Ha!

Wapokezi:           Kijembe kinalima mchanga x 3

Wadigo wanaposema kisu kimepotea nyumbani mwa mganga huwa wanamaanisha chakula kimeisha ndani ya nyumba ya mkulima. Kwa kawaida wakati wa mavuno wakulima hujizolea chakula kingi kutoka kwa mashamba yao na kuweka kwenye uchaga ili wakitumie pole pole na kwa muda mrefu. Wakati mwingine chakula hiki huisha na mara nyingi huwa wakati wa kiangazi. Wakati kama huu ndio muda wao mwafaka wa kutayarisha mashamba yao wakingojea wakati wa mvua. Vile vile wakati washapanda makonde yao huja msimu wa kupalilia mimea yao. Ni wakati kama huu wa kilimo ndipo wao hujipata wakihimizana kwa kupitia nyimbo zao za kazi mbalimbali ili wazidi kufanya bidii katika kulima na kukashifu uvivu ili wasije wakapatwa na njaa tena. Maneno kama ‘kumekucha’ ni ya kuwahimiza wale ambao bado wamelala kuwa wanatakiwa kuamka waende shambani wakalime. Mambo ya mtu kusubiri kuamshwa ndiposa aende shambani ni dalili ya uvivu ambao jamii ya Wadigo wa Msambweni wanaupiga vita sana. Hili linajitokeza katika wimbo ufuatao ambao unaonyesha maudhui ya bidii na kukashifu uvivu:

Mwongozaji: Naenda shambani nikalinde maua  
Kunde zinaisha shemegi

Wapokezi: Nifanyeje mimi dada  
Nimekuwa bung'o nalinda maua

Mwongozaji: Nimekuwa bung'o kulinda maua  
Leo nalinda maua

Wimbo huu huimbwa na Wagema kukashifu wale watu wanaopanda mimea yao na kuiacha iliwe na wanyama na wadudu. Wagemaji wanataja nafaka kama vile kunde ambazo wakulima hupanda na kisha kuziachia wanyama kuzila huko shambani bila kuenda kuzivuna. Hii ni ishara ya uvivu ambayo katika jamii ya Wadigo wa Msambweni haitakikani. Wagemaji huuimba wimbo huu ili kukashifu uvivu unaojitokeza kwa wakulima ambao wanapanda mimea, wanakosa kuishughulikia na kuiacha iliwe na wanyama. Wimbo huu unawataka wakulima waende shambani mwao wakalinde mimea yao dhidi ya wanyama. Hii ni njia moja ya kuwakumbusha wakulima kuwa bidii katika kila hatua ya ukulima ni muhimu ili watu wasikose chakula. Wimbo huu basi unaimbwaa na wagemaji kwa ajili ya kuwakumbusha wakulima kutia bidii katika kila hatua ya ukulima.

### **3.1.4 Biashara**

Wadigo wa Msambweni ni watu ambao wengi wao hawana kazi za kuajiriwa. Wao hujishugulisha na kilimo cha nafaka mbali mbali na biashara ndogo ndogo. Biashara ambayo tunaona imedumishwa sana Msambweni ni ya uchuuzi wa samaki. Wadigo huenda baharini kuvua samaki ambao huwatumia kwa kitoweo chao na wengine huuziwa wachuuzi ambao hununua samaki hao na kwenda kuwauza wabichi au hata kukaangwa na kuuzwa na wanawake kwenye mabeseni au kwenye masanduku. Biashara hii ya samaki imezingatiwa sana na wanawake ambao asubuhi huenda baharini kununua kutoka kwa wavuvi na kwenda kuwakaanga na jioni kuja baharini na masanduku yao wakauze samaki. Vile vile wanaume wale ambao sio wavuvi huenda kununua na makapu yao makubwa na kuzungusha humo mtaani au hata katika barabara kuu inayotoka Vanga kwenda Mombasa.

Vile vile, Wadigo wa Msambweni ni wanabiashara wa kuuza makuti ambayo wanawake husuka na kuyauza kwa watu wengine kwa ajili ya kuezekea paa zao za nyumba. Wanawake wanaosuka

makuti huwauzia wale ambao hawataki dhiki ya kusuka makuti au wale ambao hawana muda wa kufanya kazi hiyo. Hili linajitokeza katika wimbo ufuatao:

Ametishiwa mama  
Ametishiwa na mwanamke mwendawazimu  
Anatuliwa mizigo  
Anapandishwa wazimu  
Anatuliwa mizigo  
Yuaumwa na kichwa  
Anatuliwa mizigo  
Yuavunjwa uti wa mgongo  
Anatuliwa mizigo.

Wimbo huu huimbwa na wanawake wanapokuwa wakisuka makuti na ambayo wao huyauza kwa watu wengine. Pia makuti hayo hununuliwa na wale watu wanaojenga nyumba za watalii huko ufuoni mwa bahari kwa ajili ya kustarehe. Nyumba nyingi za mahoteli ambazo zimeezekwa kwa makuti; wenye hoteli hizo hupata makuti hayo kutoka kwa wenyeji wa Msambweni. Hii ni biashara ya kudumu kwa sababu hayo makuti baada ya kama miaka saba hivi huzeeka kwa sababu ya jua na mvua, hivyo wenye nyumba hizo hulazimika kuezeka paa hizo tena zisije kuvuja wakati wa mvua. Hii ni faida kwa Wadigo wa Msambweni hasa ikizingatiwa ya kwamba wao wako na minazi yao wenyewe ambayo iko na bado wanaendelea kupanda minazi mingine. Vile vile, Wadigo wa Msambweni hufanya biashara ya nafaka wanazopanda hasa mchele. Wakulima huwa wanauza kwa magunia na hasa kwa ndoo. Mchele huo huuziana wenyewe kwa wenyewe. Hali hii huwafanya wasaidiane kwa kupata riziki zao za kila siku. Hii inatokana na kwamba kunao wanaolima mchele mwingi sana karibu gunia arubaini au hata zaidi. Ukweli ni kwamba mtu na familia yake hawawezi kumaliza chakula hicho ndani ya mwaka mmoja.

Vile vile, watu wa Msambweni ni wanabiashara wa pombe kwa sababu tunaona tangu jadi hawa watu wakifanya kazi ya kugema. Hii pombe kwa hali halisi mtu anapoigema sio eti ni kwa lengo la kunywa yeeye mwenyewe bali huiuzia watu ambao nao wanaenda kuchuuza kwa watu wengine. Kiuhalisia dini yao ya Kiisilamu hairuhusu pombe kwa sababu inalevyo, hivyo iliharamishwa

katika dini yao ila kwa sababu hawana kazi na minazi wanayo wengi wao hujitia katika biashara hii haramu. Ndiposa tukachagua nadharia ya uhalisia kuafiki utafiti wetu kwa sababu inashughulikia hali halisi katika mazingira ya mtafitiwa.

### **3.1.5 Umuhimu wa Kupata Chakula**

Kwa kawaida, kila jamii huhimiza watu kufanya kazi. Jamii yenyewe kujizatiti kwa kufanya kazi huwa haina shida ya chakula, pesa na huweza kukimu mahitaji yake yote. Shida kubwa ambayo huikumba jamii inayoonekana inayumba katika umaskini basi ni shida ya upungufu wa chakula. Ukosefu wa chakula huweza kuwafanya watu wakakosa amani kwa sababu wapo watakaoingilia wizi na kuwahangaisha wenzao walio na mali japo kidogo. Ukosefu wa chakula pia husababisha magonjwa kama vile utapia mlo kwa watoto na pia huweza kuwafanya wengine wafe. Hivyo basi, nyimbo za hodiya ni za kutia watu mori wajizatiti kwenye mashamba yao ili wasikose chakula.

Mwongozaji: Shambani ‘chibundani’ hakufikwi kuna nini

Wapokezi: Watu wakifika kunatahiriwa wanawake.

Mwongozaji: ‘Chibundani’ hakufikwi kuna nini

Wapokezi: Kwatahiriwa wanawake

Mwongozaji: Shambani ‘chibundani’ hakufikwi kuna nini

Wapokezi: Watu wakifika kunatahiriwa wanawake.

Mwongozaji: Shambani ‘chibundani’ hakufikwi kuna nini

Katika wimbo huu, waimbaji wanazungumzia umuhimu wa kwenda shambani kufanya kazi ingawa kuna wanyama hatari. Japo huko ‘chibundani’ kwa maana ya shambani kunatisha kwa sababu kuna wanyama hatari hapo ndipo ambapo chakula hupatikana na hivyo basi itawabidi kujikaza na kwenda kufanya kazi. Wimbo huu huimbwa na wanawake wanapotwanga ili kujipa moyo wa kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili wapate chakula. Wanaonyesha umuhimu wa kupata chakula hasa pale wanapoimba wimbo wa kusaga viunga vichache. Kwamba kuna haja ya watu kufanya kazi kwa bidii ili mtu apate chakula kingi badala ya viunga vichache. Zaidi, wanaume wanapokesha baharini wakivua samaki kuhatarisha maisha yao ndani ya bahari ni dalili tosha ya kuonyesha umuhimu wa kupata chakula. Vile vile wanapokuwa wanakula viazi vichungu kwa sababu ya ukame, ni funzo la wazi kwamba kuna haja ya kufanya bidii wakati wa masika ili kuwa

na chakula cha kutosha wakati wa kiangazi. Kwa hivyo basi, wimbo huu unawahimiza watu kufanya kazi licha ya kuwepo kwa changamoto zinazohusishwa na kazi mbalimbali kama vile ukulima na uvuvi.

### **3.1.6 Heshima /Stara**

Heshima ni kitu muhimu ambacho hakinunuliwi dukani bali mtu hukipata kwa kuonyesha stara. Msichana anapaswa kujisitiri hadi atakapoolewa rasmi na bwana ambaye ametambuliwa na wazazi wake wawili. Mtu anapokosa kujiheshimu, basi huchezewa ovyo na mwishowe kupata mimba au hata maradhi ya zinaa. Hivyo wasichana wa Msambweni wanapigwa vijembe kwa kuimbiwa nyimbo wanapopachikwa mimba za mapema. Hili linafanywa ili kukomesha tabia ambazo hazivumiliki kijijini ambapo wasichana na wavulana wanajihuisha na anasa. Mtu anaposikia wimbo kama huo ukiimbwa na unataja jina la mwenzao wanayemjua hata yeze ataogopa kuchezewa na wanaume ovyo ovyo. Maneno kama “chimberembere Fatuma tumbo imberee” hadi jina la msichana linatajwa wasichana huingiwa na uoga na huishia kujiheshimu. Wanawake ndio hupenda kuimba nyimbo za kukashifu mimba za mapema. Mfano ufuatao ni wimbo wa hodiya ambao huimbwa na wanawake wanapokuwa wakisaga mahindi:

Mwongozaji: Kimbelembale Fatuma tumbo imbele x 2

Wapokezi: Kama ni uongo akaulizwe baba mdogo siri yake iligunduliwa  
polee Fatuma polee x 2

Mwongozaji: Twaona ajabu Fatuma kulala na ndugu yake x 2  
polee Fatuma polee.

Kama ni uongo akaulizwe baba mdogo siri yake iligunduliwa  
polee Fatuma pole.

Wimbo huu unakashifu tabia hasi ya msichana kuhusiana kimapenzi na ndugu yake. Mahusiano ya kimapenzi baina ya ndugu ni mwiko kwa jamii. Wanawake wanauimba wimbo huu kukashifu tabia hii kwa kumtaja Fatuma ambaye ametungwa mimba na ndugu yake. Wimbo wenyewe unaonyesha kuwa kitendo hicho ni cha aibu. Vile vile, wimbo huu unaonyesha kuwa ni muhimu kuzingatia mila na desturi za jamii. Katika mila na desturi za jamii ya Wadigo wa Msambweni, ni mwiko kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kaka yako au hata jamaa yako wa karibu. Mila

inakataza tabia hiyo na iwapo mtu atafanya kitendo hiki na kaka yake, basi itakuwa jambo la aibu na fedheha kwake na kwa jamii nzima. Hali hizi japo haziruhusiwi kufanyika lakini bado zinaonekana zikitokea na ndiposa wimbo huu huimbwa kwa kutaja jina la msichana aliyeasi tamaduni za Wadigo. Hii ni hali halisi inayoonekana katika mazingira anayoishi binadamu. Kwamba jambo linakatazwa lakini bado kunao wanaolifanya. Ni katika mazingira haya ndipo tunaona nadharia yetu ya uhalisia ikijitokeza. Kwa sababu tabia chafu kama hizi za wasichana kutungwa mimba na hata ndugu zao huko Msambweni ndipo wanawake wanapokuwa wakisuka makuti huimba wimbo kama huu ili kupiga vijembe na hata kujaribu kukomesha tabia kama hizi ambazo humfanya msichana kukosa stara na heshima.

Wanawake wanapokuwa wakisaga mahindi huimba wimbo wa hodiya ulio na maudhui ya staha na heshima kwa watu wote. Mfano ni hodiya ambayo huimbiwa wanawake ambao hawana heshima na mamezaa wao. Wanawake hawa hudhihirishwa kwa tabia za kupenda kunung'unika wanapopata mamezaa. Kwa hivyo basi, wao huimbiwa wimbo ufuatao wa kukashifu tabia hii ili wawe na heshima nao na wote waheshimiane:

Mwongozaji: Waruka ruka mavyaa

Waruka ruka

Wapokezi: Sema usikizwe

Mwongozaji: Mkaza mwana wa mwanzo

Aliondoka akasonga mbele

Wapokezi: Huyu wa pili naye alifanya kuyapuuza

Mwongozaji: Wacha umbeya mavyaa

Wapokezi: Sema usikizwe

Hodiya hii inakashifu tabia ya mavyaa ambaye anasababisha utengano wa kifamilia kwa watoto wake wa kiume. Wanawake wenzake wanataka kujua sababu ya kukosa kuwashemimu mamezaa wake kiasi cha kuwafanya kuondoka mmoja baada ya mwingine. Katika hali ya maisha ya kawaida, mamezaa na mavyaa ni watu ambao wanastahili kuheshimiana. Ila katika utafiti wetu tuligundua kuwa mavyaa hawasikilizani na mamezaa wao kwa sababu ya kusengenyanana na kunung'unika mara kwa mara. Utapata ya kwamba kijana anaweza kuoa mke wa kwanza kisha akashindwa na maisha ya pale kwa sababu ya mavyaa na akaondoka. Kijana akafanya bidii akaoa

mke wa pili ila naye akaondoka vile vile kwa sababu zile zile za kusengenywa na kuchukiwa na mavyaa wake. Msichana asipopuuza tabia za mavyaa wake basi pia yeye ataondoka aende kwao. Ni tabia chafu kama hizi ambazo huwalazimu wanawake wa Msambweni kuimba wimbo kama huu kujaribu kuwakomesha akina mama wenzao wanapokuwa wakisaga mahindi ili kukomesha utengano wa kifamilia. Maneno yanayotumiwa katika wimbo huu yanawafanya wanawake wasio na heshima na mamezaa wao kuwaheshimu kwa sababu ya kejeli wanazozipata kutoka kwa wenzao.

Wanaume pia huimbiwa hodiya za kukashifu hali ya kutowaheshimu watu wengine. Wanawake wanapokuwa wakisuka makuti hukejeli tabia za wanaume wanaopokea mahari kisha kula bila kuwazawadia watoto wao kama ilivyo ada ya Wadigo. Maneno yaliyotumiwa katika wimbo ufuatao yanaashiria aibu ambayo hutokana na kutotimiza mila za Wadigo zinazohusiana na mahari yanayolipwa kwa msichana. Wimbo wenyewe unakejeli tabia ya wanaume ya kutoheshimu mila baada ya kupokea mahari ya mwanawe. Baba anatakiwa kumzawadia msichana wake aliyelipiwa mahari ili aweze kununua bidhaa za jikoni atakapokwenda kwake.

Mwongozaji:	Sheria! Sheria!
	Kesho Asubuhi
Wapokezi:	Mama huyu babu alichukua Pesa akazitia nyumbani
	Hakumtuza mwana kumanina kivyere kesho usifanye hivyo
	Sheria kesho asubuhi

Wimbo huu huimbwa na wanawake wa Kidigo wanapokuwa wakifanya kazi ya kusuka makuti kwa lengo la kumkejeli mzee ambaye amelipwa mahari na akakosa kumzawadi msichana wake. Wanawake humkejeli mwanamume asiyetimiza mila zao kuitia kwa wimbo unaomkejeli kuwa watu wana njaa ila yake imemzidia kiasi cha kutotimiza mila za Wadigo. Wimbo wenyewe unaonyesha kuwa mzee anajikosha heshima kwa sababu kila asubuhi yuko hapo alipoolewa mwanawe ili apate chakula na hata apewe pesa. Haya yanajitokeza katika mistari ifuatayo ya wimbo sheria ya Mdigo:

Kivyere njaa na wenzako
Mbona imekuzidia wewe

Ulitaka mahari, kilemba na maziwa

Ukapewa vyote umejua kwa Kasimu ziko umerudi tena

Kulingana na mila za Wadigo, msichana anapoolewa sio vizuri kwa wazazi wake kuenda kwake mara kwa mara. Itokeapo ya kwamba yule msichana ameolewa boma ambalo wenyeji wanajiweza kidogo kimaisha na pengine kwo ni masikini basi heshima inadai kuwa hawapaswi kwenda kuombaomba kwake. Mara nyininge hutokea mzee mwenye mwanawe alibahatika na kuolewa kwa matajiri, yeze kila uchao huenda kumtembelea yule binti yake ilhali hii sio heshima kulingana na mila za Wadigo. Wazee wenyen tabia kama hizi huimbiwa na wanawake wa Msambweni wanapokuwa wakisuka makuti alikoolewa msichana kwa lengo la kumtaka mzee husika kudumisha heshima.

### **3.1.7 Busara**

Busara ni maarifa, akili na hekima ambayo hupatikana kwa uzoefu wa muda mrefu. Wadigo wa Msambweni ni watu wenyen busara kubwa inayotokana na ujuzi wao wa kufanya kazi za mikono yao kwa muda mrefu. Wadigo wa Msambweni wamekuzwa na kufunzwa kazi za mikono ambazo wamerithishwa kutoka kwa mababu zao. Vile vile, pia wako na njia za kupitisha ujumbe kwa mtu mwingine kupitia nyimbo zao za kazi, bora ujumbe umfikie mlengwa. Kwa mfano katika wimbo wa kazi ya kuvua samaki “kata nguo” tunapata picha ya mama ameshika tama kwa kuhuzunika kwa sababu wenzake wanunuliwa nguo na wana wao yeze hanunuliwi. Mlengwa wa ujumbe huo atawajibika kwa haraka ili amsaidie mama yake. Wimbo wa kata nguo umpelekee mama ni mfano mwafaka wa kuonyesha na kudhihirisha maudhui ya busara yanavyojitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni. Kwa kawaida, mali ya nguo zinazotoka China huwa ni vitenge, nguo hizo huwa ni nzito. Ni kwa mkabala huo ndiposa tunaona wanawake wazima wakizithamini sana kwa umadhubuti wake. Endapo mwanamke ataona mwenzake amenunuliwa nguo kama hizo na mwanawe na yeze pia mwanaye ana uwezo wa kumnunulia lakini hamnunulii, basi hupatwa na masikitiko makubwa. Katika mazingira yake, mtu anapokuwa mzee ambapo nguvu zimemuishia, huwategemea sana wanawe aliowazaa na kuwalea. Japo hali inapaswa kuwa hivi lakini vile vile kunao watoto ambao huyakwepa majukumu kama haya kwa wazazi wao. Utawapata wazazi wao wakiishi kwenye vibanda na kuva nguo ambazo zimechanika kana kwamba hawana wana waliowazaa. Ni katika mtazamo huu ndiposa tukachagua nadharia ya uhalisia wa binadamu na mazingira yake. Vijana kama hao wanaowapuza wazazi wao hupigwa vijembe kwa wimbo ufuatao ambao huimbwa na wanaume wakiwa uvuvini:

Nunua nguo umpelekee mama.  
Mama amezirai nyumbani kwa kilio.  
Anaona haya wenzake wameva nguo mpya  
Mali ya kichina na kitenge.  
Ameshika tama nyumbani kwa kilio.

Kutokana na wimbo huu ni wazi kuwa wanawake Wadigo wanathamini mali ya Kichina. Wanawake hawa inaonekana kuwa wanatamani sana kununuliwa vitenge na mapambo mengine ya Kichina na watoto wao kama wenzao. Kwa hivyo basi, mama ambaye hapokei mali hii kutoka kwa mwanawe hujawa na kilio na sononeko. Hili ndilo huwafanya wanaume kuwaimbia wenzao wasiowajali wazazi wao wimbo huu wanapokuwa uvuvini. Wanaume hawa wanatumia busara kuwasilisha ujumbe wao kwa wenzao wasiowajali wazazi wao. Matumizi ya busara katika kuwasilisha ujumbe kama huu ni muhimu katika kupunguza chuki mionganoni mwa marika. Mfano mwingine wa wimbo wa kimai wa kuonyesha maudhui ya busara ni ufuatao:

Mwongozaji:	Kivyere wageni wako hawa
Wapokezi:	Mama leo haa leo wamekuja
	Kanya mdomo wako
Mwongozaji:	Uko mchokozi shauri yako sisi tumekuja
Wapokezi:	Tusalimiane
Mwongozaji:	Una choyo shauri yako
Wapokezi:	Sisi tumekuja tusalimiane

Wimbo huu huimbwa na wavuvi wakijaribu kuondoa uchovu na usingizi wakiwa baharini. Hata hivyo, wimbo huu pia hupitisha ujumbe kwa njia ya busara kwa wale wanaume na wanawake wenye tabia za uchoyo. Watu wachoyo hukosa kuwashughulikia wageni wanaowatembelea lakini kwa sababu ya uchoyo wao hukasirika na kununa au hata kuongea maneno machafu kuonyesha kuwa hawapendi wageni. Hii ndio maana wavuvi huimba wimbo huu kuwakanya wenzao dhidi ya uchoyo. Watu wachoyo huambiwa maneno hayo kwa njia ya busara sana kiasi cha kwamba hawatakasirika na hivyo watarekebisha hali hizo.

### **3.2 Maudhui ya Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu**

Waswahili wa Jomvu Kuu huwa na nyimbo za hodiya ambazo huimbwa wakati wa kufanya kazi mbalimbali. Nyimbo hizi huzungumzia hali halisi ya Wajomvu na huwa na maudhui ambayo hukusudiwa kuwasilishwa katika jamii. Kwa hali hii basi, nyimbo huwasilisha maudhui maalum na ambayo yanadhihirisha uhalisia wa wanadamu katika mazingira yao. Katika sehemu hii, tunashughulikia maudhui ambayo yanajitokeza katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu. Tunaanza na umaskini kwa sababu nyimbo zao zinahimiza kufanya kazi ili kukabiliana na umaskini na ukosefu wa chakula na mambo mengine ya kimsingi.

#### **3.2.1 Umasikini**

Waswahili wa Jomvu Kuu ni watu wanaoishi kwenye mkono wa bahari. Wao ni watu ambao hawana kazi ya kuajiriwa na hutegemea kazi za kufanya kwa mikono yao. Wao hutegemea kazi za ukulima, uvuvi na ufinyanzi ambazo haziwapati pato kubwa na hili huwafanya wao kuwekwa katika kundi la masikini. Hali hii ya umasikini inadhihirishwa na nyumba zao wanazoishi ambazo ni duni na mavazi yao duni. Tulipokuwa tukifanya utafiti wetu, tuligundua ya kwamba wao hula chakula mara mbili kwa siku tofauti na jamii zingine ambapo chakula huliwa mara tatu kwa siku. Asubuhi na saa kumi na moja za jioni. Hupika chakula chao mapema kwa ajili ya kujitayarisha ili waume zao waende kukesha baharini wakivua samaki. Hata nyumba zao nyingi zimeezekwa kwa makuti yaliyochakaa na kukandikwa kwa udongo. Wengine nyumba zao zimeezekwa kwa mabati yaliyowekwa kitambo hadi sasa yamegeuka rangi nyekundu na kufanya kutu ila kwa sababu ya umasikini hawawezi kubadilisha hali hii.

Umasikini wao pia unadhihirishwa katika nyimbo wanazoziimba wakifanya kazi zao. Nyimbo zao zingine hutaja wazi kuwa wao ni masikini. Wimbo ufuatao wa wafinyanzi ambao huimbwa wanapokuwa wakifinyanga vyungu unadhihirisha umaskini:

*Tumasikini hatuna kitu*

*Ela mbelee ndo kazi yetu*

*Twatengeneza vyungu ndo tupate sima.*

Wimbo huu unaashiria umasikini ambao unapatikana kwa Waswahili wa Jomvu Kuu. Msamiati uliotumika hapa unaashiria kuwa wao ni maskini na kazi yao kuu ni kufinyanga vyungu ili angalau

wapate chakula. Hii inaonyesha kuwa wao wanafanya kazi za kijungujiko ambazo huwawezesha tu kupata chakula na wala sio mahitaji mengine ya ziada. Mathalan, wanapotumia neno ‘tumasikini’ inaonyesha kuwa wenyewe wanakiri kuwa wao ni masikini. Wimbo huu unaashiria Waswahili wa Jomvu Kuu ambao ni wafinyanzi wanapaswa kutia bidii wasije wakakosa hata chakula cha kawaida kama sima. Sima ni chakula duni sana kwa Waswahili na wala hawaithamini kama vyakula vingine. Ingawa hivyo, kwa sababu ya hali ngumu ya maisha inawalazimu wale hiyo sima ambayo pia huipata kwa shida. Hali hii inadhihirisha umaskini kwa wafinyanzi. Wafinyanzi hawa pia huimba wimbo ufuatao kudhihirisha umaskini:

*Sijaona samaki kutiwa maembe*

*Na kumbe vile kutiwa kisha ikaingizwa thembe.*

*Haifai ni churuzu inga maguu ya ng’ombe.*

Wakati wa kuandaa vyakula, Waswahili hutumia viungo mbalimbali ili kukifanya kiwe tamu. Viungo hivi huuzwa sokoni na madukani. Kwa hivyo basi, watu hupaswa kuvinunua wanapoandaa vyakula mbalimbali kukiwemo samaki. Mchuzi ambao hauna viungo vyovyote hata uwe wa maji tu hauko mzito umetiwa maembe machanga hauthaminiwi na Waswahili wa Jomvu Kuu. Kwa hivyo basi, wapishi wanatakiwa kuwa na viungo hivi wanapopika ili chakula chao kifurahishe. Lakini kwa sababu ya hali duni ya maisha, inawalazimu wale mchuzi uliochuruzika, usiotiwa viungo vinavyohitajika. Tuchukulie ni mchuzi wa samaki wa nazi. Samaki wale kwanza wakiwa wabichi huparwa vizuri. Baada ya kuparwa hutiwa kitunguu thaumu ambacho kimepondwa kikawa laini pamoja na tangawizi mbichi iliyosagwa na huwekwa na kupakwa samaki wale. Baadaye hukarangwa kwa matufa kwenye kikaango hadi kuiva. Kama ni samaki wa kutiwa nazi baadaye kuchanganywa kitunguu maji na nyanya. Mtu huhitajika tena kukaanga na mafuta kidogo na lile rojo la nyanya na vile viungo vingine. Baadaye hutiwa tuwi zito la nazi ambayo huwa imekunwa kwa kutumia mbuzi na kuchujwa kwa kutumia kifumbu na kuchanganywa kwenye samaki wale. Mchuzi huo huwa mzito na mtamu kwa sababu ya viungo mbali mbali lakini kwa sababu ya umasikini wao, baadhi ya Waswahili wa Jomvu Kuu hujipata wakila mchuzi mwepesi ambao wao huulinganisha na miguu ya ng’ombe. Waimbaji wanatumia maneno ‘miguu ya ng’ombe’ kwa kuwa ndio ambayo haithaminiwi wakati wa kula nyama ya ng’ombe kutokana na kuwa ni ngumu na kuchukuliwa kuwa haina ladha. Kwa hivyo basi, Waswahili hawa wanalinganisha mchuzi usiotiwa viungo na miguu ya ng’ombe.

Mfano mwingine wa wimbo wa hodiya unaoonyesha hali ya umasikini ni unaosema kuwa watoto wanakosa kupewa chakula na wazazi wao kwa sababu ya umaskini. Watoto hawa huishia kuwapokonya wenzao walio na chakula kwa sababu pia hawatapakuliwa kule kutokana na umaskini. Wimbo ufuatao unadhihirisha hali hii:

*Hakimu Mwamadi na waziri Kombo,*

*Kamwambie Kombo awakanye watoto wasifanye kondo,*

*Tundugu moja eee*

*Twaingia Shela tuwarembo*

*Ni mnyama gani asiye na umbo? x 2*

Katika wimbo huu, waimbaji wanaonyesha kuwa watoto wanapigana kwa sababu ya kung'ang'ania chakula. Tabia ya kung'ang'ania chakula inaonyesha kuwa hakitoshi na ndiposa wanalahazimika kukiparamia pindi tu wakipatapo. Kama tulivyotanguliza kusema awali, ni kuwa ukosefu wa chakula ni ishara ya umaskini. Watoto wanawapokonya wenzao chakula kwa sababu ya kuwa hawajakula manyumbani mwao na hivyo basi wanapowapata wenzao wakila, hawawaombi bali hukibwakura tu. Vile vile, tunaweza kusema kuwa watoto wanakosa kupakuliwa chakula na familia ambazo zimepata kwa sababu hawana cha ziada kitakachopewa watoto wagoni na hili linadhihirisha umaskini.

### **3.2.2 Ulafi au Uroho**

Uroho ni tabia ya kuwa na tamaa ya vitu na kutaka kupata kwa wingi zaidi kuliko watu wengine. Tabia hii ya uroho huweza hata kumfanya mtu kuwaumiza wengine ili achukue chakula hicho kwa lazima. Tuligundua kuwa zipo tabia za kilafi ambazo Waswahili wanajaribu kuzipiga vita kuitia kwa nyimbo zao za hodiya. Tabia kama hizo mtu akijulikana yuko nazo hujipata akiimbwa kwa kutajwa jina kwenye nyimbo zao za kazi ili kuzikomesha. Waswahili wa Jomvu Kuu wanaishi kama ndugu hivi kwamba wanapopata chakula kidogo wao hukitumia pamoja. Waswahili hawapendi tabia za ulafi na hivyo basi mtu akiwa mlafi hujipata katajwa kwenye nyimbo ya kazi. Kwa mfano wakati wa kulima wimbo unaofuata huimbwa kwa lengo la kukashifu ulafi:

*Karibuni wafalume hii ndo Jomvu Kuu.*

*Jomvu yetu ya mashimo yatuumiza maguu.*

*Saidi wa mbashiri Mchangamwe mwenye Mbeko*

*Alimpiga mamaye kwa kipande cha ukoko.*

Wimbo huu unaonyesha kuwa mtu kumpiga mama yake kwa sababu ya kipande cha utandu ni hali ya ulafi mno. Ukoko ambao ni mabaki ya sima mtu kuyapigania inadhihirisha ulafi. Ingawa hivyo, mhusika Saidi anakosa kuzingatia mbeko za jamii yake kwa kumpiga mamake. Saidi anampiga mamake kwa sababu ya ukoko ambao sio wa muhimu sana kama sima yenewe. Saidi anataka ale ukoko wote na mamake asionje na hii ni tabia ya ulafi. Waimbaji wanaikashifu tabia ya ulafi na kuonyesha kuwa Saidi amekiuka mila na tamaduni zao kwa kumchapa mamake. Mfano mwingine wa wimbo unaoonyesha maudhui ya ulafi na uroho ni kama huu wa kazi ya kulima:

*Abdalla mwijaa usifanye jeuri*

*Ukafanya kama yule, sote Jomvu tatu*

*Tu ndugu na tule.*

*Acha ulafi na uroho*

*Soteni tuleni*

Watu wa Jomvu Kuu ni watu ambao wanaishi kama ndugu. Wao hushirikiana kwa kila hali na hata hula pamoja kama familia kama inavyodhihirika katika wimbo huu. Abdalla anakanywa dhidi ya ulafi kwa kuwa anatakiwa kula kwa utaratibu kama wenzake. Maneno kama ‘sote Jomvu tatu’ yanamaanisha kuwa watu wote wa Jomvu Madafuni, Jomvu Mikanjuni na hata Jomvu Kuu ni watu wamoja wanaoishi kama ndugu. Kwa hivyo kile kipatikanacho wote wanapaswa wale kwa pamoja. Wimbo huu unakataza ulafi na hasa wakati wanakula pamoja ambapo kila mmoja anapaswa kupata kidogo. Mtu anayeonyesha ulafi huimbiwa wimbo huu kwa kutajwa jina lake na hii ni njia moja ya kuwakataza watu dhidi ya tabia ya ulafi ambayo haistahili kuwepo kwa watu wanaokula pamoja.

Waswahili wa Jomvu Kuu pia huimba nyimbo za kuonya dhidi ya ulafi wanapokuwa wanalima shambani. Hii ni iwapo kuna mmoja ambaye ni mlafi kati ya wanaofanya kazi ya kulima. Wimbo hutumiwa kama nyenzo ya kupitisha maonyo dhidi ya ulafi. Ufuatao ni wimbo wa wawe ambao huimbwa kwa lengo la kukataza tabia ya ulafi mionganini mwa wanajamii:

*Mliolala amkeni mje mumake kimako*

*Paka wa Mwingo ni mwivi*

*Kafunike chungu chako*

*Mkokonza unaanza pevuka*

*Kalinoe shoka lako*

Katika wimbo huu, Wajomvu wametumia sitiari kuonya watu walio walafi. Maneno kama ‘Paka wa Mwingo ni mwivi’ sio ati ni paka kweli, bali kuna mtu mlafi katika kundi hilo la wakulima ambaye hula kwa kuiba chakula kabla ya wenzake kufika. Maneno ya wimbo huu yanawatahadharisha watu kumhusu mmoja ambaye huingia chumbani kula wakati wengine hawako. Wimbo huu unaonyesha kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu wana desturi ya kufanya mambo pamoja hata kula. Kwa hivyo basi, anayetangulia chumbani na kula kabla ya wenzake kufika anachukuliwa kuwa mwizi na kurejelewa kama paka. Pia, wanaonyesha kuwa mlafi huyu anapaswa hata kuangamizwa. Kwa hali hii basi, mtu ambaye ni mlafi atajihadhari na kuacha tabia hii mbaya asije akaangamizwa.

### **3.2.3 Ushirikiano**

Jamii ya Jomvu Kuu ni watu wanaopenda kushirikiana kwa kila jambo ikiwemo kazini mwao. Waswahili wana imani ya kwamba wakishirikiana kama ndugu hata adui hawezi kuwasumbua. Kazi zao wanazifanya kwa pamoja kama vile katika uvuvi ambapo utawapata wavuvi wote wako baharini kila jioni wakivua samaki kwa pamoja. Mfano wa wimbo unaonyesha ushirikiano wao ni kama huu wa ‘Pweza kamwambie ngisi.’

*Pweza kamwambie ngisi tupite tukimaizi*

*Maji yakiacha mwamba tutwafutwao ni sisi.*

*Ngisi twaache tupite.*

Pweza ni mnyama anayeishi baharini aliye na umbo la duara na mwenye mikono minane. Ngisi ni mnyama wa baharini vile vile ila anatofautiana na pweza. Ngisi ana kichwa kinachokaa kama ua lililochanua, mikono kumi mirefu na hutoa kioevu cha rangi nyeusi. Kwa hivyo basi, tunaweza kusema kuwa wavuvi wanatumia wimbo huu kuonyesha kuwa wao ni tofauti ila wote wanapitia changamoto sawa. Wimbo unaonyesha kuwa licha ya tofauti zao za kiusuli na hata kimaumbile, wanatakiwa kushirikiana katika kupambana na changamoto za baharini. Kwa hivyo basi, wimbo

huu wa kimai ni wa kuwataka wavuvi kushirikiana ingawa wana tofauti zao na kusiwe na ubaguzi miongoni mwao. Maneno ya kutahadharisha kama ‘Tutwafutwao ni sisi’ huonyesha ushirikiano wao wa pamoja ambapo wanadai kuwa maadui zao huwatafuta wao wote na wala sio mtu mmoja. Wavuvi wanajua ya kwamba kule baharini maji yakijaa kuna samaki wakubwa kama papa ambao ni hatari kwa maisha yao na hivyo wanapaswa kushirikiana kwa pamoja. Kwa ujumla, Waswahili wa Jomvu Kuu huonyesha ushirikiano wao hata katika safari zao za kwenda kwa miguu. Hili linabainika katika wimbo ufuatao:

*Hapa na Jomvu si mbali.*

*Mwendo wa saa moja na mbele kuna kiwiko*

*Twendeni mkiningoja. Usikengwe ni kanuke*

*Mwana kumuiza koja*

Waswahili wanatiana moyo ili kuwawezesha kutembea mwendo mrefu bila kuchoka. Wimbo huu huimbwa wakati ambapo kuna mmoja kati ya wanaotembea kwa miguu anayeonyesha kuchoka. Maneno kama ‘Hapa na Jomvu si mbali’ ni ya kuwahimiza kuwa wanakokwenda sio mbali na basi wanatakiwa kujikaza. Wanaotembea wanatiana imani ya kutembea kwa pamoja na hata kungojana humo njiani ili waonyeshe ushirikiano wao. Mfano mwingine wa wimbo unaoonyesha ushirikiano wao ni ufuatao na ambao huimbwa na wanawake wanapokuwa wakisaga mahindi:

*Kibunzi mwakani tupite kwa juu*

*Hebu tupite kwa Pwani twende forodhani tukaoge*

*Babanda babanda singejila ndimi mwamlambaji*

*Fungu la njiwa kapata kibanda nijitie.*

Awali tulionyesha kuwa wanawake hushirikiana katika kusaga mahindi. Wimbo huu unaashiria kuwa wanapaswa kushirikiana katika kazi hii ya kusaga mahindi kama wanavyofanya wakati wa shughuli zingine kama vile kuoga mwaka na kuanza mwaka mpya pamoja. Wimbo wenyewe unaonyesha kuwa iwapo watashirikiana basi wanaweza wakafanya mambo mengi. Hili linabainika wanaposema kuwa ‘Kibunzi mwakani tupite kwa juu’ kwa maana kuwa wanaweza hata wakatumia ndege na kusafiri mbali wakiwa pamoja na hili linaonyesha ushirikiano wao.

### **3.2.4 Uvumilivu**

Uvumilivu ni hali ya kuwa na subira katika kila jambo. Japo kuna ugumu fulani maishani lakini mja anapaswa awe mstahamilivu, kwani subira huvuta heri. Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu ni watu wenye uvumilivu wa hali ya juu. Kazi ya ufinyanzi wa vyungu ni kazi ngumu kiasi kwa sababu kupata wateja haraka sio rahisi. Isitoshe, hata bei za vyungu vyao ni ya chini. Tuseme kwa ujumla sio kazi ya kutegemewa katika kukidhi mahitaji yao ya maisha. Wao wanaitegemea kwa kiasi kikubwa hata ingawa kwa mtazamo wetu tunaona haifai kutegemewa. Hao wenyewe bado wanathibitisha utegemeo wao wa kazi ya ufinyanzi kwa kuitia hata nyimbo zao za kazi ya ufinyanzi. Wanapokuwa katika kazi ya ufinyanzi, wimbo ufuatao, ‘tumasikini’ huimbwa kuashiria hali yao duni ila wao wana imani ya kwamba mbeleni kutafunguka na umasikini wao waliouvumilia kwa siku nyingi utaisha.

*Tumasikini hatuna kitu*

*Ela mbele we ndo kazi yetu*

*Twatengeza vyungu ndo tupate sima.*

Wimbo huu unaonyesha kuwa wanajua fika kuwa kazi yao ni ya kijungu jiko ingawa wanaifanya. Hali ya kuendelea kufanya kazi kwa bidii na ambayo haina kipato kizuri ni dhihirisho la uvumilivu. Kutokana na wimbo huu wanasema kuwa wao ni masikini ila kutokana na uvumilivu wao, maisha yatatengenea hapo mbeleni. Na huu ndio tunaourejelea kama uvumilivu kwa kuwa wanafanya kazi wakijua kwamba bado wanabaki kuwa masikini. Wafinyanzi wanadhihirisha sifa yao ya uvumilivu kuitia kwa wimbo huu.

Wajomvu ambao hufanya kazi ya ukulima vile vile huimba wimbo unaonyesha uvumilivu. Waswahili wanapokuwa shambani wakilima, huimba nyimbo zinazoashiria kuwa wanapitia hali ngumu na hata ya ukosefu wa chakula nyumbani ilhali wao ni wakulima. Wimbo, ‘karibuni wafalme Jomvu kuu yenye mashimo’ unaonyesha kuwa wanavumilia mahali wanapoishi kwa kuwa ni duni kutokana na namna wanavyoeleza katika misitari ifuatayo ya wimbo huu:

*Karibuni wafalume, hii ndio Jomvu Kuu.*

*Jomvu yetu ya mashimo yatuumiza maguu.*

*Saidi wa Mbashiri Mchangamwe mwenye mbeko.*

*Alimpiga mamaye kwa kipande cha ukoko.*

Wimbo huu wa Waswahili wa Jomvu Kuu unaonyesha hali yao ya kuwa wavumilivu. Wajomvu wanavumilia kukaa eneo ambalo ni duni kwa sababu hawana pesa na hivyo wanalazimika kubaki huko wakivumilia hali duni ya eneo hili. Isinge kuwa kwamba wao ni wavumilivu basi nao wangehamia mijini kutafuta vibarua kama wafanyavyo watu wengine. Jomvu kuu ina maporomoko lakini kwa vile huko ndio kwao wanavumilia kuishi huko na hawana nia kutoka huko maana ndiko wanakokujua kama kwao.

### **3.2.5 Busara**

Waswahili wa Jomvu Kuu wako na busara. Sio rahisi kukosana bila sababu isiyo na msingi. Wakati wakiwa katika shughuli ya kazi ya kulima, iwapo kuna mtu ambaye hupenda kujihusisha na mambo yasiyomhusu huimbiwa wimbo kama huu wa pweza kumwambia ngisi yasiyomhusu aachane nayo. Busara ya Wajomvu pia ilibainika wakati mzungu alipokuja akitaka kuwapokonya ngome yao kwa kupitia baadhi yao, kama Saidi Barahashi, waliwatungia nyimbo watu hao ili wamulikwe na wenzao wasipate kuitoa ngome yao. Wakiwa katika kazi yao ya ukulima, walitumia busara katika kukataa na ngome yao kwa kupitia wimbo kama huu:

*Kuna Saidi Halifa na Saidi Barahashi*

*Mzungu ataka ngome*

*Ngome ataipatapi.*

*Asipate kwa nini na Saidi Halifa ako.*

*Hivyo Wazungu waeza pata ngome*

*Kwa ushirikiano wa saidi Barahashi.*

Wimbo huu uliimbwa na wakulima ili kuwatahadharisha Wajomvu dhidi ya wazungu waliokuwa wakichukuwa ngome za watu na hasa zilizokuwa na rutuba. Busara waliyo nayo iliwawezesha kutunga wimbo ambao uliimbwa walipokuwa wakilima. Wimbo wenyewe unataja baadhi ya watu ambao walionyesha kuwa walikuwa wanashirikiana na mzungu katika kupata ngome za Waafrika. Kwa hivyo basi, waliuimba wimbo huu kwa minajili ya kuwatahadharisha wajomvu dhidi ya watu waliokuwa na ushirikiano na wazungu na ambao wangewatafutia ngome kwa Waafrika. Busara ya

Waswahili wa Jomvu Kuu inabainika hapa kwa kuwa wanaamua kutumia njia mwafaka ya kuonyana dhidi ya wazungu wanaochukuwa ngome zao badala ya kupigana vita nao.

### **3.2.6 Biashara**

Waswahili wa Jomvu Kuu ni watu waliofanya biashara ndogo ndogo. Wanawake hufanya biashara ya kuuza vyungu nao wanaume ni wauzaji wa samaki na tembo. Wajomvu wana tamaa ya kutegeea Wazungu wanaokuja Fotjizazi kutizama gadeni, wanawasifia gadeni yao. Wazungu wanapokuja kutembelea fotjizazi Wajomvu hunufaika. Licha ya kuwa Wajomvu hufanya biashara mbalimbali kama ambavyo tumeonyesha ila pia huwategemea watalii ambao hufika kutazama jengo la kihistoria kama inavyobainika katika wimbo huu:

*Na hii Fotijizazi ndo nyumba namba wani*

*Hata Wazungu wakija mpaka waingie ndani kisha watoke na nje waitizame gadeni*

*Na hii fotijizazi imepandwa na maua.*

*Ili Wazungu wakija, wapate kufurahia.*

*Kisha waipige picha waipeleke Ulaya.*

Wimbo huu unamaanisha kuwa wazungu wanapofika kutazama gadeni, huwapa Waafrika pesa. Hii ni biashara nzuri kwa kuwa wazungu huwapa pesa. Tumeonyesha kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu hufanya biashara za kuuza vyungu, tembo na samaki kama njia ya kujikimu kimaisha. Hata hivyo, kutokana na wimbo huu ambao tumeurejelea tunaweza kusema kuwa wao pia huwategemea wazungu wanaofika pwani katika kupata riziki. Wimbo mwingine unaoonyesha kuwa Waswahili ni watu wa kufanya biashara ni unaoimbwa na wanaouza madafu. Wafanyabiashara huwaita watu kwa kutumia misitari ya maneno kama vile ‘Jomvu Madafuni, Misheni na hata Jomvu Kuu’ ili waje wanywe maji ya madafu na maji ya mnazi ambayo ndio tembo lenyewe. Sio eti watawapa bure, bali watawauzia. Wimbo huu huimbwa na wagema wanapokuwa kazini mwao:

*Njooni Jomvu Madafuni*

*Misheni na hata Jomvu Kuu*

*Mufurahie madafu, maji ya mnazi.*

*Babangidaa, Mwinyikombo*

*Mnywe maji ya madafu na mnazi.*

Kama tulivytangulia kusema kwamba pombe ni haramu, Waswahili wa Jomvu Kuu hutumia busara kwa kuita wanunuzi wa tembo ili isionekane haramu kwao. Wauzaji tembo wanalirejelea kama maji ya mnazi ili wasijulikane kuwa wanaiza tembo ambalo ni haramu. Kwa hivyo basi, tunaweza kusema kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu hufanya biashara ya kuuza vyungu, samaki na tembo ambalo limeharamishwa na serikali na dini wanayoifuata.

### **3.2.7 Bidii na Kukashifu Uvivu**

Nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu pia hukashifu uvivu. Tumetangulia kusema kuwa Wajomvu hushirikiana katika kazi mbalimbali na hivyo basi uvivu hautakikani kwa kuwa itakuwa ni kuwarudisha wengine nyuma. Kwa hivyo basi, Waswahili wa Jomvu kuu hukashifu uvivu wanapokuwa wanafanya kazi mbalimbali hasa zile zinazohitaji ushirikiano. Wimbo ufuatao huimbwa na wanawake wanapokuwa katika kazi ya kutwanga mahindi:

*Mambo na wenyewe we*

*Mambo na wenyewe*

*Wenyewe ni sisi*

*Natulikokote wee x 3*

*Ubela ubela*

Katika wimbo huu, maudhui ya kukashifu uvivu yanajitokeza. Waimbaji wanaimba huku wakifanya kazi kwa pamoja. Wanasema kuwa kazi yenyewe sharti ifanywe na wao na hivyo basi uvivu hautakikani. Kutokana na wimbo wenyewe ni wazi kuwa mwanamke mvivu hukokotwa wakati wa kazi ya kutwanga mahindi. Hivyo akazanishwe viungo asiwe mvivu kwa sababu naye anapaswa kuchangamka kazini kama wenzake. Vile vile wanakashifu uvivu mionganoni mwa mwanamke ambaye anachukuliwa kuwa anaringa na kumtaka kutwanga kwa kishindo. Maneno kama ‘Memwatani kifunge kaniki’ kutwanga kwa ‘kishindo’, yana maana ya kila mmoja anapaswa kutwanga kwa nguvu. Mhusika anayerejelewa kama Memwatani anatakiwa kufunga kinu chake kaniki ili mahindi yasije yakamwagika. Misitari ifuatayo ya wimbo wa hodiya inadhihirisha bidii na kukashifu uvivu:

*Mwenyewe natwanga kinu change*

*Sitaki shari Memwatani*

*Kifunge kaniki kinu change*

*Mi natwanga kwa kishindo*

*Kisha natwanga kwa kishindo*

Mwimbaji anaimba huku akisema kuwa Memwatani anatakiwa kutwanga kwa kishindo kama afanyavyo yeye. Hivi ni kusema kuwa Memwatani hafanyi kazi kama inavyotakikana na kwa sababu wanafanya kwa pamoja basi anapaswa kumuiga mwenzake ili wakamilishe kazi hiyo haraka. Mfano mwingine wa wimbo unaoonyesha maudhui ya kukashifu uvivu ni kama huu unaoimbwa na wanawake wanapokuwa wanasaga mahindi.

*Nina maneno wee nina maneno ntaka sema*

*La kwanza tulikite hema*

*La pili wanajifunga vibwebwe wawe na hema.*

*La tatu kunakuja Warabu wadai watumwa*

*We tumchezee Kalifa bin Helesi.*

Wimbo huu unamaanisha kuwa wanawake wanapaswa kutia bidii ili kuweza kujikimu kimaisha. Vile vile, bidii yao inawawezesha kuwa na mahali pazuri pa kuishi. Wimbo wenyewe unasema kuwa wanawake wajifunge vibwebwe wakite hema. Kazi ya kukita hema ni kazi ya wanaume lakini kwa sababu hao wanawake hawapendi uvivu hata hujifunga vibwebwe wakakita hema kwa ajili ya mipangilio ya harusi. Wajomvu huringiana wakati wa harusi kwa kukita mahema wenyewe wawachezee watu wa kwa mume ambao watakuja kutoa mahari. Kazi hii ya kukita hema ni ya wanaume na inaaminika kuwa sio rahisi bali wanaifanya na hii ni njia moja ya kukashifu uvivu. Kwa mtazamo wetu, baada ya kuwahoji wanawake hao, walituambia kuwa nyimbo hizo ziliimbwa japo zinataja watu wa zamani lakini huwapa motisha ya kufanya kazi zao kwa bidii.

Mfano mwingine wa wimbo unaodhihirisha maudhui ya bidii na kukashifu uvivu na ambaio pia huimbwa na wanawake wakati wanatwanga mahindi unaashiria kuwa mama ni mfano mzuri wa kuiga. Mama yejote anapokuwa na bidii katika kazi hata watoto wake watakuwa na bidii kama huyo mama yao. Ndiposa tunaona mara kwa mara mama akishirikiana na wanawe anapokuwa

akifanya kazi kama njia moja ya kuwafunza na kukashifu uvivu. Wimbo ufuatao unadhihirisha haya:

*Kinuu kinuu, kinuu twanga*

*Mama akitwanga atwangaje*

*Nami nikatwanga vile vile*

*Kinuu kinuu, kinu twanga*

### **3.3 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangalia maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Maudhui yaliyojitokeza katika jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu ni pamoja na umasikini, ushirikiano, ulafi au uroho, busara, bidii na kukashifu uvivu, uvumilivu na biashara. Kwa upande wa Wadigo wa Msambweni, tulipata maudhui kama ushirikiano, umasikini, bidii na kukashifu uvivu, umuhimu wa kupata chakula, imani, heshima na busara. Tumeelezea maudhui haya kwa kutoa nyimbo ambazo zinayawasilisha. Maudhui haya yanaonyesha kuwa kuna mwingiliano mkubwa wa kimaudhui katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Tumeonyesha kuwa nyimbo hizi zinatofautiana katika maneno ila ujumbe unaojitokeza unaelekea kuwa sawa. Tunasema hivi kwa sababu nyimbo ambazo tumezirejelea zimezingatia maudhui ya bidii na ushirikiano zaidi. Katika sura ifuatayo tutalinganisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni.

## **SURA YA NNE**

### **KULINGANISHA NA KULINGANUA MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HODIYA ZA WADIGO NA WASWAHILI**

#### **4.0 Utangulizi**

Katika sura hii, tunalingalisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Katika sura ya tatu, tumeangazia maudhui mbalimbali ambayo yanajitokeza katika nyimbo zinazoimbwa wakati wa kufanya kazi. Katika sura hii basi, tunaangalia iwapo maudhui hayo yanafanana ama yanatofautiana hasa tukizingatia ujirani walionao Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu.

#### **4.1 Kulinganisha Maudhui Yanayojitokeza katika Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni**

Tumetanguliza kusema kuwa Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu ni majirani. Tumeonyesha nyimbo ambazo wao huimba na kuchanganua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo hizo. Katika sehemu hii, tunashughulikia maudhui sawa yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za Wadigo na Waswahili vile vile.

##### **4.1.1 Umasikini**

Kutokana na data ya utafiti wetu, tuligundua kuwa umaskini unajitokeza katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Maudhui haya yanajitokeza katika nyimbo za wawe zinazoimbwa na Wadigo wanapokuwa wakilima shambani. Kwa upande mwingine, Waswahili wa Jomvu Kuu wanapokuwa wakifinyanga vyungu huimba wimbo unaoonyesha umaskini wao. Nyimbo hizi zinaashiria kuwa Wadigo na Waswahili wanajikakamua sana kupiga vita umasikini lakini bado hawajasaidika. Umaskini unadhihirika katika nyimbo ambazo huimbwa wakati wa kufanya kazi mbalimbali kama vile ufinyanzi, ukulima, uvuvi na ugemaji. Waimbaji wanazungumzia umasikini ambao umewalemea ingawa wanaonyesha kuwa wana imani kuwa mambo yatabadilika. Nyimbo zifuatazo ambazo tumekishazirejelea zinadhihirisha maudhui ya umaskini katika jamii ya Wadigo na Waswahili:

Mwongozaji: Nina njaa mimi nina njaa  
Nalimia ‘mariga’ wee x 2

wapokezi: Nina njaa mimi nina njaa  
Nalimia ‘mariga’ wee x 2

Mwongozaji: Nina njaa mimi nina njaa  
Nalimia ‘mariga’ wee x 2

(Wadigo, wanapolima)

Nasaga viunga vyangu mimi  
Leo mimi nikaangalie mkwe wangu  
Mgeni akija mpikie sima  
Nikaangalie mkwa wangu  
Mgeni akija mpikie sima x 3

(Wadigo, wanaposaga mahindi)

Umaskini unajitokeza katika nyimbo hizi mbili za Wadigo wa Msambweni. Waimbaji wanasesma kuwa wanazimika kula ‘mariga’ kwa sababu wana njaa. Njaa ni dhihirisho la umaskini kwa sababu wanashindwa kununua chakula na badala yake wanaenda kutafuta mizizi ya mwituni ambayo inaweza kuwadhuru wasipoikausha vizuri. Wadigo wa Msambweni wanazimika kula ‘mariga’ viazi vya msituni ambavyo humea vyenyewe, wao hulazimika kuvichimba na kuvilowesha kwenye maji vitoke uchungu uliomo kisha wanavipika kama viazi washibishe matumbo yao. Vile vile, maudhui ya umaskini yanadhihirika katika wimbo wao wa kusaga ‘vidzunga’ yaani viunga vichache kupata chakula na hii inatokana na umaskini walio nao. Katika wimbo wa pili pia, wanawake Wadigo wanaosaga mahindi wanasesma kuwa wanazimika kupika sima na hii inashiria umaskini. Sima ni chakula duni kwa Wadigo ambao hupika vyakula aina mbalimbali na ambavyo huwa vimetiwa viungo. Wadigo hawaithamini sana sima kama vyakula vingine lakini kwa sababu ya umasikini inawalazimu wale vivyo hivyo.

Maudhui hayo ya umasikini pia yako katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu kwa maana kuwa yanajitokeza katika jamii zote mbili. Tuseme jamii hizi mbili ni za watu wasiojiweza kimaisha.

*1. Tumasikini hatuna kitu*

*Ela mbelee ndo kazi yetu*

*Twatengeneza vyungu ndo tupate sima.*

*2. Sijaona samaki kutiwa maembe*

*Na kumbe vile kutiwa kisha ikaingizwa thembe.*

*Haifai ni churuzu inga maguu ya ng'ombe.*

(Waswahili, wanapofinyanga vyungu)

Nyimbo hizi mbili huimbwa na wanawake Waswahili wa Jomvu Kuu wanapokuwa wakifinyanga vyungu. Maneno katika nyimbo hizi yanaashiria umaskini walio nao kama wenzao Wadigo wa Msambweni. Wafinyanzi wanataja wazi kuwa wao ni maskini wasiokuwa na chochote. Vile vile, katika wimbo huu wa pili, wafinyanzi wanasema kuwa wanakosa kutumia viungo wanapokuwa wakiandaa samaki kwa sababu ya umaskini. Umasikini wa Waswahili wa Jomvu Kuu unajitokeza wanapoimba pia kuwa inawalazimu kutembea kwa miguu kwa mwendo wa saa zima ili wasiharibu pesa zao kwa tikiti hata ya kupanda matatu. Vile vile, katika wimbo huu wa kutembea kwa miguu, Waswahili wanasema kuwa Jomvu ina mashimo na hili linaonyesha hali ya umaskini. Waswahili wanaonyesha kuwa wanashindwa hata kutengeneza mahali pao pakawa barabara zilizonyooka kwa sababu ya umaskini wao. Ni kwa sababu hii ambapo tunasema kuwa maudhui ya umaskini yanajitokeza katika nyimbo za hodiya za Wadigo na Waswahili vile vile.

#### **4.1.2 Ushirikiano**

Nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu zinaangazia maudhui ya ushirikiano vile vile. Kutokana na nyimbo zao za hodiya, jamii hizi mbili zinaashiria kuwa wao hufanya kazi kwa ushirikiano mathalan katika kazi ya ukulima, uvuvi, kutwanga na kusaga mahindi pia. Maudhui ya ushirikiano katika nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu yanajitokeza katika nyimbo zifuatazo:

*1. Pweza kamwambie ngisi tupite tukimaizi*

*Maji yakiacha mwamba tutwafutwao ni sisi.*

*Ngisi twaache tupite.*

*2. Hapa na Jomvu si mbali.*

*Mwendo wa saa moja na mbele kuna kiwiko*

*Twendeni mkiningoja. Usikengwe ni kanuke*

*Mwana kumuiza koja*

Nyimbo hizi zinaonyesha ushirikiano wa Waswahili wa Jomvu Kuu katika nyimbo zao za kazi. Katika wimbo wa kwanza, wavuvi huimba wanapokuwa wakivua kuonyesha kuwa wao ni watu walio na malengo sawa na hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano ili waweze kuyatimiza. Malengo yenye ni kuvua samaki wengi kwa kuwa ndio kazi inayowalisha na hata kuavisha. Katika wimbo wa pili, Waswahili wa Jomvu Kuu wanaonyesha kuwa wao huenda kwa mwendo wa saa zima kwa miguu wakingojana. Hii ina maana kuwa wao hutembea kwa pamoja bila kumwacha yejote aliye safarini nyuma, iwe kwamba amechoka, basi watamsubiri na kutembea huku wakitiana moyo kuwa Jomvu sio mbali. Vile vile Wajomvu hushirikiana katika kazi zao za uvuvi, ufinyanzi na kusaga mahindi. Ushirikiano wao vile vile unajitokeza wanaposema kuwa wanajifunga vibwebwe wakite na hema.

Wadigo nao huonyesha ushirikiano wao wakifanya kazi zao za kulima, kutwanga na kusaga mahindi kupitia nyimbo zao za kazi. Wadigo hushirikiana kuhakikisha kwamba kazi zinafanywa kwa pamoja na kuisha kwa haraka na kwamba ni kazi nzuri. Hata uvuvini, Wadigo wanashirikiana kwa kuwa ni vigumu sana kwa mvuvi mmoja kufanya kazi pekee yake kwa maana kuwa wanahitaji kusaidiana. Nyimbo zao ambazo zinadhahirisha ushirikiano ni kama vile:

1. Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake  
kumee magugu na nyasi.

Wapokezi: kumee magugu na nyasi,  
magugu na nyasi

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake  
kumee magugu na nyasi.

Wapokezi: kumee magugu na nyasi,  
magugu na nyasi

Mwongozaji: Atakaye pumzika shambani kwake

kumee magugu na nyasi.

## 2. Mwongozaji: Kisu kilipotea nyumbani kwa mganga

Ooh wee! Kilipotea nyumbani

Nyumbani we mganga

Kumekuchaa wee! Kumekucha

Mama kumekucha

Kijembe kinalima mchanga

Ha! Ha! Ha!

Wapokezi: Kijembe kinalima mchanga x 3

Nyimbo hizi mbili zinaashiria kuwa Wadigo wa Msambweni hushirikiana katika kazi ya ukulima. Wadigo kama walivyo Waswahili, wamedhihirisha kuwa wao hufanya kazi zao zote kwa ushirikiano. Nyimbo zao pia zinaashiria umuhimu wa ushirikiano ambapo wanasema kuwa atakayepumzika ataathirika kwa shamba lake kumea magugu. Hii ina maana kuwa kila anayelima anapaswa kufuata kasi ya wengine ili asiathirike. Vile vile, tabia ya kuamshana inaonyesha ushirikiano. Kila mmoja anakumbushwa kuwa kumekucha na hivyo basi ni aamke wakafanye kazi shambani wasije wakang'atwa na njaa.

### 4.1.3 Bidii na Kukashifu Uvivu

Kunayo pia maudhui ya kukashifu uvivu katika jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu ambayo pia yako katika jamii ya Wadigo wa Msambweni. Jamii hizi mbili zinaonyesha kuwa wanachukia uvivu kupitia kwa nyimbo zao za hodiya. Kwa hivyo wanapokuwa wakifanya kazi mara kwa mara wanaonekana wakiimba nyimbo za kazi ili kuhimiza wale wanaonekana walegevu au wanaozembea kazini. Waswahili wa Jomvu Kuu wanapokuwa wakitwanga, wanaimba nyimbo kama ‘kinu twanga’ ambapo wanajipa nguvu ya kufanya kazi hiyo. Vile vile, wanawake hawa wanadai kuwa wao hujifunga vibwebwe kwa nia ya kukita mahema wakati wa sherehe. Hii ni kazi ya kufanywa na wanaume lakini wao huifanya wenyewe ili wafanye shughuli zao zingine. Hali ya wanawake kufanya kazi ya kukita mahema na ambayo ni kazi ya wanaume inaonyesha kuwa wao

sio wavivu na wanaweza wakaifanya kazi yoyote ile. Nyimbo zifuatazo ndizo zina maudhui ya bidii na kukashifu uvivu kwa Waswahili wa Jomvu Kuu:

*1. Mwenyewe natwanga kinu change*

*Sitaki shari Memwatani*

*Kifunge kaniki kinu change*

*Mi natwanga kwa kishindo*

*Kisha natwanga kwa kishindo*

*2. Nina maneno wee nina maneno ntaka sema*

*La kwanza tulikite hema*

*La pili wanajifunga vibwebwe wawe na hema.*

*La tatu kunakuja Warabu wadai watumwa*

*We tumchezee Kalifa bin Helesi.*

Wadigo wa Msambweni pia wanayo maudhui ya bidii na kukashifu uvivu. Wanapokuwa wakifanya kazi ya kulima huimba ‘endakala nyuma ndiye gonzi’, kisha ‘enda oya mlumewe ni bobolofu’. Nyimbo hizo humtia mtu machungu ya kurejelewa kama mvivu. Kwa hivyo anayerejelewa katika wimbo husika hujikaza asionekane mvivu na kuwa chanzo cha kuwarudisha wenzake nyuma hasa katika kazi zinazofanywa kwa ushirikiano. Mfano wa wimbo unaoonyesha maudhui ya bidii na kukashifu uvivu kwa upande wa Wadigo wa Msambweni ni ufuatao:

Mwongozaji: Atakaye choka mume wake

Hana faida x 3

Bavyaa

Wapokezi: Anatembea na kicheko

Mwongozaji: Mavyaa

Wapokezi: Anatembea na kicheko

Mwongozaji: Shemegi yake!

- Wapokezi: Anatembea na kicheko  
 Mwongozaji: Shangazi yake  
 Wapokezi: Anatembea na kicheko  
 Mwongozaji: Atakayechoka mume wake  
                   hana faida x 3  
                   wazazi wake wanatembea na kicheko

Wanawake wanapouimba wimbo huu wananaua kukashifu uvivu na kuhimiza kuwepo kwa bidii mionganini mwao. Wimbo huu unaonyesha kuwa mwanamke mvivu huletea jamaa wake wote fedheha. Hii ndio maana wanauimba wimbo huu kukashifu uvivu ambao huifanya jamii ya mhusika kuchekwa kila wanapopita. Kwa kuimba wimbo huu, basi hakuna atakayetaka kuipatia jamii yake fedheha na hivyo basi atajikaza pia kama wenzake. Nyimbo za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu zinaonyesha kuwa huimbwa pia kwa ajili ya kukashifu uvivu katika jamii.

Maudhui ya biashara na busara pia yanajitokeza katika nyimbo za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu ni wachuuzi wa tembo, samaki na vyungu. Nyimbo zao za kazi zinaonyesha maudhui ya biashara. Nyimbo, ‘Unatembo tamu wee’ na ‘Wazungu walitizama gadeni kisha wapige picha wazitume ulaya’ zinaonyesha kuwa wao ni wafanyabiashara na kwamba riziki yao inatokana na kuuza tembo, samaki na kisha kutoka kwa watalii ambao huwa Wazungu. Biashara yao pia inahusisha uuzaaji wa vyungu ndio wapate pesa za kujikimu kimaisha. Yote yanaonyesha maudhui ya biashara. Wadigo wa Msambweni nao pia wanachuuza makuti, wanaauza samaki na tembo ili wapate chakula. Jamii hizi mbili ni watu wa kufanya biashara kama inavyobainika katika nyimbo zao.

Kutokana na nyimbo ambazo tumezirejelea katika utafiti huu, ni wazi kuwa jamii zote mbili zinadhahirisha maudhui ya busara. Jamii hizi mbili huwasilisha ujumbe kwa walio wavivu au wanaokwenda kinyume na kaida za jamii kwa kutumia busara. Busara hii inadhahirika katika nyimbo zao ambazo zina ujumbe muhimu kwa wanaokwenda kinyume na matakwa ya jamii husika. Wadigo wa Msambweni wanatumia busara kuambizana maneno. Katika wimbo wa ‘kata nguo,’ watu wanahimizana kuwatunza wazazi kwa kuwanunulia nguo za thamani ili wasionekane wenye huzuni mbele za wazazi wengine. Vile vile Wadigo wa Msambweni hutumia busara katika

kuambizana mambo ya dini mtu anapoonekana akifanya zinaa huhimizwa afunge ndoa za halali kupidia nyimbo za hodiya.

Waswahili wa Jomvu Kuu nao wanaonyesha busara zao hata kwa kupidia nyimbo zao za kazi. Wao hutumia tembo kama kinywaji cha kawaida. Hata katika nyimbo zao za kazi husifiana na mtu kujisifu kwa kutumia wimbo ‘unatembo tamu we’. Hii inaonyesha kuwa huwa wanatumia busara katika kuwasilisha sifa ya tembo kwa wateja wao. Busara hii pia inadhihirika wanaposema kuwa wanaauza maji ya mnazi badala ya kutumia neno tembo ambalo limeharamishwa. Kwa hivyo basi, tunaweza kusema kuwa Wadigo na Waswahili huwasilisha ujumbe kwa jamii kupidia nyimbo ambazo huimbwa wakati wa kufanya kazi ili kukashifu tabia mbalimbali hasi. Hii ni busara kwa kuwa wanaofanya kazi wataimba na kisha ujumbe wao utaeleweka na warejelewa amba wanatakiwa kubadilisha tabia inayokashifiwa na wimbo husika. Matumizi ya nyimbo katika kukashifu tabia mbaya katika jamii ni busara badala ya kugombana.

#### **4.2 Kulinganua Maudhui Yanajitokeza katika Nyimbo za Hodiya za Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni**

Tumeshughulikia maudhui ambayo yanalingana katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu hapo juu. Tumeonyesha kuwa maudhui sita yanajitokeza katika jamii zote mbili na ambayo ni: umaskini, ushirikiano, kukashifu uvivu, biashara na busara. Hata hivyo, kutokana na data ya utafiti wetu, tumegundua kuwa yapo maudhui ambayo yanajitokeza katika nyimbo za jamii moja na kukosekana kwa nyingine kama tunavyoonyesha katika sehemu hii.

##### **4.2.1 Maudhui ya Ulafi**

Maudhui ya ulafi yanajitokeza tu katika nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Maudhui hayo ya ulafi yanadhihirika kwenye nyimbo za kazi ya ukulima. Wakulima wanaimba kuwa wapo watu wengine hufanya uroho na uchoyo wakati wa kula chakula. Wimbo wenyewe unasema kuwa watu hawa hula kwa ulafi bila kuwajali wenzao. Wakati watu wanapolima huimba wimbo unaosema kuwa Abdalla Mwijaa Asifanye uchoyo kwa kuwa watu wote ni ndugu na wanastahili kula chakula pamoja. Vile vile, maudhui hayo yanapatikana kwenye wimbo wao wa kazi ya ufinyanzi ambapo watu wanatahadharishwa kufunika vyungu vyao maana paka wa mwingo ni mwizi. Sio paka tu anayetajwa bali wanaonyesha kuwa kuna mtu mlafi na mroho wa

chakula ambaye anakisiwa kula chakula peke yake. Vile vile, wimbo ‘wakanye watoto wasifanye kondo kwa sababu watu wa Jomvu Kuu ni watu wanaoishi kama ndugu’ unaonyesha ulafi na uroho. Watu ambaao ni walafi wanarejelewa kama ‘paka’ katika jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Kwa hivyo wimbo huu unakashifu ulafi na hakuna ambaye angependa kuitwa paka kutokana na ulafi wake. Kwa hali hii basi, wimbo huu unawakashifu wale ambaao hula bila kuwajali wengine. Maudhui haya ya ulafi hayajitokezi katika nyimbo za kazi za jamii ya Wadigo wa Msambweni.

#### **4.2.2 Maudhui ya Uvumilivu**

Maudhui ya uvumilivu yanabainika katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu ila hayapo katika jamii ya Wadigo wa Msambweni. Kutokana na wimbo wa Waswahili wa Jomvu Kuu unaosema kuwa ‘Tumasikini hatuna kitu’ ni kweli kuwa wao huvumilia kwa kuamini kuwa siku moja hali yao itabadilika na kuwa na afadhali. Wajomvu pia wanaimba kuwa wanavumilia kuishi Jomvu Kuu kwa kuwa imeja mashimo, wanavumilia umasikini wakula sima, ambapo wangekuwa na uwezo wasingekula sima tu wala kuishi Jomvu Kuu ya mashimo. Waswahili hawa wa Jomvu Kuu vile vile wanaonyesha kuwa wanalazimika kuvumilia mazingira duni kwa sababu ya umasikini. Maudhui haya ya uvumilivu hayajitokezi kwenye nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni. Hii inaonyesha kuwa Waswahili wa Jomvu Kuu wanahimiza uvumilivu mionganoni mwa wanajamii huku wakiwa na matumaini kuwa hali yao ya umaskini itabadilika wakati mmoja.

Kwa upande wa Wadigo wa Msambweni, maudhui ya umuhimu wa kupata chakula yanajitokeza. Jamii ya Wadigo inahimiza umuhimu wa kupata chakula kupitia kwa nyimbo zao za hodiya. Wadigo wanawataka watu kufanya kazi kwa bidii ili chakula kisikosekane manyumbani mwao. Wadigo wanaimba kuwa ‘kusaga viunga vichache’ kwa maana kuwa kuna haja ya watu kufanya kazi kwa bidii ili wapate chakula kingi baadaye ikilinganishwa na wakati huo ambapo chakula ni kidogo. Wadigo pia wanapoimba nyimbo za kimai zinaonyesha kuwa ni muhimu kutia bidii ili kusikosekane chakula nyumbani. Nyimbo hizi za hodiya za Wadigo wa Msambweni zinabainisha kuwa wao hawataki kuvumilia umasikini na hasa ukosefu wa chakula kama wenzao Waswahili wa Jomvu Kuu. Maudhui ya umuhimu wa kupata chakula hayapo kwenye nyimbo za Waswahili wa Jomvu Kuu. Wadigo wanahimizana wafanye kazi kwa bidii ili wapate chakula ndipo wawe na utulivu manyumbani mwao.

#### **4.2.3 Maudhui ya Heshima**

Vile vile nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni zinaonyesha maudhui ya heshima na stara ambapo maudhui hayo hayapo kwenye jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Wadigo wa Msambweni wanasisitiza heshima na stara kwa wakaza wana, mabinti na hata wazee. Wanawake Wadigo huimba nyimbo wanapokuwa wakitwanga au kusaga mahindi huku wakiimba kukashifu tabia ya mavyaa ya kutomheshimu mkaza-mwana. Katika wimbo huu wa mavyaa kumkosea heshima mkaza-mwana wake, waimbaji wanaauliza iweje wa kwanza na wa pili wanaondoka wote tu kisa na maana ni mavyaa. Wimbo huu unamtaka mavyaa kumheshimu mke wa mtoto wake wa kiume ili wasije wakaondoka na hatimaye mvulana abaki bila mke. Wimbo wa ‘kimbelembele Fatuma tumbo limbele’ pia unaashiria umuhimu wa kujiheshimu. Wimbo huu unamtaka msichana kujiheshimu asije akajihuisha na mahusiano ya kimapenzi kabla hajaolewa kiasi cha kutungwa mimba akiwa nyumbani kwao. Wimbo huu pia unakashifu tabia ya mahusiano ya kimapenzi baina ya watu ambao ni wa ukoo mmoja. Kulingana na Wadigo, mahusiano ya kimapenzi kati ya msichana na ndugu yake ni mwiko. Kwa hivyo wanawataka wasichana na wavulana wajiheshimu na waheshimu mila na tamaduni zao.

#### **4.3 Hitimisho**

Katika sura hii, tumelinganisha na kulinganua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Katika kulinganisha tulipata ya kwamba kuna maudhui matano ambayo yanadhihirika katika nyimbo za hodiya za jamii zote mbili, nayo ni: umasikini, ushirikiano, bidii na kukashifu uvivu, biashara na busara. Maudhui haya matano yanajitokeza katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Katika kulinganua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii hizi mbili, tumegundua kuwa Wadigo wana maudhui kama vile umuhimu wa kupata chakula na heshima ambayo hayapatikani katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu. Kwa upande mwingine, Waswahili wa Jomvu Kuu huwasilisha maudhui kama vile uvumilivu na ulafi na uroho ambayo hayapatikani katika hodiya za Wadigo wa Msambweni. Ni kwa sababu hii ambapo tunasema kuwa japo Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu ni majirani wana nyimbo ambazo zinawasilisha maudhui yanayotofautiana. Hata hivyo, maudhui matano yanafanana katika nyimbo zao za hodiya. Tumeonyesha kuwa licha ya kuwa jamii hizi mbili ni majirani, nyimbo zao za hodiya zinatofautiana kiujumbe yaani kila jamii ina wimbo wake.

Mathalan, wakulima Wadigo wana nyimbo zao huku Waswahili amba ni wakulima pia wakiwa na zao. Hali hii inajitokeza katika kazi zote. Tumeonyesha kuwa jamii hizi mbili zinafanya kazi kama vile ukulima, uvuvi, kugema, kutwanga mahindi na kusaga mahindi. Hata hivyo jamii hizi mbili zina nyimbo zao zinazoimbwa wakati wa kufanya kazi hizi.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI**

#### **5.0 Utangulizi**

Madhumuni ya sura hii ni kutoa muhtasari wa matokeo yote yaliyojitokeza katika utafiti wetu. Katika utafiti wetu tulijikita katika uchambuzi linganishi wa maudhui ya nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Kwa mujibu wa data ya utafiti wetu tumeonyesha kuwa Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu huwa na nyimbo za hodiya ambazo huimbwa wanapofanya kazi mbalimbali. Tumeonyesha kuwa kila jamii huwa na nyimbo zake ambazo huimbwa wakati wa kufanya kazi kama vile uvuvi, ukulima na hata ugemaji. Katika sura hii, tunashughulikia tathmini ya maswali ya utafiti wetu na kuangazia iwapo yanaingiliana au kutofautiana na malengo yetu. Tumetoa pia mapendekezo kwa watafiti wa baadaye kuhusiana na mada ya utafiti huu. Hatimaye tumeangazia changamoto tulizokumbana nazo wakati wa kufanya utafiti huu.

#### **5.1 Muhtasari wa Utafiti**

Katika sura ya kwanza ya utafiti wetu tuliangazia utangulizi ambaa ulishughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, msingi wa nadharia, sababu za kuteua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti na mbinu za utafiti kwa ujumla. Katika sura ya pili tuliangalia nyimbo mbalimbali za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Kwa ujumla tuliangalia nyimbo kumi na nane kila jamii. Tulielezea hizo nyimbo za hodiya za jamii mbili kwa kujikita katika kazi ya ukulima kwa jamii zote mbili, kazi ya uvuvi kwa jamii zote mbili, kazi ya kutwanga na kusaga mahindi, kazi ya usukaji wa makuti kwa jamii ya Wadigo na kazi ya ufinyanzi kwa jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Vile vile, tuliangalia kazi ya kugema ambayo hufanywa na wanaume wa jamii zote mbili.

Sura ya tatu, tuliangazia maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika hizo nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Katika kuainisha maudhui yaliyojitokeza na tuliyoyachunguza ni pamoja na umasikini, bidii na kukashifu uvivu, biashara, busara na ushirikiano, uvumilivu na ulafi kama yanavyobainika katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Tumelinganisha na kulinganua maudhui

haya katika sura ya nne ambapo tumepata kuwa yapo maudhui ambayo yanalingana katika nyimbo za kazi zinazoimbwa na jamii zote mbili na pia zipo tofauti kidogo tu. Katika kulinganisha, tulipata kuwa maudhui ya ushirikiano, bidii na kukashifu uvivu, umaskini, biashara na busara yanajitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii zote mbili. Kwa upande mwingine, yapo maudhui yanayotofautiana katika nyimbo za hodiya za jamii moja hadi nyingine. Nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni zina maudhui ya umuhimu wa kupata chakula na heshima ambayo hayapatikani katika jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Vile vile jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu huimba pia nyimbo za hodiya ambazo zinadhihirisha maudhui ya uvumilivu na ulafi na ambayo hayapatikani katika jamii ya Wadigo wa Msambweni. Kwa ujumla ni kuwa katika sura ya nne, tulifanya utafiti wetu kwa madhumuni ya kuangalia iwapo kuna usawa au tofauti kati ya maudhui ya nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni. Kulingana na maudhui yaliyojitekeza wakati wa utafiti wetu inaonyesha wazi kwamba jamii hizi mbili zina maudhui yanayokaribiana sana, kwani mengi ya maudhui ya nyimbo zao yanadhihirisha hali duni ya umasikini walio nao, ushirikiano, bidii na kukashifu uvivu katika jamii na hata biashara kwa jamii zote mbili.

Vile vile katika kuyachambua maudhui yanayopatikana katika nyimbo za hodiya za Wadigo na Waswahili tulielekezwa na nadharia ya uhalisia ambayo imejikita katika kuangalia mwanadamu na mazingira anamoishi. Nadharia hii ya uhalisia imetusaidia katika kuelezea hali ilivyo katika jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni na mazingira wanamoishi ili kutupa maudhui tuliyoyapata. Nyimbo za jamii hizi mbili zinadhihirisha hali halisi inayojitekeza katika jamii za Wadigo na Waswahili. Kwa mfano, upo wimbo wa Waswahili wa Jomvu Kuu unaosema kuwa kuna mashimo Jomvu. Wimbo huu unataja kuwa barabara za Jomvu ni mbaya kamwe ila hawana budi kuvumilia hali yao.

Tuliongozwa na madhumuni manne katika utafiti huu na ambayo ni: kuchunguza usawa uliopo baina ya maudhui ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, kubainisha tofauti za kimaudhui zilizopo kati ya nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, kueleza jinsi dini ya Kiislamu inavyojitekeza katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni, na kufafanua namna ushirikiano na ujirani kati ya jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni unavyoathiri nyimbo zao za kazi. Madhumuni haya tumeyashughulikia katika sura ya pili, tatu na ya nne. Kwa muhtasari

ni kuwa tulitaka kulinganisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni ambao ni majirani. Ni kweli kwamba huo ujirani na ushirikiano wa jamii hizi mbili umeathiri hata nyimbo zao za kazi kwani tumeona kuwa maudhui mengi yanafanana.

Utafiti wetu ulikuwa wa nyanjani na kwa hivyo basi tuliwazuru wanajamii wa jamii za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Tuliwatafiti wazee walio na umri wa zaidi ya miaka hamsini kwa kuwa ndio walio na ufahamu wa nyimbo zao za kazi. Tulitumia mbinu ya uchunguzi-shiriki na kurekodi walipokuwa wakiimba. Baadaye, data iliyokuwa imepatikana tuliinakili katika kitabu na hatimaye kuichanganua kinathari.

## **5.2 Mahitimisho ya Utafiti**

Utafiti huu ulinuia kulinganisha na kulinganua maudhui katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Tuliongozwa na madhumuni manne na ambayo tunayatolea mahitimisho katika visehemu vifuatavyo:

### **5.2.1 Usawa Uliopo baina ya Maudhui ya Nyimbo za Hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni**

Matokeo ya utafiti wetu yanaonyesha kuwa yapo maudhui yaliyo sawa katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Tuligundua kuwa maudhui ya ushirikiano, bidii na kukashifu uvivu, biashara, busara na umaskini yanadhihirika katika nyimbo za jamii zote mbili. Nyimbo za kazi ambazo tuliziangazia zinaonyesha kuwa maudhui haya yanajitokeza kwa Wadigo na kwa Waswahili vile vile. Ulinganisho huu tuluijadili katika sura ya nne.

### **5.2.2 Tofauti za Kimaudhui Zilizopo Kati ya Nyimbo za Hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni**

Data ya utafiti huu pia imedhihirisha kuwa yapo maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za hodiya za jamii moja na kukosekana kwa nyingine. Tuligundua kuwa jamii ya Wadigo wa Msambweni wana nyimbo za hodiya zilizo na maudhui ya umuhimu wa kupata chakula na heshima ambayo hayapatikani katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu. Kwa upande mwingine, Waswahili wa Jomvu Kuu wana nyimbo za hodiya zilizo na maudhui ya uvumilivu na ulafi

ambayo hayapo katika hodiya za Wadigo wa Msambweni. Tofauti hizi tumezishughulikia pia katika sura ya nne.

### **5.2.3 Kueleza jinsi Dini ya Kiislamu Inavyojitokeza katika Nyimbo za Hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni**

Tumeonyesha kuwa nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu zinaonyesha maudhui ya dini kwa uchache sana na ndio sababu hatujayashughulikia kwa kina. Dini ya Kiislamu inajitokeza ambapo vijana wanaimbiwa waoe kuliko kuhusiana kimapenzi kabla ya ndoa, jambo ambalo ni kinyume na taratibu za dini ya uislamu. Vile vile, wimbo huo unaonyesha maudhui ya dini unaashiria kuwa wanaojamiihana kabla ya ndoa watahukumiwa kesho ahera kwa kosa hili. Wimbo huu unadhihirisha taratibu za dini ya Kiislamu hasa kuhusiana na mahusiano baina ya watu ambao hawajaoana bado. Katika nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu, maudhui ya dini yanajitokeza pale ambapo wanatumia neno ‘tembo tamu’ kwa kuwa linaruhusiwa kunywewa na dini yao. Dini yao hairuhusu matumizi ya pombe ambayo hutokana na tembo kufanywa kuwa chachu na hivyo linalewesha. Kwa hivyo basi, tunaweza kusema kuwa nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni hayazingatii sana maswala ya dini.

### **5.2.4 Kufafanua namna Ushirikiano na Ujirani kati ya Jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu na Wadigo wa Msambweni Unavyoathiri Nyimbo zao za Kazi**

Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu ni majirani ambao wanakaa katika eneo moja la pwani ya Kenya. Jamii hizi mbili zinafanya kazi ambazo zinafanana isipokuwa ufinyazi ambao hufanywa na wanawake Waswahili wa Jomvu Kuu na haufanywi na wanawake wa Kidigo. Vile vile kazi ya kusuka makuti hufanywa tu na wanawake wa Kidigo na haifanywi na wenzao Waswahili. Kazi za uvuvi, ukulima, kugema, kusaga mahindi na kutwanga mahindi hufanywa na jamii zote mbili. Wanaume wa jamii zote mbili hufanya kazi ya kugema na uvuvi huku kazi za kutwanga na kusaga mahindi zikifanywa na wanawake wa jamii zote mbili. Kazi ya ukulima inafanywa na wanaume na wanawake wa jamii zote mbili. Hata hivyo, Wadigo wa Msambweni wametunga nyimbo zao za hodiya ambazo zinatofautiana na za Waswahili wa Jomvu Kuu. Kama tulivyoonyesha katika sura ya nne, maudhui matano yanafanana katika nyimbo za hodiya za jamii hizi mbili. Hii inaonyesha kuwa ushirikiano baina yao umeweza kuwaathiri kiasi cha kufanya

biashara za aina moja kama vile kuuza samaki na tembo. Vile vile, wameathiriana kikazi ambapo kila jamii inahimiza ufanyaji kazi kwa bidii kuptitia kwa kuimba nyimbo za hodiya zinazokashifu uvivu na kuhimiza ushirikiano baina ya wanajamii.

### **5.3 Changamoto za Utafiti**

Utafiti wetu ulikumbwa na changamoto nyingi sana. Utafiti wetu ilibidi uchelewe kukamilika kwa sababu ya ugonjwa wa msambao wa korona. Ilikuwa vigumu kuwatemebelea wakaaji wa maeneo lengwa kwa sababu ya hofu ya kuambukizana maradhi haya ya korona hasaa tukizingatia ya kwamba maeneo ya Jomvu Kuu ndio maeneo yaliyoathirika kabisa na maradhi hayo kwa sababu ya msongamano wa watu. Changamoto ya pili ni kwamba wazee wengi walio na uelewa wa kazi hizi wengi wameaga dunia. Ilitubidi tutembee sana tukitafuta watu wenyewe umri wa miaka hamsini na zaidi ndio waweze kutuimbia nyimbo hizi za kazi za jamii hizi mbili. Hii ilisababishwa na kwamba watu siku hizi hawaimbi hizi nyimbo maana kazi zao zinafanywa na mashine. Changamoto nyingine ni ya kifedha. Mimi mwenyewe imekuwa vigumu kupata fedha za kufanya nauli ya kutembea huko kote nilikolenga ndio maana utafiti wetu umechelewa. Vile vile, wale watu niliokusudia kuwatumia kuniimbia hizo nyimbo walitaka malipo. Walidhani ya kwamba kuna shirika ama serikali ilinituma hivyo walidhani nilipewa pesa nyingi na hilo shirika, kwa hivyo wakawa wagumu kunisaidia kwa vile walitarajia malipo. Waliona mimi nitapata pesa nyingi sana ilihali haikuwa hivyo. Mbali na hizo changamoto zote tulizokumbana nazo, tuliweza kukusanya nyimbo thelathini na sita katika hizo jamii mbili na kuweza kuzifanyia utafiti kwa kuzichanganua kimaudhui.

### **5.4 Mapendekezo**

Utafiti wetu ulijikita katika uchambuzi linganishi wa maudhui ya nyimbo za hodiya za jamii ya Wadigo wa Msambweni na nyimbo za hodiya za jamii ya Waswahili wa Jomvu Kuu. Tumeona kuna mwingiliano mkubwa wa kimaudhui baina ya nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu. Tungependekeza kuwa,

- i. Tafiti zingine zifanywe juu ya uchambuzi linganishi wa fani na mtindo katika nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Hili lilitokana na kwamba kipengele cha fani hakikutafitiwa.

- ii. Tungependekeza tafiti nyingine zifanywe kuhusiana na kuchunguza lahaja ya Kijomvu kuona hasa kama ingali inatumika ama la katika nyimbo zao za hodiya. Kwani sisi utafiti wetu haukuegemea kwenye kuchambua lahaja iliyotumika katika nyimbo za hodiya tulizozitafiti.

## MAREJELEO

- Beja, K. (2001) *Giriama Funeral Songs. Functional Aesthetic Study: Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.*
- Dau, M. (2014) *Uchambuzi Linganishi wa Maudhui na Majukumu ya Nyimbo za Harusi za Wadigo na Waswahili. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.*
- Khatib, M. S. (1987) Taarab katika Fasihi Simulizi. *Katika Makala ya Semina ya Fasihi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam Uk. 16-25.*
- Kinoti, T. (2007) *Fasihi Simulizi na Utamaduni.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, P. (2007) *Phonological Theory, History and Development.* Dar-es-salaam: TUKE.
- Matei, A. K. (2011) *Fani ya Fasihi Simulizi.* Nairobi: Oxford University Press.
- Mjomba, G. (2001) *Uchambuzi wa Nyimbo za Harusi za Wadawida. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.*
- Mugambi, H. (2007) *Uchambuzi wa Nyimbo za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.*
- Njogu, K. na Wafula, M. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1990) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu za Uhakiki.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Spear, T. T. (1978) *The Kaya Complex.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Timammy, R. (2002) *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A Stylistic Analysis, Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.*
- TUKE (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar-es-salaam: Oxford University Press.
- Wafula, R. M. and Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi:* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitilia, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix publishers Ltd.

\_\_\_\_\_ (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

\_\_\_\_\_ (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

\_\_\_\_\_ (2008) *Kanzi ya Misingi ya Uchunguzi wa Fasihi* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

## **DATA YA UCHANGANUZI**

Tulikusanya nyimbo za hodiya za Wadigo wa Msambweni na Waswahili wa Jomvu Kuu. Tunawarejelea waliotusaidia katika utafiti huu na kisha tumeandika nyimbo za hodiya zinazojitokeza kwa Wadigo na Waswahili ambazo tulizitumia katika utafiti huu. Maandishi katika viambatisho hivi yamehifadhiwa katika hali yake halisi na lahaja iliyotumiwa katika nyimbo hizi za kazi.

### **Kiambatanisho 1**

Baadhi ya waliohojiwa kuhusu nyimbo za kazi za jamii ya Wadigo wa Msambweni.

#### **1. Mohamed Hamisi Dzenze**

Huyu ni mzee anayeishi katika kijiji cha mabatani. Ana umri wa miaka sabini. Kazi yake kubwa ni ya uvuvi. Alituimbia nyimbo za kazi ya uvuvi.

#### **2. Omari Mwitu**

Ni mzaliwa wa kijiji cha Milalani huko Msambweni. Ni mzee mwenye umri wa miaka sabini. Kazi yake kubwa ni ukulima. Alituimbia nyimbo za kazi ya ukulima.

#### **3. Halifani Omari Chimoche**

Huyu ni mkaaji na mzaliwa wa Msambweni Milalani. Kazi yake kuu ni kugema. Alituimbia nyimbo za kazi ya kugema.

#### **4. Hemedi Mwabazura**

Huyu ni mwanamume mwenye umri wa miaka sabini na tano. Alizaliwa Msambweni maeneo ya Vingujini. Yeye ni mvuvi wa miaka mingi. Alituimbia nyimbo za kazi ya uvuvi.

#### **5. Ndaro Mwandaro**

Huyu ni mkaaji wa Msambweni ya Mwaembe. Yeye ni mzee mwenye umri wa miaka sitini na tano. Kazi yake kubwa ni ya ukulima na kugema. Ni mtu mwenye ujuzi wa miaka mingi, alituimbia nyimbo za kazi ya ukulima na kazi ya kugema.

## **6. Mwanatumu Shughuli**

Huyu ni mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na tano. Ni mkaaji wa Msambweni ya Vingujini. Yeye alituimbia nyimbo za kazi ya kusuka makuti, kusaga mahindi na kutwanga.

## **7. Mwanamwema Rama**

Huyu ni mwanamke mwenye umri wa miaka sabini na ni mzaliwa wa Msambweni eneo la Mwaembe. Aliolewa hapo na sasa yuko na hata vitukuu. Yeye alituimbia nyimbo za kutwanga, kusaga na kusuka makuti.

## **8. Mchalika Chikarata**

Huyu ni mwanamke mzaliwa wa kitongoji cha Mabatani huko Mwaembe. Ni mama mjane aliyefiwa na mumewe hivi majuzi. Hata ingawa ni mzee sana, bado aliquwa na uwezo wa kutuimbia nyimbo za kutwanga, kusaga na kusuka makuti.

## **9. Mwanaisha Shabani**

Huyu mwanamke aliolewa Milalani. Kwao alikozaliwa ni Tiwi. Yuko na mji wake hapo Mabatani. Alituimbia nyimbo za kazi ya kusuka makuti.

## **10. Binti Omari Changoma**

Huyu ni mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na nane, anaishi Msambweni ya Mwaembe. Alituimbia nyimbo za kusuka makuti, kutwanga na kusaga mahindi.

## **Kiambatanisho II**

Wahojiwa wa nyimbo za hodiya za Waswahili wa Jomvu Kuu.

### **1. Mohamed Hassan**

Huyu ni mzee mwenye umri wa miaka sitini na tano. Alizaliwa Jomvu Kuu na kuishi huko Jomvu Kuu hadi sasa. Yeye ni mvuvi wa miaka mingi sana. Alituimbia nyimbo mbalimbali za wavuvi.

## **2. Mwinyikombo Juma**

Huyu ni mzee mwenye umri wa miaka sitini na moja. Yeye anaishi Jomvu Mikanjuni. Ni mvuvi mashuhuri. Yeye pia alituimbia nyimbo za aina mbalimbali za wavuvi.

## **3. Suleiman Omari**

Huyu ni mzee wa miaka sitini na tatu. Ni mkaaji wa Jomvu Madafuni. Yeye kazi yake hasa ni ya kugema. Alituimbia nyimbo za kazi ya kugema.

## **4. Swalehe Ali**

Huyu ni mzee mwenye umri wa miaka sitini na mbili. Yeye ni mzaliwa wa Jomvu Kuu. Kazi yake ni ya kulima. Alituimbia nyimbo za kazi ya kulima.

## **5. Sudi Jumaa**

Huyu ni mzee mwenye umri wa miaka sitini na tano. Yeye pia alituimbia nyimbo za wakati wa kulima.

## **6. Zaituni Omari**

Huyu ni mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na tano. Alizaliwa Jomvu Kuu na anaishi huko Jomvu Kuu. Yeye ni mfanyakazi wa jadi. Alituimbia nyimbo za kazi ya ufinyanzi.

## **7. Amina Suleiman**

Huyu ni mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na nane. Yeye anaishi Jomvu Mikanjuni. Alituimbia nyimbo za kazi ya kutwanga na kusaga mahindi za wanawake wa Jomvu Kuu.

## **8. Mwanamwinyi Abdalla**

Huyu ni mzaliwa wa Jomvu Misheni, ni mwenye umri wa miaka sitini na saba naye vile vile alituimbia nyimbo za hodiya za wanawake za kazi ya kutwanga, kusaga na kufinyanga vyungu.

## **9. Zulfa Ali**

Huyu ni mzaliwa wa Jomvu Misheni, ni mwenye umri wa miaka sitini na tano. Yeye alituimbia nyimbo za hodiya za wanawake za kazi ya kutwanga, kusaga na kufinyanga vyungu.

## **10. Bakari Hassan**

Ni mzaliwa wa Jomvu Madafuni aliye na umri wa miaka hamsini na sita. Yeye alituimbia nyimbo za hodiya za wavuvi.

### **VIAMBATISHO VYA NYIMBO ZA HODIYA ZA WADIGO NA WASWAHILI**

#### **Nyimbo za Wadigo Kazi ya Ukulima**

**1.** Mwongozaji: Endekala nyuma ndiye, gonzi gonzi baa x 2

Wapokezi: Gonzi wee baa,

Gonzi wee baa,

Gonzi wee baa,

Mwongozaji: Endekala nyuma ndiye,

Gonzi gonzi baa x 2

Wapokezi: Gonzi wee baa

Mwongozaji: Endekala nyuma ndiye

Gonzi gonzi baa x 2

Wapokezi: Gonzi wee baa x 2

**2.** Mwongozaji: Nanzala mayo nanzala

Narimira mariga wee

Nanzala mayo nanzala

Narimira mariga wee x 2

Wapokezi: Nanzala mimi nanzala

Narimira mariga wee

Nanzala mimi nanzala

Narimira mariga wee x 2

Mwongozaji: Nanzala mayo nanzala

Narimira mariga wee

Nanzala mayo nanzala

Narimira mariga wee

**3.** Mwongozaji: Chirumu changamika nyumbani

We mganga ooh wee! Changamika

Nyumbani we mganga

Kukachaa weeee kukacha

Mayo kukacha we chijembe

Chinaburuga mtsanga

Ha ha ha ha

Wapokezi: Chijembe chinaburuga

Mtsanga

Mwongozaji: Ha ha ha x 3

Wapokezi: Chijembe chinaburuga

Mtsanga x 3

### **Nyimbo za Hodiya za Wadigo za Kutwanga Nafaka**

**4.** Mwongozaji: Ndiye ooya mundawe

Naumere tsuchi na ndago

Wapokezi Tsuchi! Tsuchi! Na ndago

Mwongozaji: Ndiye ooya mundawe

Naumere tuchi na ndago  
Wapokezi                    Tuchi! Tuchi! Na ndago  
Mwongozaji:                Ndiye ooya mundawe  
                              Naumere tuchi na ndago  
Wapokezi                    Tuchi! Tuchi! Na ndago

**5.** Mwongozaji: Chibundani kakufipkwa kunani

Wapokezi:                kuchifipkwa kunadepkwa achetu  
Mwongozaji:              Chibundani kakufipkwa kunani  
Wapokezi:                kuchifipkwa kunadepkwa achetu  
Mwongozaji:              Chibundani kakufipkwa kunani  
Wapokezi:                kuchifipkwa kunadepkwa achetu

**6.** Mwongozaji: Yenderemwa mlumewe ni

                              bobo lofu x 3  
                              Ise vyala naye ni bobo lofu  
Wapokezi:                Ananyendeka na chitseko  
Mwongozaji:              Nine vyala  
Wapokezi:                Ananyendeka ni chitseko  
Mwongozaji:              Mlamuwe!  
Wapokezi:                Ananyenduka na chitseko  
Mwongozaji:              Shangazire  
Wapokezi:                Ananyendeka na chitseko  
Mwongozaji:              Yendremwa mlumewe ni  
                              bobo lofu x 3

Avyazie

Wapokezi: Ananyendeka na chitseko

**Nyimbo za Hodiya za Wadigo za Kusaga Mahindi**

7. Mwongozaji: Chimbere mbere Fatuma tumbo imbere x 2

Wapokezi: Kama ni hanzo kamuuze baba mdide

We mwenye wagunduliwa poreee

Fatuma poree

Mwongozaji: Naona ajabu Fatuma kulala na nduguyeee x 2

Wapokezi: chamba ni hanzo kamuuze baba mdide go

gakoo gagunduliwa poree Fatuma poree

8. Nasaga vidzunga uyangu mino reroo wee mino.

Nkalole mtsedza wangu. Mjeni achedza munjitire sima

Nkalole mtsedza wanguuu mjeru

Acheza m jitire sina x 3

9. Mwongozaji: Unaphaya phaya we mayo unaphaya

Wapokezi: Gomba usikirwe

Mwongozaji: phaya we mayo unaphaya

Wapokezi: Gomba usikirwe

Mpkwaza mwanaa wa mwanzo

Mpkwaza mwana wa mwanzo

Naye wahenda uka

Achisengera mbere

Ta yuyu wa phiri naye  
Wahenda gapuza puzaa  
Richa umbeye mayo vyala  
Richa umbeya  
Wapokezi: Gomba usikirwe  
Mwongozaji: Una nung'unung'u mayo vyala  
Una nun'gu nun'gu  
Gomba usikirwe

### **Nyimbo za Hodiya za Wadigo za Kusuka Makuti**

**10.** Mwongozaji: Sheria! Sheria!

Sheria mhondo Lungunzu x2

Wapokezi: Sheria mhondo Lungunzu  
  
Mayo yuno tsawe wahala  
  
Magana achigatiya nyumbani  
  
Kayafungula mwana kumanina  
  
Chivyere mwenehu usiende hivyo  
  
Sharia mhondo lungunzu

### **11. Chivyere wee! Nzala na ayao**

Mbona ikakuverera

Chivyere wee! Nzala na ayao

Mbona ikakuverera

Mwenye wataka mahari

Chiremba na maziya

Uchihewa tsetsetse

Ukamanya wee pha Kasimu

ziphapho chivyere wee

nzala na ayao mbona

ikakuverera!

**12. Nkaangirwaaa! Nkaangirwa**

Nkaangirwa mayo ho nkaangirwa

Mchetu wakoma mayo wee

Anahulwa mizigo

Anajita koma wee

Anahulwa mizigo

Analumwa inchitswa we

Anahulwa mizigo

Anavunzwa mongomongo we

Anahulwa mizigo

**Nyimbo za Hodiya za Wadigo za Uvuvi**

**13. Mwongozaji:** Richa Richa chiruwa

Cha matsere

Wapokezi: Maimbi hiya maimbi higo

Haya nabwa nago sawa

Wapokezi: Maimbi hiya maimbi higo

Haya nabwa nago sawa

Wapokezi: Maimbi hiya maimbi higo  
Haya nabwa nago sawa

Wapokezi: ukapata haya ukakosa haya  
Maimbi higo haya nabwa nago sawa

**14.** Mwongozaji: Chivyere ajenio hana haa

Wapokezi: Mayo rero haa rero akedzu  
Kanya mlomooo

Mwongozaji: Unachibako shaunvuo sino  
Idikedza tutamusana  
Unayanya ganya shabinado  
Sino ukedza tulamusane

Wapokezi: Tulamusane

Mwongozaji: Una uchoyo shaunyoo

Wapokezi: Sino ukedza tulamusane

**15.** Kata nguooo umphirikire maayo

Ye mwenye anazarai nyumbani kwa  
Chorirooo. Anaona haya aya ni  
bumu bumu. Kura ni mchina, kura ni chitenge  
Akachita gonga nyumbani phahi pkwa chirirooo

**Nyimbo za Hodiya za Wadigo za Kugema**

**16.** Mwongozaji: Naphiya mndani nkarinde maruwa kunde zinasira mlamu niendeze

Mpokezi: Niendeze mimi dede nkakala bung'o kurinda maruwa x 2  
Naphiya mndani nkarinde maruwa kunde zinasira mlamu niendeze  
Niendeze mimi dede nkakala bung'o kurinda maruwa x 2

Mwongozaji: Nkakala bung'o kurinda maruwa wee  
Rero narinda maruwa

**17. Juma lola lola dedee x 2**

Kurusa kuna tabu lola dedee  
Uchifikiri dini ahera kuna mambo  
Roho zindapheya x 2  
Mbere ya Mungu

**18. Naihwa ni mayooo**

Dzombo ni kuree  
N'tsape naphi ko  
Nyikaa kuna adzomba  
Naihwa ni mayoo  
Dzombo ni kuree  
Nitsape naphi ko nyikaa  
Kuna adzombaa

**Nyimbo za Hodiya za Waswahili za Uvvi**

**19. Pweza kamwambia ngisi tupite tukimaizi.**

Maji yakiacha mwamba tutafutwao nsisi.  
Ngisi tuache tupite.

**20. Jomvu si mbali**

Mwendo wa saa moja na mbele

Kuna kiwiko

Twendeni mkiningoja msikengwe

Ni Kanuke mwana kumuiza koja.

**21. ni nani**

Akaniitiye Swalehe, kero hakubwaga zani

Kucheza ngoma pekee

Kucheza ngoma pekee na jeuri tele

Utdadhani hana watu kero

Hukubwaga zani kucheza ngoma pekee.

**Nyimbo za Hodiya za Waswahili za Ukulima**

**22. Abdalla Mwijaa usifanye jeuri**

Ukafanya kama yule sote Jomvu

Tatu na tule. Ulafi na uroho sote tule

**23. Kuna Saidi Halifa na Saidi Barahashi**

Mzungu ataka ngome

Ngome ataipatapi

Asipate kwa nini na Saidi Halifa ako.

Hivyo Wazungu wanaeza pata ngome

Kwa ushirikiano wa Saidi Barahashi.

**24.** Karibuni wafalume, hii ndio Jomvu Kuu.

Jomvu yetu ya mashimo yatumiza maguu

Saidi wa Mbashiri, Mchangamwe mbeko,

Alimpiga mamaye kwa kipande cha ukoko.

**Nyimbo za Hodiya za Waswahili za Kugema**

**25.** Unatembo tamuu weee una tembo tamu

Unatembo tamu weee u mnazi wa jaka x 3

**26.** Na hii Fotijizazi ndo nyumba namba wani

Hata Wazungu wakija mpaka waingie ndani kisha watoke na nje waitizame gadeni

Na hii fotijizazi imepandwa na maua.

Ili Wazungu wakija, wapate kufurahia.

Kisha waipige picha waipieleke Ulaya.

**27.** Njooni Jomvu madafuni,

Misheni na hata Jomvu Kuu,

Mufurahie madafu, Maji ya mnazi,

Babangidaa Mwinyikombo mnywe maji ya madafu na mnazi.

**Nyimbo za Hodiya za Waswahili za Kusaga Mahindi**

**28.** Kibunzi mwakani tupite kwa juu

Hebu tupite kwa Pwani twende forodhani tukaoge

Babanda babanda singejila ndimi mwamlambaji

Fungu la njiwa kapata kibanda nijitie.

**29.** Hakimu Mwamadi na waziri Kombo,

Kamwambie Kombo awakanye watoto wasifanye kondo,

Tundugu moja eee

Twaingia Shela tuwarembo

Ni mnyama gani asiye na umbo x 2

**30.** Nina maneno wee nina maneno ntaka sema

La kwanza tulikite hema

La pili wanajifunga vibwebwe wawe na hema.

La tatu kunakuja Warabu wadai watumwa

We tumchezee Khalifa bin Helesi.

**Nyimbo za Hodiya za Waswahili za Ufinyanzi**

**31.** Sijaona samaki kutiwa maembe

Na kumbe vile kutiwa kisha ikaingizwa thembe.

Haifai ni churuzu inga maguu ya ng'ombe.

**32.** Mliolala amkeni mje mumake kimako

Paka wa mwingo ni mwivi

Kafunike chungu chako.

Mkoko una pevuka kalinoe shoka lako.

**33.** Tumasikini hatuna kitu ela mbeleee ndo kazi yetu

Twatengeza vyungu ndo tupate sima

Tumasikini hatuna kitu

Ela mbelee ndo kazi yetu.

## **Nyimbo za Hodiya za Waswahili za Kutwanga Mahindi**

### **34. Mambo na wenyewe wee**

Mambo na wenyewe

Wenyewe ni sisi

Natulikokote wee x 3

Ubela ubela

### **35. Mwenyewe natwanga kinu change**

Sitaki shari memwatani kifunge kaniki

Kinu changu ni mutwanga kwa kishindo

Kisha natwanga kwa kishindo

### **36. Kinuu kinu**

Kinu twanga

Mama akitwanga atwangaje

Nani nikatwanga kama yeye

Kinuu kinu

Kinu twanga